# Kiswahili

## Shule za Sekondari

## Kitabu cha Mwanafunzi

**Kidato cha Pili**




Taasisi ya Elimu Tanzania

Fot online use only
do not duplicate

# Kiswahili

## Shule za Sekondari

### Kitabu cha Mwanafunzi

### Kidato cha Pili

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 525

Jina la Chapisho: Kiswahili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Pili

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-268-0

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 10 Juni, 2021 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Kidato cha Pili katika ngazi ya Elimu ya Sekondari nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa mwaka 2005.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

Taasisi ya Elimu Tanzania

Fot online use only
do not duplicate

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2021

Kimechapishwa 2021

ISBN: 978-9987-09-268-0

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam - Tanzania

Simu: +255735041170/+255735041168
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

FOR ONLINE USE ONLY

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri, wala kutoa sehemu ya kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.



KISWAHILI FINAL.indd 2 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

# Yaliyomo

**Orodha ya Vielelezo** ........ iv

**Vifupisho** ........ v

**Shukurani** ........ vi

**Dibaji** ........ vii

**Sura ya Kwanza**

Dhana za msingi za sarufi maumbo ........ 1

**Sura ya Pili**

Uundaji wa maneno ........ 8

**Sura ya Tatu**

Matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ........ 13

**Sura ya Nne**

Uhakiki wa kazi za fasihi simulizi ........ 27

**Sura ya Tano**

Utungaji wa kazi za fasihi simulizi ........ 43

**Sura ya Sita**

Uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi ........ 61

**Sura ya Saba**

Uandishi ........ 67

**Sura ya Nane**

Usimuliaji ........ 89

**Sura ya Tisa**

Ufahamu ........ 96

**Faharasa** ........ 113

**Bibliografia** ........ 116

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI FINAL.indd 3 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

# Orodha ya Vielelezo

3.1: Aina za utata........................................................................23

4.1: Vipengele vya uhakiki wa fasihi simulizi........................................30

9.1: Ukurasa wa kamusi.........................................................................107

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI FINAL.indd 4 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| CKD | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| DUCE | Dar es Salaam University College of Education |
| LUKU | Lipia Umeme Kadiri Unavyotumia |
| MNMA | Mwalimu Nyerere Memorial Academy |
| NECTA | National Examinations Council of Tanzania |
| S.L.P | Sanduku la Posta |
| TAMISEMI | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TATAKI | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| TUKI | Taasisi ya Ukuzaji Kiswahili |
| UDOM | University of Dodoma |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UMISSETA | Umoja wa Michezo Shule za Sekondari Tanzania |

FOR ONLINE USE ONLY

Fot online use only
do not duplicate


# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki. Pia, TET inatoa shukurani kwa taasisi zote za umma na binafsi zilizoshiriki kwa namna moja ama nyingine katika kufanikisha uandishi wa kitabu hiki. Taasisi hizo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (CKD - DUCE), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Pia, TET inatoa shukurani kwa Vyuo vya Ualimu, Shule za Sekondari, na Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule.

Kipekee, TET inatoa shukurani za dhati kwa michango iliyotolewa na wataalamu wafuatao:

**Waandishi:** Bw. Tumaini M. Mahendeka, Bw. Adelgot J. Mapunda, Bi. Aurelia F. Mutajunwa, na Bw. Jailan M. Hafidhi (TET)

**Wahariri:** Dkt. Rehema O. Stephano (UDOM), Dkt. Zabron T. Philipo (UDOM), Dkt. Titus M. Ngeme (CKD), Dkt. Rajabu A. Chipila (CKD), Dkt. Edith B. Lyimo (CKD), Dkt. Luinasia E. Kombe (CKD - DUCE), na Bw. Mussa R. Kaoneka (BAKITA)

**Msanifu:** Bw. Sultan A. Tamba

**Wachoraji:** Bw. Fikiri A. Msimbe na Alama Art and Media Production Co. Ltd

**Mratibu:** Bi. Aurelia F. Mutajunwa

Pia, TET inatoa shukurani kwa walimu na wanafunzi wa shule za sekondari walioshiriki katika hatua ya ujaribishaji wa muswada wa kitabu hiki.

Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandishi na uchapaji wa kitabu hiki.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania


FOR ONLINE USE ONLY

Fot online use only
do not duplicate

# Dibaji

Kitabu hiki ni cha pili katika mfululizo wa vitabu vinne vya Somo la Kiswahili kuanzia Kidato cha Kwanza hadi Kidato cha Nne. Kimeandaliwa mahususi kwako mwanafunzi wa Kidato cha Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kitabu hiki kimeandaliwa kulingana na Muhtasari wa Somo la Kiswahili wa mwaka 2005 uliotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Maudhui yaliyomo katika kitabu hiki ni mwendelezo wa yale yaliyomo katika kitabu cha Kiswahili Kidato cha Kwanza.

Kitabu kimegawanywa katika sura tisa: Dhana za msingi za sarufi maumbo, Uundaji wa maneno, Matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali, Uhakiki wa kazi za fasihi simulizi, Utungaji wa kazi za fasihi simulizi, Uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi, Uandishi, Usimuliaji, na Ufahamu. Maudhui ya kitabu hiki yamewasilishwa kwa njia ya matini, kazi za kufanya, vielelezo, pamoja na picha. Yote haya yanalenga kuchochea ujenzi wa umahiri unaokusudiwa kwa kila sura. Vilevile, katika kila sura kuna mazoezi yenye lengo la kupima na kujenga uelewa na ujuzi wa somo hili. Hivyo basi, unapaswa kufanya mazoezi na kazi zote zilizomo kwenye kitabu hiki, pamoja na kazi nyingine utakazopewa na mwalimu.

FOR ONLINE USE ONLY

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

Fot online use only
do not duplicate

# Sura ya Kwanza

## Dhana za msingi za sarufi maumbo

### Utangulizi

*Katika lugha, maneno huwa na maumbo mbalimbali yenye dhima za kisarufi. Maumbo hayo huchunguzwa katika taaluma ya sarufi maumbo na huwakilishwa na dhana mbalimbali. Katika sura hii, utajifunza dhana za msingi za taaluma ya sarufi maumbo. Dhana hizi ni mzizi, kiambishi, mofu, na mofimu. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kubainisha na kuchanganua maumbo mbalimbali ya maneno ya Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, utajua maumbo ya maneno mbalimbali unayoyatumia katika mawasiliano ya kila siku na utayatumia vizuri zaidi.*

### Kazi ya 1.1

**Soma majigambo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

FOR ONLINE USE ONLY

**Mzizi:**
Mimi jabali la neno, mimi kiini cha neno,
Nimezibeba maana, tena za msingi sana,
Sifanani na kinyonga, kamwe sitabadilika,
Nani ananibishia, si mhimili wa neno?
Wasomi wanyambuapo, lazima wananibeba.

**Kiambishi:**
Wewe mzizi nyamaza! Tena ufunge mdomo,
Bila ya kuwapo mimi, maana za ziada huna,
Mimi ndiye nakupamba, kwa maana kemkemu,
Ninakuvika maana, hata kama u kiini,
Mimi ninakuwezesha, yafaa uniheshimu.

**Mofu:**
Mzizi na kiambishi, acheni yenu mizengwe,
Mimi umbo 'metulia, kwa bashasha nimetua,
Mzizi na kiambishi, bila umbo hamuishi,
Mimi ni mjenzi wenu, mwapaswa kunikubali,
Mzizi na kiambishi, nipeni yangu heshima.



KISWAHILI FINAL.indd 1 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Mofimu:** Nimewapa masikio, sasa mimi nimechoka,
Mzizi na kiambishi, nawe mofu tulieni,
Mimi huwapa maana, ili mpate yakini,
Bila kuwapo mofimu, nyinyi hamna maana,
Tafadhali heshimuni, yale ninayoyafanya.

**Mofu:** Mofimu sikia vyema, tena kwa makini sana,
Mofu mimi ninaitwa, vizuri nimejengeka,
Ni huru na tegemezi, zote ni zangu aina,
Zijengazo umbo langu, niweze kuwa imara,
Silingani na mofimu, nipeni yangu heshima.

**Kiambishi:** Acheni kuyumbayumba, mimi ni kiboko yenu,
Ninaambikwa mwanzoni, na mwishoni mwa mzizi,
Wananiita Awali, na Tamati jina langu,
Hayo ni majina yangu, waungwana tambueni,
Mnapotaka maana, kumbukeni kuambika.

**Mofimu:** Naziona mbwembwe zenu, mimi ni kiboko yenu,
Nataja nafsi na njeo, na idadi zake pia,
Kauli zote ni zangu, na sarufi kedekede,
Mimi nipo peke yangu, sifanani na yeyote,
Nasema tena kwa dhati, mimi ndiye kubwa lenu.

FOR ONLINE USE ONLY

**Maswali**

1. Pendekeza kichwa cha majigambo uliyoyasoma.
2. Kwa mujibu wa majigambo uliyoyasoma, mzizi ni nini?
3. Kwa mujibu wa ubeti wa pili, kiambishi kina dhima gani?
4. Kutokana na majigambo uliyoyasoma, umbo linatajwa kuwa ni nini?
5. Bainisha dhima za mofimu zilizotajwa katika majigambo uliyoyasoma.
6. Majigambo uliyoyasoma yanaeleza aina gani za viambishi?
7. Taja aina mbili za mofu zilizobainishwa katika majigambo uliyoyasoma.
8. Eleza kwa kifupi sifa mbili kwa kila dhana ya msingi ya kisarufi iliyojitokeza katika majigambo uliyoyasoma.



KISWAHILI FINAL.indd 2 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Kazi ya 1.2**

Kusanya maneno kumi ya aina mbalimbali, kisha bainisha viambishi na mofu zinazounda maneno hayo.

**Zingatia**

Mzizi ni kiini cha neno. Ni sehemu ya neno ambayo haibadiliki. Kwa mfano, katika kitenzi **anapika** na **wanacheza**, **-pik-** ni mzizi wa neno anapika na **-chez-** ni mzizi wa neno wanacheza.

Kiambishi ni umbo linalopachikwa kwenye mzizi wa neno ili kutekeleza dhima ya kisarufi au kuunda neno jipya. Katika lugha ya Kiswahili, kuna aina mbili za viambishi ambazo ni viambishi awali na viambishi tamati. Viambishi awali hupachikwa kabla ya mzizi wa neno, ilihali viambishi tamati hupachikwa baada ya mzizi wa neno. Kwa mfano, katika kitenzi **anapiga**, **a-** na **-na-** ni viambishi awali, **-pig-** ni mzizi, na **-a** ni kiambishi tamati.

Mofu ni umbo linalowakilisha mofimu. Lugha ya Kiswahili ina aina mbili za mofu ambazo ni mofu huru na mofu tegemezi. Mofu huru ni maneno yanayoundwa na umbo moja lisiloweza kugawanyika katika maumbo madogo zaidi bila kupoteza maana. Mifano ya maneno hayo ni **mama**, **bata**, **hatari**, na **sana**. Mofu tegemezi ni maumbo ambayo hayawezi kujitegemea yakiwa pekee. Mifano ya mofu tegemezi ni **m-** na **-ti** katika neno **mti**. Mofu **m-** haiwezi kuwa na maana ikiwa pwekepweke, vivyohivyo **-ti**.

Mofimu ni kipashio dhahania ambacho huwakilishwa na mofu. Mofimu ni maana zilizomo katika mofu. Mofimu ni dhahania kwa kuwa haitamkiki wala haiandikiki. Mofimu hudokeza taarifa za kisarufi kama vile nafsi, njeo, idadi, hali, na kauli. Kwa mfano, katika neno **anakula**, mofu **a-** imebeba mofimu ya nafsi ya tatu umoja; katika neno **tumechelewa**, mofu **tu-** imebeba mofimu ya nafsi ya kwanza wingi; na katika neno **hujakiona**, mofu **hu-** imebeba mofimu ya nafsi ya pili umoja. Vilevile, mofimu hudokeza njeo. Kwa mfano, katika neno **waliuleta**, mofu **-li-** imebeba mofimu ya njeo ya wakati uliopita; katika neno **tunayatunza**, mofu **-na-** imebeba mofimu ya njeo ya wakati uliopo; na katika neno **utasoma**, mofu **-ta-** imebeba mofimu ya njeo ya wakati ujao. Aidha, mofimu hudokeza idadi. Kwa mfano, katika neno **viti**, mofu **vi-** imebeba mofimu ya wingi; katika neno **wanafunzi**, mofu **wa-** imebeba mofimu ya wingi; na katika neno **mganga**, mofu **m-** imebeba mofimu ya umoja. Pia, mofimu hudokeza hali. Kwa mfano, katika neno **ameondoka**, mofu **-me-** imebeba mofimu ya hali timilifu. Pamoja na hayo, mofimu hudokeza kauli mbalimbali. Kwa mfano, katika maneno **amepigwa**, **wamekatwa**, na **imesomwa**; mofu **-w-** imebeba mofimu ya kauli ya kutendwa.



KISWAHILI FINAL.indd 3 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Zoezi la 1.1**

1. Bainisha mizizi ya maneno yafuatayo:
   (a) anabisha
   (b) nimeibeba
   (c) pamba
   (d) wezesha
2. Tenganisha mofu za maneno yafuatayo:
   (a) amechoka
   (b) mpikie
   (c) shuleni
   (d) warembo
3. Fafanua aina za viambishi zinazojitokeza katika maneno uliyopewa katika swali la pili.

**Zingatia**

Kuna uhusiano mkubwa baina ya mofu na mofimu. Kama ilivyoelezwa awali, mofu ni umbo linalowakilisha mofimu. Hivyo, mofu ni umbo linalositiri mofimu. Ubainishaji wa dhana hizi katika utendaji huzingatia umbo ambalo ndilo mofu, wakati maana ya umbo hilo ndiyo mofimu. Kwa mfano, mofu **-na-** katika kitenzi **anakuja** imebeba mofimu ambayo ni njeo ya wakati uliopo hali ya kuendelea.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la marudio la 1

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

   (i) Kitenzi kipi kinaonesha kwamba umeme ulitoweka?
   (a) Aliukata
   (b) Ulikatiwa
   (c) Ulikatika
   (d) Tulikatiwa
   (e) Walikatika

Fot online use only
do not duplicate

(ii) Kiambisha kinachodokeza ukanushi ni ....................

(a) wa-

(b) sh-

(c) -a

(d) si-

(e) na-

(iii) Upi ni uchanganuzi sahihi wa mofu zinazounda kitenzi **watachekeshana**?

(a) Wa-ta-che-ke-sha-na

(b) Wata-cheke-sh-ana

(c) Wa-ta-chek-esh-a-na

(d) Wa-ta-ch-ek-e-sh-an-a

(e) Wa-ta-chek-esh-an-a

(iv) Kauli mbalimbali za kitenzi ni dhima ya ....................

(a) mofu

(b) mofu huru

(c) mofimu

(d) mzizi

(e) mofu tegemezi

FOR ONLINE USE ONLY

(v) Neno lipi kati ya haya ni mofu huru?

(a) Uji

(b) Uzuri

(c) Uchache

(d) Ufa

(e) Upweke

Fot online use only
do not duplicate

2. Oanisha dhana zilizopo fungu A na mifano yake iliyopo fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi.

| **Fungu A** | **Fungu B** |
|---|---|
| (i) Mzizi | A. mtu |
| (ii) Mofu huru | B. sasa |
| (iii) Kiambishi awali | C. cham- |
| (iv) Kiambishi cha kauli | D. -chok- |
| (v) Kiambishi tamati | E. -an- |
| | F. -ji. |
| | G. u- |

3. Ambisha mizizi ifuatayo kulingana na mahitaji ya mzizi husika.
   (a) pik-
   (b) on-
   (c) -sem-
   (d) -chokoz-
   (e) tengenez-
   (f) temb-
   (g) -toto

FOR ONLINE USE ONLY

4. Onesha mzizi wa kila kitenzi katika sentensi zifuatazo:
   (a) Mtoto anaimba wimbo mzuri.
   (b) Mwalimu aliwatambulisha wanafunzi wageni shuleni.
   (c) Juzi hatukusomeana vitabu.
   (d) Wanafunzi wanakimbizana uwanjani.
   (e) Wazazi wao wanalipishana gharama za upotevu wa mali.

5. Andika maneno 15 yenye viambishi. Katika kila neno, chambua viambishi ukionesha viambishi awali, tamati, na mzizi wa neno.



KISWAHILI FINAL.indd 6 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

6. Eleza mofimu iliyobebwa na kila mofu iliyopigiwa mstari.

   (a) Kijitabu hiki hakisomeki vizuri.

   (b) Anatembea kichovu sana.

   (c) Amekwenda sokoni kununua mchele na maharage.

   (d) Kiti hiki kimevunjika.

   (e) Jitu lile linapenda kuabudiwa.

   (f) Akifika, mwambie aje ofisini.

   (g) Anapenda kusoma mashairi kutoka kitabuni.

   (h) Hapendi mchezo wakati wa masomo.

7. Kwa kutumia mifano, eleza dhima za uambishaji.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI FINAL.indd 7 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

# Sura ya Pili

## Uundaji wa maneno

### Utangulizi

*Lugha huhitaji kuongeza msamiati wake kwa kuunda maneno mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano. Mawasiliano huhitaji lugha iwe na msamiati wa kutosha. Katika sura hii, utajifunza kuunda maneno ya Kiswahili kwa kutumia njia mbalimbali. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuunda maneno ya Kiswahili kwa kutumia njia mbalimbali na kuyatumia katika mazingira mbalimbali kukidhi mahitaji ya mawasiliano.*

### Kazi ya 2.1

**Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Ndauka na Kambala ni marafiki wanaosoma Kidato cha Pili. Siku moja, Ndauka alimwambia Kambala, "Tucheze mchezo wa kuongezeana maneno. Mimi nikitaja neno moja, wewe unaongezea maneno mengine matatu yanayotokana na neno nililotaja." Kambala akajibu, "Sawa! Tuanze."

Ndauka akataja neno **piga**. Kambala akaongeza, "Pigapiga, pigana, kipigo." Ndauka akataja neno jingine, **cheza**. Kambala akaongeza, "Mchezaji, mchezo, watachezesha." Ndauka akamwambia Kambala, "Sasa ni zamu yako kutaja neno." Kambala akataja neno **ruka**. Ndauka akasema, "Mbona rahisi tu, rukaruka, rukia, rukwa." Kambala akataja neno **omba**. Ndauka akaongeza, "Ombi, ombaomba, mwombaji." Waliendelea kutaja maneno hadi kengele ya kuingia darasani ilipogongwa wakakimbia kuingia darasani.

FOR ONLINE USE ONLY

**Maswali**

1. Kutokana na kisa ulichokisoma, Ndauka na Kambala walicheza mchezo gani?
2. Kati ya maneno aliyoyatamka Ndauka, ni maneno yapi yameundwa kwa kurudiwarudiwa?
3. Taja maneno matatu yaliyotamkwa na Kambala yenye viambishi kabla na baada ya mzizi.



KISWAHILI FINAL.indd 8 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Zingatia**

Jambo kuu linalosababisha uhitaji wa maneno mapya ni mabadiliko katika nyanja mbalimbali za kimaisha. Nyanja hizo ni za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, kisayansi, na kiteknolojia. Mabadiliko yanapotokea katika nyanja hizo, huchochea uhitaji wa maneno mapya yatakayotumika kuelezea mabadiliko hayo. Kwa hiyo, maneno mapya huhitajika ili kuwakilisha dhana mpya zinazoibuka. Kwa mfano, maneno kama **data**, **kisimbuzi**, **udukuzi**, **baruapepe**, **nukushi**, na **kompyuta** yameundwa katika Lugha ya Kiswahili ili kuwakilisha dhana zilizoibuka katika nyanja za sayansi na teknolojia.

Maneno huundwa kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na unyambulishaji, uambatanishaji, ukopaji, uradidi, ufupishaji, na ufananisho. Unyambulishaji ni uongezaji wa viambishi katika mzizi wa neno ili kupata maneno mapya. Kwa mfano, neno **taifa** lenye mzizi **taifa** linaweza kuongezwa kiambishi **u-** mwanzoni na kutupatia neno **utaifa**. Aidha, neno **piga** lenye mzizi **pig-**, likiongezewa kiambishi **ki-** au **m-** mwanzoni na kiambishi **-o** mwishoni mwa mzizi, tunapata maneno mapya kama vile **kipigo** na **mpigo**.

Ukopaji ni njia ya kuchukua neno la lugha nyingine na kuliingiza katika matumizi ya lugha husika. Kwa mfano, maneno kama **achali**, **ikulu**, na **ngeli** ni ya mkopo katika Lugha ya Kiswahili. Baadhi ya maneno yaliyokopwa hurekebishwa matamshi au maumbo yake ili yaendane na sarufi ya lugha iliyokopa. Urekebishaji wa maneno hayo hujulikana kama utohoaji. Mfano wa maneno ya Kiswahili yaliyotoholewa kutoka katika Lugha ya Kiingereza ni **polisi**, **sketi**, na **baiskeli**.

FOR ONLINE USE ONLY

Njia nyingine ya uundaji wa maneno ni uambatanishaji. Hii ni mbinu ya kuunganisha maneno mawili au zaidi ili kupata neno moja lenye maana tofauti na maneno yaliyounganishwa. Kwa mfano, maneno **mwana** na **nchi** yakiambatanishwa, tunapata neno **mwananchi**. Maneno **askari** na **kanzu** yakiambatanishwa, tunapata neno **askarikanzu**.

Uradidi ni njia nyingine ya uundaji wa maneno ambayo huhusisha urudiaji wa neno zima au sehemu ya neno. Mfano wa maneno yaliyoundwa kwa njia ya uradidi wa neno zima ni **mbogamboga** na **ombaomba**. Mfano wa maneno yaliyoundwa kwa uradidi wa sehemu ya neno ni **kinyumenyume** ambalo limetokana na neno **kinyume** na sehemu ya neno hilo iliyorudiwa ni **nyume**. Neno lingine ni **kichurachura** ambalo limetokana na neno **kichura** na sehemu ya neno hilo iliyorudiwa ni **chura**.

Pia, maneno huweza kuundwa kwa njia ya ufupishaji. Ufupishaji wa maneno ni kitendo cha kuchukua herufi za mwanzo za maneno au sehemu ya neno ili kuunda



KISWAHILI FINAL.indd 9 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

neno jipya. Kuna aina mbili za ufupishaji ambazo ni akronimia na uhulutishaji. Akronimia ni ufupishaji wa kuchukua herufi au silabi za mwanzo za kila neno kuu katika jina ambalo linaundwa na maneno mengi ili kuunda neno jipya. Mifano ya maneno hayo ni TAMISEMI, TATAKI, na LUKU. Neno TAMISEMI limetokana na jina Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, neno TATAKI limetokana na jina Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, na neno LUKU limetokana na jina Lipia Umeme Kadiri Unavyotumia. Uhulutishaji ni ufupishaji wa kuchukua sehemu ya neno na kuiunganisha na sehemu ya neno lingine ili kuunda neno moja jipya. Kwa mfano, maneno **chakula cha mchana** yakihulutishwa tunapata neno **chamcha**.

Aidha, maneno huweza kuundwa kwa njia ya ufananisho. Njia hii hutumika kuunda maneno kwa kufananisha kitu na umbo lake, tabia yake, mlio wake au matumizi ya kitu husika. Kwa mfano, neno **nyau** limetokana na ufananisho wa mnyama anayerejelewa na neno hilo na mlio wake. Pia, silaha ya kivita iitwayo **kifaru** imeitwa hivyo kutokana na umbo lake kufananishwa na mnyamapori aitwaye kifaru. Vilevile, mmea uitwao **kifaurongo** umeitwa hivyo kutokana na kufananishwa na tabia yake ya kujikunja unapoguswa. Kujikunja huko hufananishwa na hali ya kufa, yaani kufa kwa uongo. Aidha, maneno **kinyonyi** na **kikokotozi** yameundwa kwa njia ya kufananisha kitu kinachorejelewa na maneno hayo, na kazi au matumizi yake. Kinyonyi ni kifaa kidogo kinachotumika kunyonya au kuhamishia data kutoka kwenye kompyuta, na kikokotozi ni kifaa kinachotumika kukokotoa hesabu.

FOR ONLINE USE ONLY

**Zoezi la 2.1**

1. Eleza njia zilizotumika kuunda maneno yafuatayo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) | pigana | (f) | mchezo |
| (b) | harakaharaka | (g) | ombi |
| (c) | mwananchi | (h) | televisheni |
| (d) | BAKITA | (i) | UKIMWI |
| (e) | pikipiki | (j) | TAMISEMI |

2. Kuna tofauti gani kati ya mbinu zilizotumika kuunda maneno **mwanamuziki** na **mbogamboga**?
3. Orodhesha maneno mengine matano yaliyoundwa kwa kila njia uliyoibainisha katika swali la kwanza.



KISWAHILI FINAL.indd 10 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

## Kazi ya 2.2

Soma matini kutoka katika andiko lolote kama vile kitabu, gazeti au jarida, kisha bainisha maneno yaliyoundwa kwa njia ya unyambulishaji, utohoaji, na ukopaji.

## Zoezi la marudio la 2

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

(i) Mifano ya maneno yaliyoundwa kwa njia ya uambatanishaji ni .....................

(a) shughulisha, polepole, mtutu
(b) pigapiga, pigilia, mapigo
(c) baruapepe, isimujamii, pakashume
(d) mwimbishaji, bunguabongo, chajio
(e) hatimiliki, utaifishaji, vilevile

(ii) Unyambulishaji katika Lugha ya Kiswahili huhusisha upachikaji wa viambishi .....................

(a) kabla ya mzizi
(b) katikati ya mzizi
(c) baada ya mzizi
(d) kabla na baada ya mzizi
(e) kabla, katikati, na baada ya mzizi

FOR ONLINE USE ONLY

(iii) Maneno yapi kati ya haya yafuatayo yameundwa kwa njia ya ufananisho?

(a) Vigelegele na chururu
(b) Kibebeo na kijenzi
(c) Kinasasauti na pikipiki
(d) Kitegauchumi na kikokotozi
(e) Kitegauchumi na kinyonyi

(iv) Neno lipi kati ya haya yafuatayo halitokani na utohoaji?

(a) Posta
(b) Kompyuta
(c) Polisi
(d) Boksi
(e) Achali

Fot online use only
do not duplicate

(v) Maneno yapi yametokana na mbinu ya ukopaji?
  (a) Duka na chujio
  (b) Karoti na kibatari
  (c) Namba na kuku
  (d) Pikipiki na papai
  (e) Chajio na chamcha

2. Oanisha maneno yaliyopo fungu A na fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi ili kuunda maneno sahihi ya Kiswahili.

| Fungu A | Fungu B |
|---|---|
| (i) Mwana | A. tumbo |
| (ii) Kidole | B. maumbo |
| (iii) Hati | C. choma |
| (iv) Sarufi | D. wamiliki |
| (v) Nyama | E. umbo |
| | F. anga |
| | G. mlazo |

FOR ONLINE USE ONLY

3. Kwa kutumia mifano, eleza sababu tano za uundaji wa maneno mapya katika lugha.
4. Kuna tofauti gani kati ya unyambulishaji na uambatanishaji?
5. Kwa kutumia njia ya unyambulishaji, unda maneno matano kwa kila mzizi wa kitenzi uliopewa.
   (a) pit-
   (b) sem-
   (c) andik-
   (d) lip-
   (e) fung-
6. Taja njia zilizotumika kuunda maneno yafuatayo:
   (a) chemshabongo
   (b) UMISSETA
   (c) kilimo
   (d) mchapishaji
   (e) hekaheka
   (f) pachapacha
7. Tunga sentensi mbili kwa kila neno ulilopewa katika swali la 6.



KISWAHILI FINAL.indd 12 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

# Sura ya Tatu

## Matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali

### Utangulizi

*Lugha ni kipengele muhimu katika mawasiliano ya wanadamu. Ili lugha ikidhi haja ya mawasiliano, ni lazima itumiwe kulingana na muktadha. Hivyo, matumizi ya lugha ni namna watu wanavyoweza kuwasiliana kwa kuzingatia historia, mila, na desturi za jamii inayohusika. Katika sura hii, utajifunza rejesta, misimu, lugha ya mazungumzo na ya maandishi, matamshi na lafudhi ya Kiswahili Sanifu, na utata katika mawasiliano. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia Lugha ya Kiswahili kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali.*

### Kazi ya 3.1

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

FOR ONLINE USE ONLY

**Rejesta na marafiki zake**

Hapo zamani za kale, katika Kijiji cha Lukaso, palikuwa na mzee mmoja aliyeitwa Rejesta. Mzee huyo alikuwa na marafiki wawili, Misimu na Utata. Watu hawa walikuwa na tabia zilizowashangaza wakazi wa kijiji hicho. Mzee Rejesta alikuwa na tabia mithili ya kinyonga, kwani alijibadilisha kulingana na mazingira aliyokuwa akienda. Kila mahali alipokwenda, alibadilika. Alipofika hotelini, alijiita *nani wali kuku*; hospitalini, alijiita *meza kimoja kutwa mara mbili* na *maji mengi*; na mahakamani, alijiita *mheshimiwa hakimu naomba unipunguzie adhabu*. Watu wa kijiji hicho walishangazwa sana na tabia zile na walipojaribu kumuuliza sababu ya kufanya vile, aliwajibu kwamba yeye alitaka kuwa wa kipekee na hakutaka kueleweka kwa watu wengine.

Mzee Rejesta aliendelea kusema kwamba, wakati mwingine, alifanya hivyo ili kutambulisha mazungumzo yake awapo katika mazingira tofauti, kuokoa muda wa mazungumzo, kukuza lugha, na kupamba mazungumzo baina yake na wazungumzaji wengine.

Mazungumzo yalipokuwa yakiendelea, mkazi mmoja ajulikanaye kwa jina la Nguzokazi aliuliza, "Mbona marafiki zako, Mzee Misimu na Utata, wana tabia



KISWAHILI FINAL.indd 13 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

za kushangaza kama zako?"

Mzee Rejesta alijibu, "Mzee Misimu yuko vile kwa sababu huvuma na kufanya kazi kwa muda fulani kulingana na matukio yanayotokea katika jamii." Aliendelea kusema kuwa Mzee Misimu alikuwa vile kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Aidha, matukio ya kisiasa, kijamii, kiuchumi, na kiutamaduni yalimfanya awe katika hali ile. Zaidi, alisema kwamba tabia aliyokuwa nayo Mzee Misimu ilisababishwa na utani unaozuka miongoni mwa watu katika jamii.

Mzee Rejesta aliendelea kufafanua kwamba Mzee Misimu alipendwa na watu kwa sababu ya kubadilikabadilika kulingana na matukio yaliyopo katika jamii. Pia, alipendwa kwa sababu ya lugha ya kificho isiyo sanifu. Mzee Misimu alikuwa na watoto watatu, ambao ni Pekee, Kitarafa, na Zagao.

Pamoja na maelezo ya Mzee Rejesta kuhusu Mzee Misimu, mwanakijiji mwingine alitaka kujua lengo la Mzee Misimu kufanya vile alivyokuwa anafanya. Mzee Rejesta aliendelea kueleza kinagaubaga kuwa Mzee Misimu alifanya hivyo ili kuipamba lugha, kukuza msamiati, kutunza historia ya jamii, na kuibua hisia mbalimbali za wazungumzaji wa lugha.

Baada ya maelezo ya Mzee Rejesta, Nguzokazi alitaka kujua kuhusu Mzee Utata. Mzee Rejesta aliendelea kwa kusema, "Mzee Utata yuko hivyo kutokana na tabia ya kuwa na maana zaidi ya moja. Siku zote, jina lake linapotajwa, watu hufikiri zaidi na hupata maana zaidi ya moja. Jina hilo huleta maana zaidi ya moja litajwapo kama neno moja peke yake au likiwa katika muundo wa sentensi."

Nguzokazi aliendelea kuuliza namna ambavyo wanakijiji wanaweza kumsaidia Mzee Utata kuondokana na tabia yake. Mzee Rejesta alijibu kuwa wanakijiji wanaweza kumsaidia kwa kuweka mkazo mahali panapostahili wakati wa matamshi ya maneno na kuzingatia matumizi sahihi ya alama za uandishi. Vilevile, wanatakiwa kuteua maneno kulingana na muktadha ili kumsaidia Mzee Utata kuacha tabia yake. Mzee Rejesta alimaliza kwa kusema kwamba mambo haya yote yakizingatiwa, watu wataweza kuwasiliana katika miktadha mbalimbali kwa mitindo tofauti na kuondokana na tabia za Mzee Utata.

**Maswali**

1. Mzee Rejesta alikuwa na marafiki wangapi? Taja majina yao.
2. Kwa nini Mzee Rejesta alikuwa na tabia ya kubadilikabadilika kama kinyonga?



KISWAHILI FINAL.indd 14 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

3. Kwa mujibu wa habari uliyoisoma, Mzee Misimu alikuwa na sifa gani?
4. Mambo gani yanapaswa kufanyika ili kumsaidia Mzee Utata kuepuka tabia yake ya kuwa na maana zaidi ya moja?
5. Chunguza mitindo ifuatayo ya lugha, kisha bainisha mahali inapotumika.

   (a) Mahakama imekukuta na hatia kama ulivyoshitakiwa.

   (b) Makongoro yapo.

   (c) Mwalimu, huyu ni mchokozi.

   (d) Ameze kidonge kimoja tu asubuhi kabla ya kula chochote.

## Rejesta

**Kazi ya 3.2**



1. Tembelea maeneo yafuatayo, kisha chunguza lugha inayotumika katika maeneo hayo.
   (a) hospitalini au zahanati
   (b) sokoni au gulioni
2. Andika kwa ufupi mazungumzo yaliyotumika katika maeneo hayo kwa kuzingatia:
   (a) tofauti za matumizi ya lugha katika maeneo hayo mawili
   (b) sababu za tofauti hizo

FOR ONLINE USE ONLY

**Zingatia**

Lugha hutumika katika miktadha mbalimbali kutegemeana na mada inayohusika, malengo ya watumiaji wa lugha, na uhusiano baina ya wazungumzaji. Kutokana na mazingira ya watumiaji wa lugha kutofautiana kishughuli, kiuhusiano, na kiutamaduni, mitindo mbalimbali ya lugha katika mazingira mahususi hujitokeza. Mitindo hiyo huitwa *rejesta*. Kwa mfano, mtindo wa lugha inayotumika hospitalini, shuleni, mahakamani, msikitini, kanisani, shambani, ziwani, au baharini hutofautiana. Hivyo, rejesta ni mtindo wa lugha unaotumika kulingana na muktadha.

Rejesta huweza kusababishwa na mambo mbalimbali, yakiwamo *upekee wa*



KISWAHILI FINAL.indd 15 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

*kundi la watumiaji wa lugha*, *shughuli wanazozifanya*, na *mahitaji ya kuficha jambo*. Kutokana na madhumuni ya kukidhi haja ya mawasiliano katika mazingira mahususi, aina mbalimbali za rejesta hujitokeza. Baadhi ya aina hizo ni: rejesta ya hotelini, rejesta ya mahakamani, rejesta ya nyumba za ibada, rejesta ya hospitalini, na rejesta ya mtaani.

**Kazi ya 3.3**



Katika kikundi, igiza mazungumzo yanayoweza kupatikana shuleni, kijiweni, hotelini au mgahawani, kisha bainisha sifa za mazungumzo yaliyotumika katika kila muktadha.

**Zoezi la 3.1**

1. Andika mfano mmojammoja wa rejesta za maeneo yaliyotajwa hapa chini:
   (a) bungeni
   (b) michezoni
   (c) shuleni
   (d) mtaani
   (e) kwenye nyumba za ibada
2. Eleza sababu tano za kujitokeza kwa rejesta katika jamii.

FOR ONLINE USE ONLY

## Misimu

**Kazi ya 3.4**

1. Kusanya misimu ishirini inayotumika katika miktadha mbalimbali, kisha wasilisha mbele ya wanafunzi wenzako darasani.
2. Kwa kutumia mifano ya misimu uliyoiwasilisha darasani, eleza hasara za matumizi ya misimu.

**Zingatia**

Misimu ni maneno yasiyo sanifu yanayozuka na kutumiwa na watu kwa muda fulani kutokana na kuibuka kwa matukio mbalimbali. Huzushwa na wazungumzaji wa lugha kwa ajili ya kukidhi haja ya kimawasiliano kulingana na wakati wa tukio mahususi. Kwa mfano, mnamo miaka ya 2010, wakati wauzaji wa petroli



KISWAHILI FINAL.indd 16 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

na mafuta ya taa walipokuwa wakichanganya mafuta hayo ili wapate faida zaidi, uliibuka msimu **chakachua**.

Misimu ikiendelea kutumika na kudumu kwa muda mrefu, hukubalika na kupandishwa hadhi kwa kusanifishwa na kuwa maneno rasmi katika msamiati wa lugha. Aidha, huingizwa katika kamusi. Kwa mfano, maneno **kasheshe**, **daladala**, na **chakachua** yamesanifishwa na kuingizwa katika kamusi baada ya kutumika kwa muda mrefu na kukubaliwa na wazungumzaji wa Kiswahili. Kwa hiyo, sifa kuu ya misimu ni kuzuka na kupotea katika matumizi baada ya mahitaji yake kukoma.

Misimu ina dhima anuwai katika lugha. Miongoni mwa dhima hizo ni kukuza msamiati, kupamba lugha, kutunza historia ya jamii, na kuibua hisia mbalimbali za wazungumzaji na wasikilizaji.

### Zoezi la 3.2

1. Kwa kutumia mifano, bainisha aina za misimu.
2. Eleza sifa za misimu, ukitoa mifano miwili kwa kila sifa.
3. Bainisha changamoto zinazoweza kujitokeza kutokana na utumiaji wa misimu katika lugha ya Kiswahili.
4. Fafanua jinsi ambavyo misimu inaweza:
    (a) kukuza lugha;
    (b) kupamba lugha; na
    (c) kutunza historia ya jamii.

FOR ONLINE USE ONLY

## Lugha ya mazungumzo na maandishi

### Kazi ya 3.5



**Soma matini zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Matini A**

**Todo:** Hivi ndugu yangu, utajiheshimu lini?

**Wakulo:** Kwani unataka nijiheshimuje? Au labda unataka nikunyenyekee?

**Todo:** Hapana, sitaki uniheshimu mimi. Jiheshimu mwenyewe.

**Wakulo:** Halafu ndugu yangu, unaona madhara ya kukimbia shule? Kutorokea machokoroni na kucheza bao kumekunyima Kiswahili



KISWAHILI FINAL.indd 17 2021/09/13 12:13

Fot online use only
don't duplicate

kinyofu; unaboronga tu!

**Todo:** Kwani Kiswahili kinaliwa? Ebu achana na mimi. Kisa umetangulia kuzaliwa! Usinisumbue sasa, wala usizalau wenzio.

**Wakulo:** Najiheshimu. Ndiyo maana ninanyoosha lugha. Sikiliza ndugu yangu, tusigombane. Najua ulikasirika, kisa nilimtolea maneno makali rafiki yako Chausiku.

**Mpitanjia:** Nyie mapacha au vipi? Mbona nimesikia kama mnalumbana?

**Wakulo:** We mzee, shika njia zako!

**Matini B**

Baada ya uhuru, hali ya usafiri nchini Tanzania ilianza kubadilika kidogokidogo na kuwa nzuri. Mathalani, idadi ya magari iliongezeka. Hali hii ilifanya usafirishaji wa watu na bidhaa mbalimbali kuwa rahisi zaidi. Hivyo, watu waliweza kusafiri kwenda sehemu mbalimbali za nchi.

Barabara zilitunzwa na Wizara ya Ujenzi. Wizara hiyo ilikuwa na watumishi walioshughulika na ujenzi na uangalizi wa barabara na miundombinu mingine. Miongoni mwao, walikuwamo wafanyakazi na mafundi hodari waliopata mafunzo na kufuzu. Mipango yote iliyohusika na barabara ilipangwa na mhandisi mkuu wa kila mkoa na kusimamiwa na watumishi wengine.

FOR ONLINE USE ONLY

**Maswali**

1. Tofautisha mitindo ya lugha iliyotumika katika matini A na B.
2. Kati ya matini A na B, matini ipi imetumia lugha ya mazungumzo na ipi imetumia lugha ya maandishi? Kwa nini?
3. Bainisha sifa zinazofanana baina ya matini A na B.
4. Bainisha makosa yanayojitokeza katika matini A.
5. Andika kwa ufasaha matini A.

**Zingatia**

Lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi zina dhima ya kuwezesha mawasiliano ya binadamu. Lugha ya mazungumzo ni namna ya mawasiliano inayomwezesha mtu kujieleza kwa njia ya mdomo ikiambatana na ishara za viungo vya mwili. Chanzo chake ni *mzungumzaji* na kikomo chake ni *msikilizaji*. Lugha ya mazungumzo huruhusu mabadiliko ya papo kwa papo na haihitaji ujuzi wa kusoma wala kuandika.



KISWAHILI FINAL.indd 18 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

Ili mazungumzo yafane, mzungumzaji anapaswa kuzingatia mambo yafuatayo: ufasaha wa lugha, mpangilio wa mawazo kimantiki, kutoa sauti ya kutosha, kuonesha vitendo au ishara zinazoendana na maneno anayoyatamka, kuuliza maswali, na kutoa mchango unaoendana na mada. Kwa upande mwingine, msikilizaji anapaswa kuwa mtulivu na msikivu, kufahamu kinachozungumzwa, pamoja na kupima mazungumzo aliyoyasikiliza ili kuwa na uwezo wa kuchangia hoja na kuuliza maswali endapo kuna mahali hajaelewa.

Lugha ya mazungumzo huzingatia mambo mbalimbali. Miongoni mwayo ni mada inayozungumziwa, muktadha wa mazungumzo, lengo la mazungumzo, na uhusiano uliopo baina ya wazungumzaji.

Lugha ya maandishi ni njia ya mawasiliano inayomwezesha mtu kujieleza kwa njia ya maandishi. Chanzo chake ni *mwandishi* na kikomo chake ni *msomaji*. Lugha ya maandishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi, huhitaji stadi za kusoma na kuandika, ujumbe wake huweza kudumu kwa muda mrefu kama kumbukumbu baada ya kuandikwa na, hivyo, huweza kurejelewa. Mwisho, ujumbe wa kimaandishi huwasilishwa kwa kuzingatia kikamilifu kanuni za kisarufi na kiuandishi.

**Kazi ya 3.6**

FOR ONLINE USE ONLY



1. Sikiliza taarifa ya habari kutoka kwenye redio, kisha nukuu taarifa hiyo kimaandishi.
2. Je, unadhani lugha ya taarifa ya habari ni ya maandishi au ya mazungumzo?
3. Bainisha sifa za lugha ya mazungumzo na ya maandishi ili kutetea jibu lako katika swali la pili.
4. Eleza tofauti zilizopo kati ya lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi.

## Matamshi na lafudhi ya Kiswahili Sanifu

**Kazi ya 3.7**



**Fuatilia mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Ngocha:** Woi! Woi! Aisee Mura...! Hii nyama choma bira ya kichuri? Piripiri pekee haitoshi.



KISWAHILI FINAL.indd 19 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Wachu:** Mama yangu! Wee, Ngocha fipi aisee! Ina maana babaangu bila hiyo kichuri huli nyama? Mimi hata bila chumvi nakula aisee...! Nyama ni ta…ni tamu kweli.

**Njango:** Nani anachema nyama chio tamu? Au anataka ipikwe na nchele kabicha? Njomba njomba...! Umechiba ndio mana unaleta chalau.

**Wachu:** Ha ha haaa! Umesoea kula samaki mchanga wewe, sasa nyama ya ng'ombe wapi na wewe? Pisha huko…kiruu!

**Ukuko:** Hapa ningepata na ka-swoda, haka kanyama kangeteremka vizuri kooni. Ngocha ee, sasa vipi…! Kichuri huna, swoda huna, hamkujipanga!

**Njango:** Wewe Ukuko wewe, unapenda choda wewe! Bachi mwambie Meku akupe hata mbege uchuchie nyama. Wachu umechikia?

**Wachu:** Haiwesekani kabisa, sina hela. Kwansa ni nani alimwita Ukuko hapa?

**Maswali**

1. Huku ukitoa sababu za kutetea jibu lako, eleza kila mhusika katika mazungumzo anatokea mkoa gani wa Tanzania?
2. Bainisha sentensi zenye makosa ya kimatamshi kutoka katika mazungumzo uliyoyasoma, kisha pigia mstari makosa hayo.
3. Andika kwa usahihi sentensi zenye makosa.
4. Kwa kutumia matamshi sahihi ya Kiswahili, andika upya mazungumzo hayo.

FOR ONLINE USE ONLY

**Zingatia**

Matamshi ni namna maneno yanavyosemwa. Wazungumzaji hutamka maneno mbalimbali ili kuwasiliana na wasikilizaji. Hivyo, dhima kuu ya lugha ni kuwezesha watumiaji wake kuwasiliana. Lugha huweza kutimiza dhima hiyo pale watumiaji wake wanapozingatia utamkaji sahihi wa maneno. Utamkaji sahihi huwawezesha wasikilizaji kuelewa vizuri. Matamshi sahihi ni yale yanayozingatia kanuni za kisarufi.

Katika lugha ya Kiswahili, kuna vipengele vikuu vitatu vinavyozingatiwa kwenye matamshi. Vipengele hivyo ni *kiimbo*, *mkazo*, na *lafudhi*. Kiimbo ni sifa ya kimatamshi inayohusu kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti za lugha

Fot online use only
do not duplicate

wakati wa utamkaji. Kuna aina nne za kiimbo ambazo ni kiimbo cha maelezo, kiimbo cha swali, kiimbo cha amri, na kiimbo cha mshangao. Kiimbo cha maelezo huwa na mawimbisauti ya msemaji yaliyo katika hali iliyonyooka (bila kupanda wala kushuka). Kiimbo cha swali huwa na mawimbisauti ya msemaji ambayo hupandishwa yanapokaribia mwishoni mwa usemi na kumalizia kwa kushushwa. Kiimbo cha amri huwa na mawimbisauti yatolewayo kwa kiwango cha juu zaidi. Kiimbo cha mshangao hujitokeza kwa kupandisha, kushusha, na kupandisha tena mawimbisauti katika silabi za mwishoni mwa neno. Kiimbo ni muhimu kwa sababu husaidia kubainisha lengo lililokusudiwa na mzungumzaji.

Mkazo ni kiwango cha nguvu inayotumika katika utamkaji wa silabi. Silabi yenye mkazo hutamkwa kwa nguvu kuliko silabi isiyokuwa na mkazo katika neno. Katika Kiswahili Sanifu, mkazo huwekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho wa neno. Katika maandishi, mkazo huoneshwa kwa namna mbalimbali. Mwandishi anaweza kutumia alama ya ritifaa kabla ya silabi husika, kwa mfano, "sawa'sawa" na "bara'bara". Kadhalika, anaweza kuandika silabi yenye mkazo kwa kutumia herufi kubwa au wino mkozo, kwa mfano, "sawaSAwa" au "sawa**sa**wa". Katika usemaji, mkazo huwa na dhima ya kubainisha maana ya mazungumzo. Mbali na matumizi haya ya kawaida, mkazo pia hutumiwa kusisitiza jambo. Ni muhimu kutumia mkazo ipasavyo kwa sababu matumizi mabaya ya mkazo huweza kusababisha matamshi yasiyo sahihi au kubadili kabisa maana ya neno.

Lafudhi ni matamshi ya mtu au jamii ya watu yatokanayo na utamkaji wa maneno ya lugha wanayoitumia. Ni matamshi ya mtu binafsi au jamii ambayo huwapa utambulisho wa kijamii au kieneo. Hivyo, huweza kumtambulisha mtu au jamii kijiografia kwa sababu ya athari za kimazingira. Kupitia lafudhi, mtu anaweza kutambulika kuwa ametoka katika jamii ya Kisukuma, Kipare, Kiarabu, Kihindi, au Kizungu. Aidha, kupitia lafudhi, eneo analotoka mzungumzaji, kama vile Mara, Mtwara, Kilimanjaro, Arusha, au Pwani huweza kutambuliwa kutokana na anavyotamka maneno.

**Kazi ya 3.8**



Sikiliza mazungumzo mbalimbali yenye matamshi na lafudhi mchanganyiko, kisha bainisha matamshi na lafudhi hizo kimaandishi ukizilinganisha na lafudhi ya Kiswahili Sanifu.




KISWAHILI FINAL.indd 21 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

## Utata katika mawasiliano

### Kazi ya 3.9

**Chunguza picha zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.**




FOR ONLINE USE

**Maswali**

1. Bainisha matendo na majina ya vitu vinavyoonekana katika picha.
2. Bainisha maana tofauti zinazopatikana kutokana na picha.
3. Maana ulizozibainisha katika swali la pili zinadhihirisha tabia gani ya maneno?
4. Tunga sentensi moja kwa kila picha iliyopo katika kazi ya 3.9.


**Zingatia**

Utata ni hali ya neno au kifungu cha maneno kuwa na maana zaidi ya moja. Utata, katika mawasiliano, hutokea pale maneno au sentensi zinapokuwa na maana zaidi ya moja na, hivyo, kusababisha msikilizaji au msomaji ashindwe kuelewa maana iliyokusudiwa. Kuna utata wa kimsamiati na kimuundo. Utata wa kimsamiati hujitokeza katika ngazi ya neno na utata wa kimuundo huweza kujitokeza katika vifungu vya maneno kama vile virai, vishazi, na sentensi.



KISWAHILI FINAL.indd 22 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate




**Kielelezo Namba 3.1:** *Aina za utata*

Utata wa kimsamiati hujitokeza pale neno moja linapokuwa na maana zaidi ya moja. Kwa mfano, neno **ua** huweza kuwa na maana ya kutoa uhai wa kiumbe, sehemu ya mmea inayochanua, au wigo uliojengwa kuzunguka nyumba. Utata wa kimuundo hujitokeza pale kifungu cha maneno kama kirai au sentensi kinapokuwa na maana zaidi ya moja. Kwa mfano, tazama sentensi ifuatayo:

Amelala kwenye nyumba ya wageni.

Sentensi hiyo ni tata kwa sababu ina maana tatu. Mosi, nyumba alimolala hutumiwa na wageni kulala kwa malipo. Pili, amelala kwenye nyumba ambayo inamilikiwa na wageni, yaani watu wasio wenyeji wa eneo hilo. Tatu, amelala kwenye nyumba iliyoandaliwa mahususi kwa ajili ya malazi ya wageni.

Utata katika lugha huweza kusababishwa na mambo mbalimbali. Baadhi ya mambo hayo ni matumizi ya neno lenye maana zaidi ya moja, matumizi ya mofu ya kauli ya kutendea {i}, utamkaji wa maneno usio sahihi, na mpangilio wa maneno katika sentensi.

FOR ONLINE USE ONLY

Ili kuepukana na makosa hayo, mtumiaji wa lugha anapaswa kuzingatia mambo kadhaa. Kwanza, kuweka mkazo mahali panapostahili katika neno ili kuonesha kwamba silabi ipi ina mkazo. Pili, kutumia kwa usahihi alama za uandishi (kama vile mkato, nukta, alama ya kuuliza, na mshangao). Tatu, kuepuka mpangilio wa maneno katika sentensi wenye kuleta utata. Nne, kuteua vizuri maneno na kuyafafanua kulingana na muktadha. Tano, kuzingatia upatanisho wa kisarufi na kutumia kwa uangalifu lugha ya picha kadiri ya muktadha na hadhira.

**Kazi ya 3.10**

1. Chunguza maneno na sentensi zifuatazo, kisha bainisha utata unaojitokeza kwa kutoa maana mbili kwa kila neno.
   (a) shinda
   (b) ndege
   (c) fua
   (d) kiboko

Fot online use only
do not duplicate

(e) buni
(f) dumu
(g) kamba
(h) jua
(i) kaa
(j) jaa
(k) vua
(l) panda

2. Chunguza sentensi zifuatazo, kisha bainisha utata unaojitokeza kwa kutoa maana mbili kwa kila sentensi.
   (a) Kazamwendo alilalia uji.
   (b) Mama alimpigia Lutendege simu.
   (c) Baba Mwajuma atafika kesho.
   (d) Mama ananijali zaidi kuliko baba.
3. Onesha namna ya kuondoa utata ulioubainisha katika swali la kwanza na la pili.

## Zoezi la marudio la 3

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

(i) Utokeaji wa misimu katika jamii hutegemea ...............
   (a) uchaguzi wa viongozi
   (b) mabadiliko ya kijamii
   (c) shughuli itendekayo
   (d) utani uliopo miongoni mwa wanajamii
   (e) kutumika na kudumu kwa muda mrefu

FOR ONLINE USE ONLY

(ii) Tatizo la kushindwa kutamka vizuri maneno husababishwa na ...................
   (a) kuzungumza sana
   (b) kuzungumza lugha zaidi ya moja kwa ufasaha
   (c) kuwa na visawe vingi

Fot online use only
do not duplicate

(d) kutumia mkazo

(e) kuathiriwa na lugha mama

(iii) Ili kuepuka utata katika tungo, ni muhimu ................

(a) kuepuka matumizi ya maneno yenye maana zaidi ya moja

(b) kutumia nahau

(c) kutumia aina zote za maneno katika tungo

(d) kutumia alama za uandishi

(e) kutumia mofu ya kauli ya kutendea

(iv) Nyenzo kuu ya lugha ya mazungumzo ni ................

(a) usimuliaji

(b) mdomo

(c) maandishi

(d) vitendo

(e) ishara

FOR ONLINE USE ONLY

(v) Ipi ni sababu mojawapo ya kutumia lugha kulingana na muktadha?

(a) Kuzuka kwa matukio mbalimbali

(b) Kuendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia

(c) Kumudu shughuli inayofanyika

(d) Kupamba mazungumzo

(e) Kuwezesha mawasiliano

Fot online use only
do not duplicate

2. Oanisha maelezo yaliyopo fungu A na dhana zilizopo fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi ili kukamilisha maana.

| **Fungu A** | **Fungu B** |
|---|---|
| (i) Mitindo tofauti ya lugha katika miktadha mbalimbali | A. lugha ya hospitalini |
| (ii) Upekee wa kundi la watu na shughuli inayofanyika | B. mkazo |
| (iii) Kupamba lugha, kuficha ujumbe, kukuza lugha | C. dhima za rejesta |
| (iv) Kutwa mara tatu | D. lugha ya mahakamani |
| (v) Mheshimiwa hakimu | E. chanzo cha rejesta |
| | F. misimu |
| | G. rejesta |

3. Eleza dhima za misimu katika lugha ya Kiswahili.
4. Bainisha dhima za rejesta.
5. Fafanua sifa za lugha ya mazungumzo.
6. Tofautisha rejesta na misimu.
7. Kwa ufupi, eleza mambo yanayotofautisha lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi.
8. Kwa kutumia mifano, eleza aina za kiimbo katika lugha ya Kiswahili.
9. Utata katika tungo za Kiswahili unaweza kuondolewa kwa namna gani?
10. Eleza umuhimu wa kutumia lugha kulingana na miktadha mbalimbali.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI FINAL.indd 26 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

# Sura ya Nne

## Uhakiki wa kazi za fasihi simulizi

### Utangulizi

*Uhakiki wa kazi za fasihi ni uchambuzi ambao hufanywa kwa kuzingatia vipengele vya fani na maudhui ili kujua namna kazi husika ilivyowasilishwa pamoja na kilichowasilishwa. Katika sura hii, utajifunza kuhakiki kazi za fasihi simulizi, hususani mashairi na maigizo. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuchambua kazi mbalimbali za fasihi simulizi na kuelewa namna zilivyowasilishwa pamoja na mambo yaliyowasilishwa.*

### Kazi ya 4.1

**Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Sifa za Kiswahili**

FOR ONLINE USE ONLY

1. Kiswahili lugha safi, lugha iso na mzozo,
Imetoka kwenye ghafi, imeshika muongozo,
Ni tajiri kwa sarufi, na stadi zifunzazo,
Hakika ndiyo johari, lugha yetu Kiswahili.

2. Lugha yetu ina nguvu, hakika twajivunia,
Tena ni lugha angavu, elimu kufundishia,
Inatupa ushupavu, sote tunaisifia,
Ni amali na johari, lugha yetu Kiswahili.

3. Kiswahili kina nuru, kimetutoa gizani,
Tukaupata uhuru, umoja nayo amani,
Wachache wanakufuru, wageni wakitamani,
Ni amali na johari, lugha yetu Kiswahili.

4. Yatupasa kushukuru, kimeondoa mizozo,
Kimetwangazia nuru, hakuna mnyong'onyezo,



KISWAHILI FINAL.indd 27 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

Tukaupata uhuru, na furaha mzomzo,
Ni amali na johari, lugha yetu Kiswahili.

5. Lugha hii ina nguvu, tuipe msisitizo,
Tena ni lugha shupavu, ipewe muendelezo,
Imejaa uangavu, uliojaa uwezo,
Ni amali na johari, lugha yetu Kiswahili.

6. Ni lugha yenye ushindi, Tanzania yetu nguzo,
Imetawala makundi, japo wapo wenye bezo,
Ila wengi walo ndani, na wa nje ni tukuzo,
Ni amali na johari, lugha yetu Kiswahili.

7. Leo sisi ni taifa, twajuliwa pande hizo,
Kiswahili kimasafa, ki mbele ya nyinginezo,
Chadumisha yetu sifa, na shufaa tuko nazo,
Ni amali na johari, lugha yetu Kiswahili.

8. Hapa natia komeo, ishara ya kibwagizo,
Ni ishara ya kituo, mwisho wa muendelezo,
Nashika fumo na ngao, nimeziimba sifazo,
Ni amali na johari, lugha yetu Kiswahili.

FOR ONLINE USE ONLY

**Chanzo:** Nuru (1975:57 - 58), limeboreshwa na TET.

**Maswali**

1. Kila ubeti wa shairi ulilolisoma una vipande vingapi vya mshororo?
2. Kila kipande katika mshororo kina silabi ngapi?
3. Lugha iliyotumika katika shairi hili ni ya aina gani?
4. Ni ujumbe gani ulioupata kutokana na shairi ulilolisoma?
5. Umegundua vitu gani vinavyofanana katika shairi ulilolisoma?
6. Je, vitu ulivyovigundua katika swali la 5 vinaitwaje?

Fot online use only
do not duplicate


**Zingatia**

Kuhakiki ni kitendo cha kuchambua fani na maudhui ya kazi za fasihi ili kupata ujumbe uliomo katika kazi hizo na ufundi wa kisanaa uliotumika kufikisha ujumbe huo. Uhakiki wa kazi ya fasihi hautoki katika ombwe wala haufanywi kiholela. Mhakiki afanyapo kazi yake, hutathmini, hueleza, huainisha, na hutoa maoni kuhusu kazi ya fasihi kwa kuongozwa na kanuni na taratibu mbalimbali. Miongoni mwa taratibu hizo ni: Kuzingatia vipengele vya fani na maudhui, kueleza ubora na udhaifu wa kazi husika kwa kuzingatia hali halisi ya jamii, na kueleza ukweli na umuhimu wa mambo yanayoelezwa kwa jamii.

Uhakiki una dhima mbalimbali. Miongoni mwazo ni kuweka bayana mafunzo yaliyomo katika kazi ya fasihi, kujua ubora na udhaifu wa kazi za fasihi, kuwasaidia wasomaji kuielewa kazi ya fasihi kwa urahisi, na kukuza kazi za fasihi. Aidha, uhakiki hushirikisha fikra za kihakiki katika kazi za fasihi na kuweka bayana kila kipengele cha fani na maudhui. Katika fasihi simulizi, uhakiki hufanyika kwa kuzingatia vipengele vya fani na maudhui kama vinavyoonekana katika Kielelezo Namba 4.1.

FOR ONLINE USE ONLY

Fot online use only
do not duplicate




**Kielelezo Namba 4.1:** *Vipengele vya uhakiki wa fasihi simulizi*

## Uhakiki wa kazi za ushairi

**Kazi ya 4.2**

Kusanya kanda na vinasasauti vilivyohifadhi kazi za ushairi, kisha sikiliza na uchambue vipengele vya maudhui vinavyojitokeza katika kazi hizo.



KISWAHILI FINAL.indd 30 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Zingatia**

Katika uhakiki wa kazi za ushairi, mhakiki huchambua jinsi kazi hizo zinavyowasilishwa pamoja na yanayowasilishwa. Kazi za ushairi huhusisha nyimbo, tenzi, mashairi, na ngonjera. Uhakiki wa fani kama unavyooneshwa katika Kielelezo Namba 4.1, unahusu vipengele vitano ambavyo ni muundo, mtindo, matumizi ya lugha, wahusika, na mandhari.

Katika ushairi, **muundo** ni mjengo, mpangilio, au sura ya kazi ya ushairi. Mjengo huo hubainishwa kutokana na jinsi mtunzi alivyoteua na kupangilia vipengele mbalimbali. Kwanza, muundo hubainishwa kwa *idadi ya mizani*. Mizani ni idadi ya silabi katika mshororo wa ushairi. Idadi ya mizani zinazounda mishororo hutofautiana kulingana na kipera kinachohusika. Kwa mfano, mshororo wa mashairi ya kimapokeo huwa na mizani kumi na sita, lakini mshororo wa tenzi huwa na mizani nane. Ukichunguza mshororo ufuatao, kutoka ubeti wa kwanza wa shairi la 'Sifa za Kiswahili' lililoko katika sura hii utabaini mizani hizo kumi na sita.

|Ki|swa| hi| li| |lu|gha| |sa| fi|, |lu|gha| |i| so| |na| |m| zo| zo|
1 2 3 4 5 6 7 8 9 10 11 12 13 14 15 16

Kadhalika, ukichunguza mshororo ufuatao, kutoka ubeti wa pili wa utenzi wa Uzindushi ulioko katika sura ya tano, idadi hiyo ya mizani nane inadhihirika.

|Ha| ta| |u| ki| wa| |na| |ma| li|
1 2 3 4 5 6 7 8

Pili, muundo hubainishwa kwa *vina*. Vina ni silabi za kati na za mwisho katika mshororo. Tunapochunguza vina, tunaangalia urari wa vina hivyo. Urari huu huangaliwa baina ya vina vya kati na vya mwisho. Kadhalika, urari huangaliwa katika idadi ya mizani. Katika mshororo, urari wa vina na mizani hujitokeza katika tungo zote za ushairi, isipokuwa kwa baadhi ya tungo za ushairi wa kisasa. Tazama mfano wa ngonjera ifuatayo:

FOR ONLINE USE ONLY

**Mjomba:** Zipo sheria adhimu, tulia usihukumu,
Hilo mbona halidumu, wazazi usituhumu,
Wewe ikuze nidhamu, utaishika kalamu,
Msingi ukimaliza, sekondari utakwenda.

**Beatu:** Mjomba nimeelewa, yote uliyonambia,
Mzigo umenituwa, nilikuwa naumia,
Nadhani utatatuwa, janga kwenye familia,
Uduni wangu udogo, ngeweza fuatilia.

**Chanzo:** Mbijima (2020:39).



KISWAHILI FINAL.indd 31 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

Katika mfano huu wa ngonjera, vina vimewekwa kwa urari. Katika ubeti wa kwanza, kina cha kati katika mishororo mitatu ya kwanza ni 'mu' na kina cha mwisho ni 'mu'. Kadhalika, katika ubeti wa pili, kuna urari wa vina. Kina cha kati ni 'wa' katika mishororo mitatu ya kwanza na kina cha mwisho ni 'a.'

Tatu, muundo pia hubainishwa kwa *beti* zinavyojengwa. Tunapohakiki muundo wa kazi za ushairi, tunazingatia idadi ya mishororo inayounda kila ubeti wa kazi husika. Tofauti ya idadi ya mishororo katika beti huibua miundo mbalimbali. Shairi lililoundwa kwa beti za mshororo mmojammoja huitwa tathmina, lenye beti zenye mishororo miwilimiwili huitwa tathinia na lenye beti zenye mishororo mitatumitatu huitwa tathlitha. Mashairi yaliyoendelezwa na kuzoeleka zaidi katika Kiswahili ni yale yenye mishororo minneminne ambayo huitwa tarbia, na yenye mishororo mitanomitano ambayo huitwa takhmisa. Shairi lenye mishororo zaidi ya mitano huitwa sabilia.

Nne, muundo hubainika pia kwa kuangalia *vipande* ambavyo ni sehemu ya mshororo katika shairi. Kwa kawaida, kipande kimoja na kingine hutenganishwa kwa alama ya mkato. Uhakiki wa muundo wa kazi za ushairi huhusisha idadi ya vipande vinavyojenga kazi hizo kwa kuwa idadi ya vipande inaweza kutofautiana baina ya vipera vya ushairi. Kwa kawaida, mashairi na ngonjera huwa na vipande viwili na tenzi huwa na kipande kimoja katika kila mshororo. Kwa upande wa nyimbo, idadi ya vipande hutegemeana na matakwa ya mtunzi. Hata hivyo, nyimbo nyingi huwa na kipande kimojakimoja. Kama ubeti unapaswa kurudiwa, kipande cha mwisho huwekewa alama ya kuzidisha na idadi ya marudio yanayotakiwa huoneshwa kwa namba. Kwa mfano, huandikwa ×2 au ×3. Tazama mfano wa wimbo ufuatao:

FOR ONLINE USE ONLY

**Mazingira**

Pamoja mimi nawe
Tuyatunze mazingira
Hata sisi watoto eeh
Tuyapende mazingira

*Mazingira yetu*
*Tuyatunze tuyalinde*
*Yanaharibika*
*Tuyatunze tuyalinde x2*

Mafuriko, kimbunga husababishwa
Na tofauti ya mazingira, aaah
Hali ya hewa kuwa mbaya, husababishwa
Na tofauti ya mazingira, aaah



KISWAHILI FINAL.indd 32 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

Moshi wa viwanda, ukomeshwe
Malighafi sandarusi, zikomeshwe
Utupaji wa taka, uboreshwe
Ukataji miti, ukomeshwe
Uchomaji misitu, ukomeshwe
Uvuvi haramu, ukomeshwe

**Chanzo:** Namite Giuseppe (Di Namite).

Katika beti hizi za wimbo, ubeti wa kwanza una kipande kimojakimoja katika kila mshororo, ilihali katika ubeti wa pili na wa tatu, kuna vipande viwiliviwili katika kila mshororo. Hali hii ya kutofautiana kwa idadi ya vipande hutegemea matakwa ya mtunzi.

Tano, mhakiki anaweza kubaini muundo wa kazi ya ushairi kwa kuchunguza *kituo*. Kituo ni mshororo wa mwisho katika ubeti. Mshororo huo ni kimalizio au kiini cha kazi ya ushairi. Kituo kinakuwa kiini iwapo kimerudiwa katika beti zote. Mshororo unaporudiwarudiwa katika beti zote huitwa *kituo bahari*. Tazama mfano ufuatao:

**Umuhimu wa elimu**

Tuitafute elimu, vitabu vyote vyasema,
Ni kitu kilo muhimu, kwa maisha yako mema,
Tuipate na idumu, ijenge yalo hekima,
Elimu dira sahihi, ongoza yetu maisha.

Elimu kwetu ni mali, uishike ninasema,
Haitaki ukatili, ya kutaka kuwa mwema,
Maisha kuyakabili, kuyafanya yalo mema,
Elimu dira sahihi, ongoza yetu maisha.

Katika shairi la 'Umuhimu wa elimu' hapo juu, mshororo wa mwisho ambao ni "elimu dira sahihi, ongoza yetu maisha," ni kituo bahari kwa sababu umerudiwa katika beti zote.

Sita, muundo wa kazi ya ushairi hubainika kupitia *muwala*. Muwala ni mtiririko mzuri wa mawazo kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. Mtiririko huo hukamilisha maana ya shairi zima.

Saba, muundo wa kazi za ushairi hubainishwa kwa *utoshelevu*. Utoshelevu ni hali ya ubeti kujikamilisha kimaana bila kutegemea kukamilishwa na ubeti mwingine. Uhakiki wa mashairi huzingatia utoshelevu wa ubeti mmoja. Katika

Fot online use only
do not duplicate

utenzi, utoshelevu hubainika kutokana na mjumuisho wa beti zinazounda utenzi huo ambazo huibua wazo moja. Katika nyimbo na ngonjera, utoshelevu hujidhihirisha katika ubeti mmoja au mfululizo wa beti kutegemeana na kusudio la mtunzi.

**Mtindo** ni upekee wa utunzi unaojibainisha katika kazi husika. Upekee huo humtofautisha mtunzi mmoja na mwingine na hujipambanua katika namna mbalimbali. Kwa mfano, mtunzi anaweza kutumia mtindo wa kurudiarudia silabi mbili za mwisho za mshororo na mwingine anaweza kufupisha maneno au silabi za mshororo. Upekee huu ndio huchunguzwa na kubainishwa wakati wa uhakiki wa kazi za ushairi.

**Matumizi ya lugha** ni kipengele kingine cha uhakiki ambapo mhakiki huchunguza masuala mbalimbali yanayohusiana na namna lugha ilivyotumika. Kwanza ni *mpangilio wa maneno*. Kazi ya ushairi huweza kuwa na mpangilio wa maneno ulio tofauti na kazi zingine za fasihi simulizi. Wakati mwingine, kazi ya ushairi hufupisha au kugeuza mpangilio wa maneno unaokubalika kisarufi. Pili ni *matumizi ya lugha ya picha* au *taswira*. Mhakiki huchunguza namna mshairi alivyotumia maneno yanayojenga picha ya kitu au hali fulani katika akili ya msomaji, hivyo kupata ujumbe uliokusudiwa. Kwa mfano, matumizi ya neno **wazururaji** hutupatia picha ya watu wanaotembea tu bila kufanya kazi. Tatu ni *matumizi ya tamathali za semi* kama vile takriri, sitiari na tashihisi ambazo hutumika katika shairi. Mshairi huweza kutumia tamathali za semi kwa lengo fulani kama vile kupamba kazi yake, kuficha maana, kuweka msisitizo wa jambo fulani, au kuleta athari fulani aliyoikusudia. Nne ni *matumizi ya lugha ya mkato*. Mhakiki huchunguza jinsi mshairi alivyotumia ufundi wake kukatisha maneno au tungo ili kutimiza idadi ya mizani. Neno huweza kukatwa kwa kudondosha baadhi ya herufi au silabi. Kwa mfano, katika shairi la 'Umuhimu wa elimu' kuna kipande cha "Ni kitu kilo muhimu" ambacho kimekatisha neno "kilicho" na kuwa "kilo". Tano ni *matumizi ya semi* kama vile methali, nahau, misemo, na vitendawili. Mhakiki huchunguza aina ya semi zilizotumika, namna zilivyotumika, pamoja na jinsi zilivyosaidia kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa.

Katika kipengele cha **wahusika**, mhakiki huchunguza matumizi ya watu, wanyama, na viumbe wengine katika kazi za ushairi. Kwa mfano, katika diwani ya *Chungu Tamu*, ubeti wa tatu wa shairi la 'Thomasi na Doto,' mtunzi ametumia wahusika Roland na Rosalind.

Katika kipengele cha **mandhari**, mhakiki huchunguza mahali matukio ya kifasihi yanapotendekea. Mandhari huweza kuwa halisi kama vile baharini, njiani,



KISWAHILI FINAL.indd 34 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

msituni, kijijini, au mijini. Pia, huweza kuwa ya kufikirika kama vile kuzimu, mbinguni, au peponi. Tazama wimbo ufuatao:

Acha nibaki na raha zangu,
Kwa nini nisifurahi?
Kuzaliwa Tanzania, kwa baba na mama - ni kwetu!
Ni kisiwa cha amani, moyo hautetemeki - hakika,
Pita huku, nenda kule, wasiwasi haupati - ni uhuru,
Kote wendako nyumbani, iwe hata Zaramoni - umefika.

**Kiitikio:** *Nihame niende wapi?*
*Nimefika, siondoki.*
*Acha nipatunze kwetu!*
*Hatua tumezipiga, maishani,*
*Huoni miundombinu? Imejaa,*

Barabara za chuma, na majengo teletele - mazuri,
Maji yametapakaa, nyumbani kila mahali - masafi,
Shule nyingi zapendeza, zimesheheni majengo - na walimu,
Elimu mepanda juu, watu wameelimishwa - wasomi.

Katika wimbo huu, mandhari inayoonekana ni halisi ambayo ni Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY

**Maswali**

1. Wimbo huu una beti ngapi?
2. Sehemu ya kiitikio inatofautiana vipi na beti zilizopo?
3. Mtunzi anaposema “kote wendako amani” anamaanisha nini?
4. Pendekeza jina la wimbo huu.
5. Umepata ujumbe gani kutokana na wimbo huu?

**Zingatia**

Uhakiki wa maudhui ya kazi yoyote ya fasihi simulizi, ukiwamo ushairi, huhusisha vipengele anuwai kama ilivyoainishwa katika Kielelezo Namba 4.1. Navyo ni dhamira, mgogoro, ujumbe, falsafa, msimamo, na mtazamo. Mhakiki

Fot online use only
do not duplicate

huchunguza mawazo makuu yanayomsukuma mtunzi wa kazi husika kutunga kazi hiyo. Uhakiki wa ujumbe huangalia taarifa inayotolewa na mtunzi wa kazi za ushairi. Pia, hujumuisha mafunzo, fundisho, nasaha, au maonyo yatolewayo na watunzi wa kazi hizo. Vilevile, uhakiki wa maudhui huchunguza migogoro, yaani kuwapo au kutokuwapo kwa mivutano au misuguano baina ya mtu na mtu, mtu na nafsi yake, mtu na kikundi cha watu, mtu na hali fulani ya maisha, na jamii na jamii.

Uhakiki wa maudhui pia huchunguza falsafa ya mtunzi. Ili kulifanikisha hili, mhakiki hubainisha tafakuri inayopatikana katika kazi ya ushairi kuhusu nyanja mbalimbali za maisha.

Katika kuhakiki mtazamo wa mtunzi wa kazi za ushairi, mhakiki huchunguza namna mtunzi anavyoyaona maisha kupitia kazi yake. Mtazamo huo unaweza kuwa halisi au dhahania. Pia, mhakiki huhakiki namna mtunzi anavyotetea jambo fulani au kulipinga akitaka mabadiliko katika jamii.

**Kazi ya 4.3**

Hakiki vipengele vya fani na maudhui katika shairi la Sifa za Kiswahili.

**Zoezi la 4.1**

FOR ONLINE USE ONLY

1. Bainisha vipengele vikuu viwili vinavyozingatiwa katika uhakiki wa shairi.
2. Kwa ufupi, eleza vipengele vya uhakiki wa fani katika ngonjera.
3. Fafanua vipengele vya uhakiki wa maudhui katika nyimbo.

## Uhakiki wa maigizo

**Kazi ya 4.4**

**Soma igizo lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Tiamaji:** (*Anatembea akipepesuka mithili ya mtu mwenye njaa.*) Ohaa! Mbona mnazingua wana?

**Odongo:** Kimya mwana, usizingue! Tunatafakari tunavyopigika tu. (*Anajikuna kichwani.*)

Fot online use only

**Tiamaji:** (*Anamsogelea Odongo.*) Mwanaume … umepata mchongo? Wewe ndiwe chuma changu. Ulinipokea mjini. (*Anajisogeza jirani na Odongo huku akiimba.*)

**Sugaya:** (*Anazinduka usingizini na kunyanyuka mtaroni huku akiwa amebeba kipande cha boksi.*) Mshua unazingua … umenipigia makelele hadi nimeamka. Nilitaka nilale zaidi ili nisahau njaa niliyolala nayo; sasa umenitingisha. Haya, nifichie hili godoro langu manake juzi mwizi kapita. (*Ananyoosha mkono kwa Tiamaji akimpa kipande cha boksi chenye unyevu.*)

**Odongo:** (*Anainuka, huku akiimba na kucheza. Suruali yake imeraruliwa, mguu mmoja mrefu na mwingine mfupi.*) ... twende tukawinde, leo … tukawinde vipepeo …

**Tiamaji:** (*Anamtolea jicho Odongo.*) Nitakuzingua. Achana na wimbo wangu mwana. Niliutunga mwenyewe tangu nikiwa bushi. (*Odongo anaendelea kuimba. Hajali.*) Mwana, hunisikii? (*Anainuka kumfuata Odongo na kumshika shati.*) Odongo anampiga ngumi mgongoni. Wanavutana kwa takribani dakika tatu na kuangushana.

**Sugaya:** (*Anaamka.*) Ohaa! Nyie masela vipi? Ha ha haa! (*Anacheka kwa sauti kubwa, anawasogelea na kuwaachanisha; kila mmoja akielekea mbali kidogo na mtaro wautumiao kama malazi.*)

**Odongo:** (*Baada ya dakika mbili, anawasogelea wenzake kama vile anataka kuwasemesha, lakini Sikitu anamwahi kusema.*)

**Sikitu:** "Duu! Hivi sisi tumemkosea nini Muumba? Tunaishi mitaroni tangu wadogo hadi twazeeka. Leo tujitahidi walau tuambulie ukoko kwa mamantilie. Mama Wawili hana choyo. Atatugea tu.

**Odongo:** Au siyo! Yule ndiye mdau wetu wa misosi. Jana wajanja walituwahi tukakosa mazagazaga wakatulaza njaa. (*Anaingiza mkono mfukoni na kutoa noti ya shilingi elfu kumi akionesha kuwaringishia wenzake.*)

**Sugaya:** Aaah! Mshua umetoa wapi mapene yote hayo?

**Odongo:** Mtoto wa kitaa haulizwi maswali mepesi kama hayo. Nililala njaa na utajiri wangu.

**Sugaya:** Poa mwana! (*Anasimama akizungukazunguka, kisha anaongea kama vile hataki.*) Mwana, sisi wenzako tulishaacha kupiga ganja na wewe ni bora uache! Linazeesha na kuchosha akili.



KISWAHILI FINAL.indd 37 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Sikitu:** (*Ghafla, anamwona askari polisi kwa mbali. Anawapa ushauri.*) Wanangu, tuamshe. Hawa hawana urafiki na mtu.

**Tiamaji, Odongo, Sugaya, Sikitu:** (*Wote wanaondoka eneo hilo kuwakimbia polisi.*)

**Maswali**

1. Bainisha wahusika wa igizo hili.
2. Ni mafunzo gani unayapata kutokana na igizo hili?
3. Tabia zipi zimejitokeza katika igizo hili? Je, unadhani zinafaa kuigwa au la? Kwa nini?

**Zingatia**

Katika maswali uliyoyajibu, umebainisha vipengele vya fani na maudhui. Uhakiki wa maigizo hufanywa kwa kuzingatia vipengele hivyo, kama ilivyo kwa tanzu zingine za fasihi simulizi. Mtindo wa maigizo hutegemea uwezo wa wahusika katika utendaji wa jambo husika. Hivyo, mhakiki anapaswa kuchunguza jinsi watendaji wanavyowasilisha kipera husika. Mathalani, mhakiki huchunguza jinsi watendaji wanavyotumia vifaa kama maleba, filimbi, baragumu, au ngoma katika kuamsha hisia za hadhira. Pia, huangalia matumizi ya mbinu zingine za kisanaa kama vile wahusika kutumia nyimbo, na usimulizi ili kuwasisimua watazamaji.

Vilevile, mhakiki huangalia namna visa na matukio yanavyowasilishwa katika jambo linaloigizwa, mgogoro unaoibuliwa, na hitimisho la mgogoro linavyotolewa. Mtiririko wa matukio unapaswa uoneshe kama ni wa moja kwa moja au ni wa rejea, yaani unakwenda mbele na kurudi nyuma.

Pia, mhakiki huangalia mandhari, yaani sehemu, mazingira au muktadha ambamo visa na matukio hutendekea. Mandhari huweza kuwa halisi (kama vile mtoni, porini, shambani, au msituni) au ya kufikirika (kama vile kuzimu, mbinguni, au peponi). Mhakiki hana budi kujiuliza iwapo igizo linadhihirisha wakati au mahali halisi ambapo hadhira hushirikishwa katika utendaji.

Mbali na vipengele vya mtindo na mandhari, mhakiki pia huchunguza uwezo wa mtunzi wa maigizo katika kuwajenga wahusika wake kisanaa ili waweze kuibua hisia mbalimbali katika usimulizi au utendaji wao. Usimulizi au utendaji hutegemea aina na uwasilishaji wa igizo. Wahusika huweza kutumia vifaa au vitu vingine kwa kuzingatia muktadha wa utendaji. Kwa mfano, katika kipera cha majigambo, wahusika ni watambaji ambao hujigamba au kujisifia kutokana na matukio na matendo waliyoyafanya. Mtambaji ambaye aliweza kumuua simba



KISWAHILI FINAL.indd 38 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

ili asiwadhuru wanakijiji anaweza kujigamba kwa kutumia mkuki na kuonesha matendo aliyoyafanya. Katika kuhakiki maigizo, ni vyema mhakiki akachunguza wahusika kwa kuongozwa na maswali yafuatayo: Wahusika wanasimulia au wanatenda? Wahusika wanatumia lugha gani au maneno gani kuamsha hisia kwa watazamaji? Wahusika wanahamasisha jambo gani katika jamii? Wahusika wamejengwa kikamilifu? Wahusika wanawakilisha nini au nani? Wahusika wanatumia vifaa au ala gani na zina umuhimu gani?

Kadhalika, mhakiki wa maigizo hushughulikia vipengele muhimu vya uchambuzi wa lugha iliyotumika. Vipengele hivyo ni semi, nahau, misemo, methali, vitendawili pamoja na uteuzi mzuri wa maneno.

Katika kipengele cha maudhui, mhakiki hutakiwa kuchunguza vipengele vyote vya kimaudhui ambavyo ni migogoro, dhamira, ujumbe, mtazamo, msimamo, na falsafa. Yote hayo kwa pamoja ndiyo humsaidia mhakiki kubaini ukinzani wa igizo na maisha halisi ya jamii ambayo ndiyo hadhira ya igizo hilo.

**Kazi ya 4.5**



Igiza na wenzako darasani kuhusu mada ya uchaguzi wa serikali ya wanafunzi, kisha, bainisha vipengele vya kifani na kimaudhui vilivyomo katika igizo hilo.

FOR ONLINE USE ONLY

**Zoezi la 4.2**

1. Eleza tofauti ya muundo wa mashairi na wa maigizo.
2. Uhakiki wa matumizi ya lugha katika maigizo huzingatia vipengele gani?
3. Tofautisha uwasilishaji wa mashairi na wa maigizo.
4. Ainisha vipengele vya fani vinavyohakikiwa katika maigizo.
5. Kwa kifupi, eleza maana ya istilahi zifuatazo:
   (a) fani
   (b) maudhui
   (c) mtindo
   (d) muundo
   (e) mandhari
   (f) mafunzo
   (g) ujumbe
   (h) dhamira
   (i) mgogoro
   (j) falsafa
6. Fafanua vipengele vya kuzingatia wakati wa uhakiki wa maudhui katika maigizo.



KISWAHILI FINAL.indd 39 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Zingatia**

Baada ya mhakiki kuchambua kazi ya fasihi kwa kuzingatia vipengele vyote vya fani na maudhui ya kazi za ushairi na maigizo, anatakiwa kupima kufaa au kutofaa kwa kazi husika. Kufaa au kutofaa kwa kazi ya fasihi simulizi kunajumuisha uhalisi wa kazi hiyo, umuhimu wa mambo yaliyosemwa na mtunzi, na uhalisi wake katika jamii. Maswali yafuatayo yatamsaidia mhakiki kupima kazi inayohusika:

(a) Mtunzi ametumia lugha kulingana na mawazo aliyoyaeleza?

(b) Kuna mpangilio mzuri wa vina, mizani, mishororo, beti, kituo, au visa ambavyo vinamsaidia msikilizaji kuelewa kazi husika?

(c) Wahusika waliomo katika ushairi au maigizo wanawakilisha mambo gani katika jamii?

(d) Mandhari iliyotumika inasaidia kutambua dhamira za mtunzi?

(e) Dhamira alizozijenga mtunzi zina uhalisi katika jamii?

(f) Ujumbe wa mtunzi una ukweli wowote katika maisha? Unafaa kulingana na mabadiliko yanayotokea katika jamii?

(g) Kazi ya fasihi simulizi inayohakikiwa ina umuhimu wowote kwa jamii iliyolengwa?

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la marudio la 4

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

(i) Uchambuzi wa kazi yoyote ya fasihi huzingatia vipengele gani vikuu viwili?

(a) Fani na muundo

(b) Fani na mtindo

(c) Fani na maudhui

(d) Falsafa na fani

(e) Muundo na maudhui



KISWAHILI FINAL.indd 40 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

(ii) Ni kipengele gani kati ya vifuatavyo hakijumuishwi katika uhakiki wa kazi za ushairi?

(a) Nyimbo

(b) Ngonjera

(c) Mashairi

(d) Majigambo

(e) Tenzi

(iii) Kipi kati ya vipengele vifuatavyo hakibainishi muundo?

(a) Mizani

(b) Vina

(c) Beti

(d) Kituo

(e) Bahari

(iv) Bainisha kipengele cha maudhui ambacho kinachunguza jinsi mtunzi wa kazi ya fasihi anavyoyaona maisha.

(a) Dhamira

(b) Ujumbe

(c) Mgogoro

(d) Mtazamo

(e) Falsafa

FOR ONLINE USE ONLY

(v) Utoshelevu na muwala ni vipengele vya ......................

(a) mtindo

(b) matumizi ya lugha

(c) muundo

(d) ujumbe

(e) falsafa

Fot online use only
do not duplicate

2. Oanisha maelezo yaliyopo fungu A na dhana zilizopo fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi ili kukamilisha maana ya kauli hizo.

| Fungu A | Fungu B |
|---|---|
| (i) Huweza kutumia vifaa au vitu vingine kwa kuzingatia muktadha wa utendaji | A. mandhari |
| (ii) Ujumbe, mafunzo, na mtazamo wa mtunzi wa kazi ya fasihi simulizi | B. muundo |
| (iii) Huwasilishwa kwa njia ya usimulizi na utendaji wa matukio | C. utenzi |
| (iv) Ni mazingira ya utendaji au usimulizi | D. matumizi ya lugha |
| (v) Semi, nahau, misemo, methali, vitendawili, na tamathali za semi | E. wahusika |
| | F. maudhui |
| | G. dhamira |

3. Fafanua vipengele vikuu viwili vya kuzingatia katika uhakiki wa kazi za ushairi na maigizo.

4. Chambua vipengele vya maudhui katika maigizo.

5. Eleza umuhimu wa wahusika katika maigizo na kazi za ushairi.

6. Uhakiki una umuhimu gani katika fasihi simulizi?

7. Bainisha umuhimu wa mandhari katika maigizo.

FOR ONLINE USE ONLY

Fot online use only
do not duplicate

# Sura ya Tano

## Utungaji wa kazi za fasihi simulizi

**Utangulizi**

*Jamii huweza kuburudika na kuelimika kupitia kazi mbalimbali za fasihi simulizi. Katika sura hii, utajifunza namna ya kutunga mashairi, tenzi, ngonjera, na maigizo kwa kuzingatia kanuni za utunzi wa kazi hizo. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutunga kazi za fasihi simulizi zenye dhima mbalimbali katika jamii.*

### Kutunga mashairi

**Kazi ya 5.1**

**Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Kama mnataka mali**

FOR ONLINE USE ONLY

1. Karudi baba mmoja, toka safari ya mbali,
Kavimba yote mapaja, na kutetemeka mwili,
Watoto wake wakaja, ili kumtaka hali,
Wakataka na kauli, iwafae maishani.

2. Akatamka mgonjwa, ninaumwa kwelikweli,
Hata kama nikichanjwa, haitoki homa kali,
Roho naona yachinjwa, kifo kimenikabili,
Semeni niseme nini, kiwafae maishani.

3. Yakawatoka kinywani, maneno yenye adili,
Baba yetu wa thamani, sisi tunataka mali,
Urithi tunatamani, mali yetu ya halali,
Sema iko wapi mali, itufae maishani.

4. Baba aliye kufani, akajibu lile swali,
Ninakufa maskini, baba yenu sina hali,



KISWAHILI FINAL.indd 43 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

Neno moja lishikeni, kama mnataka mali,
Kama mnataka mali, mtayapata shambani.

5. Wakazidi kumchimba, baba mwenye homa kali,
Baba yetu watufumba, hatujui fumbo hili,
Akili zetu nyembamba, hazijajua methali,
Kama tunataka mali, tutapataje shambani?

6. Kwanza shirikianeni, nawapa hiyo kauli,
Fanyeni kazi shambani, mwisho mtapata mali,
Haya sasa buriani, kifo kimeniwasili,
Kama mnataka mali, mtayapata shambani.

7. Alipokwishakutaja, fumbo hili la akili,
Mauti nayo yakaja, roho ikaacha mwili,
Na watoto kwa umoja, wakakumbuka kauli,
Kama mnataka mali, mtayapata shambani.

8. Fumbo wakatafakari, watoto wale wawili,
Wakakata na shauri, baada ya siku mbili,
Wote wakawa tayari, pori nene kukabili,
Kama mnataka mali, mtayapata shambani.

FOR ONLINE USE ONLY

9. Wakazipanda shambani, mbegu nyingi mbalimbali,
Tangu zile za mibuni, hadi zitupazo wali,
Na mvua ikaja chini, wakaona na dalili,
Kama mnataka mali, mtayapata shambani.

10. Shamba wakapalilia, bila kupata ajali,
Mavuno yakawajia, wakafaidi ugali,
Wote wakashangilia, wakakumbuka kauli,
Kama mnataka mali, mtayapata shambani.

Fot online use only
do not duplicate

11. Wakanunua na ng'ombe, majike kwa mafahali,
    Wakapata na vikombe, mashine na baiskeli,
    Hawakuitaka pombe, sababu pombe si mali,
    Kama mnataka mali, mtayapata shambani.

12. Wakaongeza mazao, na nyumba za matofali,
    Pale penye shamba lao, wakaihubiri mali,
    Wakakiweka kibao, wakaandika kauli,
    Kama mnataka mali, mtayapata shambani.

**Chanzo:** TET (1974).

**Maswali**

1. Beti za shairi ulilolisoma zimeundwa na mishororo mingapi kila mmoja?
2. Shairi lenye beti zenye idadi ya mishororo uliyoitaja katika swali namba 1 linaitwaje?
3. Bainisha vina vya kati vya ubeti wa 2 na wa 8.
4. Mshororo wa kwanza katika ubeti wa 5 una vipande vingapi?
5. Bainisha wahusika waliojitokeza katika shairi hilo.
6. Eleza mafunzo matatu uliyoyapata kutokana na shairi ulilolisoma.

FOR ONLINE USE ONLY

**| Zingatia |**

Kutunga ni kitendo cha kuunda au kuzua mawazo kwa kutumia fikira, kuyapanga mawazo hayo katika mtiririko unaofaa na kufikiria lugha itakayotumika katika kuyawasilisha ili yatoe ujumbe uliokusudiwa. Utungaji huweza kufanyika kwa njia mbili ambazo ni mazungumzo na maandishi. Utungaji wa kazi za fasihi huzingatia vipengele vikuu viwili ambavyo ni fani na maudhui.

Katika uwanja wa fasihi simulizi, fani ni umbo la nje la kazi ya fasihi. Fani hujumuisha muundo, mtindo, matumizi ya lugha, wahusika, na mandhari. Muundo ni mjengo, mpangilio, au sura ya kazi ya fasihi simulizi. Mtindo ni namna ambavyo mtunzi anaiwasilisha kazi yake. Matumizi ya lugha huhusu maneno ambayo fanani huteua na kuyatumia katika kazi yake. Wahusika ni watu, wanyama, na viumbe wengine ambao mtunzi wa fasihi simulizi huwatumia katika kufikisha kile alichokikusudia kwa hadhira yake. Mandhari ni mwonekano



KISWAHILI FINAL.indd 45 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

wa mahali ambapo kazi ya fasihi simulizi hutendeka. Mandhari hujumuisha miti, mito, milima, misitu, na sehemu nyingine.

Maudhui ni jumla ya mambo yote yanayoelezwa katika kazi ya fasihi simulizi. Kipengele hiki hujumuisha dhamira, mtazamo, msimamo, migogoro, falsafa, na ujumbe. Dhamira ni mawazo makuu yanayomsukuma mtunzi kutunga kazi yake. Pia, dhamira ni lengo kuu ambalo mtunzi wa kazi ya fasihi simulizi amekusudia kulifikisha. Mtazamo ni namna mtunzi anavyoyaona mambo yanayotendeka katika maisha. Msimamo ni namna mtunzi anavyoshikilia jambo. Migogoro ni hali ya kutoelewana kwa pande mbili. Falsafa ni imani ya mtunzi kuhusu maisha ya kila siku. Ujumbe ni taarifa yenye mafunzo inayopatikana katika kazi ya fasihi simulizi.

**Kazi ya 5.2**

Kusanya mashairi kutoka katika vyanzo vyovyote, kisha yawasilishe darasani.

**Zingatia**

Shairi ni utungo wa kisanaa wenye kutumia mpangilio maalumu wa maneno wenye lugha ya mkato, picha, na tamathali za semi. Mpangilio huo hutumia mapigo ya kimuziki ambayo hujengwa kwa urari wa vina, mizani, na muwala maalumu. Mtunzi wa mashairi hutakiwa kuzingatia kanuni maalumu za utungaji. Kanuni hizo ni kuwapo kwa mpangilio maalumu wa maneno, uzingatiaji wa muwala, matumizi ya lugha ya picha, matumizi ya tamathali za semi, hadhira, pamoja na muktadha. Kanuni nyingine ni matumizi ya vina, mizani, vipande, mishororo, vituo, na beti.

Ili kuweza kutunga shairi, mtunzi anapaswa kuwa na jambo la kutungia na kubuni jina la shairi linalowiana na maudhui. Pia, anapaswa kutumia urari wa mizani kumi na sita. Aidha, anapaswa kuteua maneno, misemo, methali, tamathali za semi, na lugha ya picha inayowiana na jambo analolitungia. Pia, mtunzi wa shairi anapaswa kutumia lugha ya mkato ili kusaidia kujenga urari wa mizani, na lugha ya mficho ili kuleta mvuto na kumfikirisha msomaji. Vilevile, anatakiwa kuchagua idadi ya mishororo atakayoitumia kujenga beti, idadi ya beti, idadi ya vipande, mizani, na aina ya kituo. Zaidi, anatakiwa kuchagua vina vya kati na vya mwisho.



KISWAHILI FINAL.indd 46 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

## Kazi ya 5.3

**Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Vijana wameamua, malengo yao kuweka,
Uvivu kuuondoa, mikakati wameweka,
Maisha kuyafungua, malengo kukamilika,
Maisha kufanya kazi, vijana wameamua.

Hakuna tena kucheza, kazi inahitajika,
Maisha ni kuyawaza, hali ikabadilika,
Wazazi kuwashangaza, na taifa kadhalika,
Maisha kufanya kazi, vijana wameamua.

1. Bainisha muundo wa shairi ulilolisoma.
2. Tunga shairi lenye beti nne zenye muundo kama wa shairi ulilolisoma, kisha bainisha:
   (a) Vina vya kati na vya mwisho; na
   (b) Kituo bahari.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la 5.1

1. Kwa ufupi, fafanua kanuni za utungaji wa mashairi.
2. Lugha ya mficho na ya mkato ina kazi gani katika shairi?
3. Soma ubeti ufuatao, kisha ongeza beti mbili za shairi hilo kwa kufuata mtiririko wa ubeti wa kwanza ukizingatia kanuni za utunzi wa mashairi.

   Dunia yachechemea, ikijawa na machozi,
   Gonjwa limetulemea, vilio kufanya kazi,
   Mifumo yote potea, imeingia ulozi,
   Gonjwawe umefikaje, rudi ulikotokea.



KISWAHILI FINAL.indd 47 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

## Kutunga utenzi

### Kazi ya 5.4

**Soma sehemu ya utenzi wa Uzindushi, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Uzindushi**

1. Uwapo mkakamavu,
Usiwe kwayo maovu,
Huo siyo uerevu,
Hata ukiwa na mali.

2. Sipende kuacha utu,
Kwa kutamania kitu,
Sijeitwa mtukutu,
Hata ukiwa na mali.

3. Na uvae upendeze,
Kama mwezi uangaze,
Akhi usijipumbaze,
Kujivika ujahili.

**Chanzo:** Abedi (1954:89), umeboreshwa na TET.

FOR ONLINE USE ONLY

**Maswali**

1. Bainisha idadi ya mizani iliyopo katika mishororo ya ubeti wa kwanza.
2. Mstari wa tatu katika ubeti wa pili una vipande vingapi?
3. Onesha vina vilivyopo katika ubeti wa pili.
4. Mtunzi ana maana gani anaposema, "Akhi usijipumbaze"?
5. Utenzi huu unazungumzia tukio gani?

**| Zingatia |**

Utenzi ni utungo wa kishairi ambao hueleza kwa kina kuhusu tukio fulani linalotokea au lililowahi kutokea kama vile matukio ya kihistoria au maisha ya watu. Aidha, utenzi huweza kutoa mawaidha. Ingawa utenzi wa mfano uliotolewa ni mfupi, kwa kawaida, utenzi huwa mrefu, kiasi cha beti 50 na kuendelea. Kimaudhui, utenzi huelezea dhamira moja kwa upana. Kifani, utenzi una sifa kama zile za mashairi. Tofauti ya utenzi na tanzu nyingine za ushairi ni kuwa na beti nyingi na kipande kimoja chenye mizani nane kwa kila mshororo. Miongoni mwa mambo ya kuzingatia wakati wa kutunga utenzi ni matumizi ya vina. Katika utenzi, vina hufanana katika mishororo mitatu ya mwanzo ya kila ubeti, lakini,

Fot online use only
do not duplicate

wakati mwingine, hubadilika ubeti hadi ubeti kutegemeana na uamuzi wa mtunzi. Mshororo wa mwisho ambao haubadiliki katika beti zote huitwa kituo bahari.

Kama yalivyo mashairi, tenzi zote huwa na beti zenye idadi mbalimbali za mishororo. Mishororo hiyo hujengwa kwa kipande kimoja tu. Tenzi nyingi huwa na beti zenye idadi ya mishororo isiyozidi minne. Utunzi wa tenzi pia huzingatia matumizi ya lugha ya picha na tamathali za semi. Pia, mtindo wake hujidhihirisha katika matumizi ya takriri zinazolenga kusisitiza jambo. Vilevile, mtindo huhusisha uteuzi wa maneno na mpangilio wa vina ili kubainisha upekee wa mtunzi.

Mwisho, katika utunzi wa tenzi, lazima kuwe na jambo la kutungia, jina la utenzi linaloendana na jambo linalowasilishwa, vina, mizani, na lugha ya mkato itakayokidhi kuelezea maudhui ya utenzi.

**Kazi ya 5.5**

Kwa kuzingatia taratibu za utunzi wa tenzi, tunga utenzi wenye beti tano kuhusu umuhimu wa barabara.

**Zoezi la 5.2**

1. Bainisha sifa za utenzi.
2. Utenzi hutofautianaje na shairi?

FOR ONLINE USE ONLY

## Kutunga ngonjera

**Kazi ya 5.6**

**Soma ngonjera ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Ujangili**

**Mandawa:** Hodi hodi uwanjani, mtambaji naingia,
Nilonge yalo moyoni, ukweli kuwapatia,
Wakubwa shikamooni, heshima nawapatia,
Wanyama pori tulinde, ujangili tokomeza.

**Manenge:** Nawaeleza ya moyo, yalojiri akilini,
Niwakonge zenu nyoyo, myaweke akilini,
Tuunganishe mioyo, tutunzieni vichwani,
Wanyama pori si kitu, ni bora waangamie.



KISWAHILI FINAL.indd 49 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Mandawa:** Wanyamapori hazina, tunu yetu kuwatunza,
Kipingamizi hakuna, kwa wanyama kuwekeza,
Faida nyingi kuona, kipato kukiongeza,
Wanyama pori tulinde, ujangili tokomeza.

**Manenge:** Usemalo sijaona, wanyama pori ni nini?
Faida zake hakuna, tuwalinde wao nani?
Hasara nyingi twaona, tusifichue kwa nini?
Wanyama pori si kitu, ni bora waangamie.

**Mandawa:** Vivutio vya nchini, hupendeza yetu macho,
Majirani watamani, kupata tulichonacho,
Tutilie maanani, kwa wanyama tuwe macho,
Wanyama pori tulinde, ujangili tokomeza.

**Manenge:** Tija zipi mwasemea, hasara wasababisha,
Vifo vingi hutokea, poteza watu maisha,
Chui, simba kitokea, watu rehani maisha,
Wanyama pori si kitu, ni bora waangamie.

FOR ONLINE USE ONLY

**Mandawa:** Wanyama ni watulivu, binadamu majangili,
Huwaua kiuovu, tena kwa njia katili,
Huendeleza uovu, kwa yetu rasilimali,
Wanyama pori tulinde, ujangili tokomeza.

**Manenge:** Usalama kutoweka, wanyama pori hatari,
Kifaru, tembo kumbuka, ni wanyama wa hatari,
Matatani kujiweka, kwa hawa wanyama pori,
Wanyama pori si kitu, ni bora waangamie.

**Mandawa:** Wanyama wana thamani, kutunzwa letu jukumu,
Watalii kuvuteni, fedha kigeni muhimu,
Mapato kuongezeni, kwa uchumi wa kudumu,
Wanyama pori tulinde, ujangili tokomeza.

Fot online use only
do not duplicate

**Manenge:** Sasa ndugu nakubali, wanyama pori kulinda,
Thamani yao ya kweli, yafaa sote kulinda,
Tutaneemeka kweli, ikiwa tutawalinda,
Wanyama pori tulinde, ujangili tokomeza.

**Mandawa:** Ngorongoro, Serengeti, twajivunia nchini,
Ujangili kiberiti, kwa wanyama hifadhini,
Tunu hii madhubuti, kwa pamoja tulindeni,
Wanyama pori tulinde, ujangili tokomeza.

**Wote:** Tamati tumefikia, pumziko kituoni,
Yote tuliyowambia, tahadhari chukueni,
Majangili twawambia, ujangili uacheni,
Tuwalindeni wanyama, kwa maisha endelevu.

**Maswali**

1. Bainisha wahusika waliojitokeza katika ngonjera ya Ujangili.
2. Onesha kina cha kati na cha mwisho katika ubeti wa tatu.
3. Eleza tofauti iliyopo kati ya ubeti wa mwisho wa ngonjera na beti zingine.
4. Mshororo mmoja wa beti za ngonjera uliyoisoma una jumla ya mizani ngapi?

FOR ONLINE USE ONLY

**Zingatia**

Mashairi ya majibizano baina ya pande mbili au zaidi kuhusu jambo fulani hujulikana kama ngonjera. Majibizano hayo huwa na malumbano yenye lengo la kutoa ujumbe maalumu kwa hadhira au jamii husika. Msemaji mmoja huuliza swali au hueleza jambo katika ubeti mmoja na mwingine hutoa jibu katika ubeti unaofuata. Majibizano ya hoja huendelea hivyo hadi kufikia mwafaka wa mada ya mjadala kwa upande mmoja kukubaliana na upande wa pili. Pia, ngonjera ina sifa ya kuwa igizo kwa sababu hutungwa na kutambwa jukwaani ikiambatana na matendo ya wahusika. Kwa upande wa fani, ngonjera zina vina, mizani, na kituo kama mashairi. Kutokana na sifa zake, ngonjera hupatikana katika utanzu wa ushairi na maigizo.

Utunzi wa ngonjera huzingatia matumizi ya vina, mizani, beti, mishororo minne,



KISWAHILI FINAL.indd 51 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

vitendo kulingana na muktadha, wahusika wawili au zaidi, na lugha ya kishairi. Aidha, ngonjera hutungwa kwa kuzingatia uteuzi wa mada ya kutungia, dhamira ya ngonjera, uteuzi wa wahusika wawili au zaidi, na kuwatengenezea maudhui yenye majibizano. Zaidi, ngonjera huzingatia matumizi ya kituo, muwala, utoshelevu, na uwasilishaji unaohusisha vitendo.

**Kazi ya 5.7**



Katika vikundi vya wanafunzi watano, tunga ngonjera ya beti tano kuhusu "Nafasi ya kilimo katika kuinua uchumi," kisha, wasilisha darasani na wenzako.

## Kutunga maigizo

**Kazi ya 5.8**



**Soma igizo lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Nufaida:** Hodi! (*Pazia linafunguliwa. Nufaida anaonekana akigonga mlango kwenye nyumba ya Ngineo kubisha hodi.*)

**Mafito:** Karibu! (*Anaitikia kwa haraka.*)

**Nufaida:** Mama Anna yupo?

**Mafito:** Ndiyo! (*Anaita.*) Ngineo.

**Ngineo:** Abee! Baba Anna, unasemaje? (*Anaitika kutoka uani.*)

**Mafito:** Kuna mgeni.

**Ngineo:** Nani?

**Mafito:** Njoo umwone!

**Ngineo:** Sawa! (*Anatoka uani kuja kumwona mgeni. Anakuta ni Nufaida.*) Habari za leo shoga yangu?

**Nufaida:** Nzuri! Unafanya nini shoga yangu?

**Ngineo:** Ninasimamia kazi ya kufua nguo. Nina dada wa kazi mdogo. Ninamsimamia anapofanya kazi. Yupo uani anafua marundo mengi ya nguo. Akimaliza, anadeki nyumba.

**Nufaida:** Mh! Mbona kazi nyingi. Unamlipa shilingi ngapi?

**Ngineo:** Simlipi chochote. Mshahara wake ni kula tu.

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI FINAL.indd 52 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Nufaida:** Ninaweza kwenda kumwona?

**Ngineo:** Unaweza shoga yangu. (*Wanatoka wote kuelekea uani ambako Kabala anafanya kazi.*) Ndiye huyu.

**Kabala:** Shikamoo! (*Anamsalimia Nufaida huku akiendelea na kazi ya kufua nguo.*)

**Nufaida:** Marahaba! (*Anaitikia salamu na kumwonea huruma. Anamwambia Ngineo watoke uani. Wanatoka uani kuelekea ndani ya nyumba.*)

**Ngineo:** Umemwona dada wa kazi?

**Nufaida:** Ndiyo! Mbona ni binti mdogo sana. Anasoma?

**Ngineo:** Hasomi. Asome tena! Kazi atamwachia nani?

**Nufaida:** Lo! Huoni kwamba unamtumikisha mtoto? Serikali imekataza ajira kwa watoto. Shoga yangu acha mara moja. Huyo mtoto alitakiwa awe shuleni. Kwa nini unamtumikisha namna hiyo? Acha kumtumikisha kuanzia sasa.

**Ngineo:** Siachi hata kidogo. Ngoja achape kazi mpaka akome!

**Nufaida:** Ninakwenda polisi kutoa taarifa. Itakula kwako ujue!

**Ngineo:** Utajiju! Eti unakwenda polisi. Nenda! Unamtisha nani? Eti itakula kwangu. Ha! Ha! Ha! Ha! Ha! Haaaa .... (*Anacheka kwa dharau.*)

**Nufaida:** Sawa. (*Anaondoka polepole. Siku inayofuata anakwenda Kituo cha Polisi cha Urafiki na kupokelewa na Afande Bahati.*)

**Afande Bahati:** Karibu! (*Anamkaribisha Nufaida.*)

**Nufaida:** Asante!

**Afande Bahati:** Unasemaje?

**Nufaida:** Nimekuja kutoa taarifa kuhusu utumikishwaji wa mtoto. Rafiki yangu aitwaye Ngineo anayeishi jirani na Kituo Kikuu cha Mabasi cha Ubungo anamtumikisha binti mdogo ambaye alitakiwa kuwa shuleni. Mbaya zaidi, hamlipi chochote.

**Afande Bahati:** Tunashukuru kwa taarifa. (*Anaita.*) Nzala!

**Afande Nzala:** (*Anaitika kwa nguvu.*) Ndiyo afande!

**Afande Bahati:** Huyu mama ameleta taarifa juu ya utumikishwaji wa



FOR ONLINE USE ONLY

Fot online use only
do not duplicate

mtoto mdogo. Mlalamikiwa ni Ngineo anaishi karibu na Kituo Kikuu cha Mabasi cha Ubungo. Chukua pingu ili tukamkamate.

**Afande Nzala:** Ndiyo afande! (*Anachukua pingu. Wanaondoka na Nufaida ili akawaoneshe mahali anapokaa mtuhumiwa. Wanafika nyumbani kwa mtuhumiwa.*)

**Afande Bahati:** Hodi! (*Anagonga mlango.*)

**Ngineo:** Karibu! (*Anatoka ndani. Anakutana na polisi na Nufaida. Anashtuka baada ya kuona polisi wakiwa na pingu.*)

**Afande Nzala:** Uko chini ya ulinzi. (*Anamkamata Ngineo mikono na kumfunga pingu.*)

**Afande Bahati:** Mama, unatuhumiwa kwa kumtumikisha mtoto.

**Ngineo:** Hapana! (*Anaongea huku akitetemeka. Anaondoka na polisi hadi Kituo cha Polisi.*)

**Afande Bahati:** Afande, mweke ndani.

**Afande Nzala:** Ndiyo afande! (*Ngineo anawekwa mahabusu. Baada ya muda, anatolewa kwa ajili ya kuhojiwa.*)

**Afande Bahati:** Afande, hebu mlete huyo mtuhumiwa ili tumhoji na kumfungulia mashitaka.

FOR ONLINE USE ONLY

**Afande Nzala:** Ndiyo afande! (*Anafungua mlango wa mahabusu. Ngineo anatolewa nje ili ahojiwe.*)

**Afande Bahati:** Mama hebu tueleze. Ilikuwaje?

**Ngineo:** Mimi nililetewa huyo binti na mama yake afanye kazi na niwape malipo kidogo. Mtoto mwenyewe alikataa shule.

**Afande Bahati:** Mama, huoni kwamba umevunja sheria?

**Ngineo:** Ninaomba msamaha.

**Afande Bahati:** Umevunja sheria makusudi. (*Anaandika maelezo ya Ngineo, kisha anamwambia Ngineo asaini.*

**Ngineo:** (*Anasaini.*)

**Afande Bahati:** (*Anaita.*) Nzala!

**Afande Nzala:** Ndiyo afande!



KISWAHILI FINAL.indd 54 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Afande Bahati:** Chukua hii hati ya maelezo ya mtuhumiwa. Mrudishe mahabusu na kesho tumpeleke mahakamani. (*Anamkabidhi hati ya mashitaka. Siku inayofuata, wanampandisha Ngineo kwenye karandinga kumpeleka mahakamani. Muda si mrefu, wanafika mahakamani na wanashuka kwenye karandinga. Wanaingia kwenye chumba cha mahakama.*)

**Polisi:** Kooorti! (*Hakimu anaingia na watu wote wanasimama.*)

**Hakimu:** Watu wote tukae sasa. (*watu wote wanakaa.*)

**Karani wa Mahakama:** (*Anaanza kuita kesi*) Kesi ya jinai Na. 2/2019, Jamhuri dhidi ya Ngineo Madulu Malulu.

**Ngineo:** (*Anasimamishwa kizimbani.*)

**Mwendesha Mashitaka:** Mheshimiwa, kesi leo imekuja kwa mara ya kwanza. Mshitakiwa Ngineo yupo. Mheshimiwa ninaomba kumsomea mshitakiwa hati ya mashitaka.

**Hakimu:** Sawa! Hebu msomee mashitaka.

**Mwendesha Mashitaka:** Ndiyo Mheshimiwa! (*Anajibu na kumsomea Ngineo mashitaka.*) Mshitakiwa, mnamo tarehe 9/8/2019, katika eneo lililopo ndani ya Wilaya ya Ubungo, Mkoa wa Dar es Salaam, ulikutwa ukimtumikisha mtoto aitwaye Kabala, kinyume na sheria. Mshitakiwa unashitakiwa kwa kosa la kumfanyisha mtoto kazi kinyume cha Sheria ya Haki ya Mtoto, Sheria Na. 2/2019.

**Hakimu:** (*Anamuuliza mwendesha mashitaka.*) "Umemaliza?"

**Mwendesha Mashitaka:** Ndiyo, Mheshimiwa!

**Hakimu** Mashitaka hayo ni ya kweli? (*Anamuuliza Ngineo kuhusu ukweli wa tuhuma hizo.*)

**Ngineo:** Ni ya kweli Mheshimiwa!

**Hakimu:** Je, mashitaka ni ya kweli? (*Anarudia kumuuliza Ngineo mara tatu.)*

**Ngineo:** (*Anakiri kosa mara zote tatu.*)

**Hakimu:** Una lolote la kujijitetea? (*Anamuuliza Ngineo.*)

**Ngineo:** Sikujua kama ni kosa Mheshimiwa Hakimu, mimi



KISWAHILI FINAL.indd 55 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

nilikuwa na uhitaji wa mtu wa kunisaidia kazi za nyumbani.

**Hakimu:** Una lolote la kusema? (*Mheshimiwa Hakimu anamuuliza Afande Bahati.*)

**Afande Bahati:** Mtuhumiwa ni mkosaji wa mara ya kwanza. Hata hivyo, anatakiwa apewe adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine.

**Hakimu:** Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha 78 cha Sheria ya Haki ya Mtoto ya Mwaka 2019, mahakama inakutia hatiani na inakuhukumu kifungo cha miezi mitatu jela au faini ya shilingi laki moja. Kosa hili umelikiri mwenyewe mahakamani. Rufaa iko wazi ndani ya siku 21 kuanzia leo kama hautaridhika na uamuzi wa mahakama.

**Polisi:** Kooo...rti (*Mahakama inaahirishwa. Ngineo anachukuliwa na askari na kuwekwa kwenye karandinga na anapelekwa gerezani tayari kwenda kutumikia kifungo chake.*)






KISWAHILI FINAL.indd 56
2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Maswali**

1. Pendekeza kichwa cha igizo.
2. Ni sifa gani za maigizo zinazodhihirika katika igizo ulilolisoma?
3. Bainisha wahusika waliojitokeza katika igizo hilo.
4. Eleza tabia ambayo Ngineo alikuwa anaionesha kwa mfanyakazi wake.
5. Ni funzo gani ulilolipata kutokana na igizo ulilolisoma?

**Zingatia**

Maigizo ni michezo inayoigizwa jukwaani. Michezo hiyo huweza kuandikwa na kuigizwa jukwaani na wahusika kwa lengo la kuburudisha na kuelimisha jamii kuhusu jambo fulani. Katika fasihi simulizi, uigizaji hufanyika kwa kuhusisha maneno yanayoambatana na matendo ya wahusika kuhusu matukio mbalimbali ya kijamii.

Utunzi wa maigizo ni kitendo cha kubuni wahusika na kuwapa matendo na maelezo watakayoyatenda jukwaani baada ya kuchagua mada. Maigizo hutungwa kwa kuzingatia taratibu ambazo humwongoza mtunzi wa maigizo kufanya kazi yake kwa ufanisi na kuvutia hadhira. Taratibu hizo ni: Kwanza, kuchagua wazo ambalo litamwongoza kutunga igizo lake. Pili, kuchagua mandhari ambapo matukio yote ya igizo yatatendeka. Mandhari hiyo huweza kuwa ya kubuni kama vile peponi au mazingira halisi kama vile ofisini, baharini, msituni, shuleni, au barabarani.

Tatu, kuamua kuhusu mtindo atakaoutumia kuwasilisha ujumbe anaokusudia kuifikishia hadhira yake. Anaweza kutumia mafumbo, vichekesho, na nyimbo. Pia, anaweza kucheza ngoma au kutumia mbinu nyingine ili kuongeza mvuto katika kazi yake.

Nne, kuzingatia mpangilio wa visa na matukio ili kuzua migogoro ambayo huibua dhamira zinazokusudiwa. Suluhisho la mgogoro hupatikana pale igizo linapofikia kilele. Kwa mfano, mwishoni mwa igizo, mtuhumiwa anaweza kufungwa au kuachiwa huru asipopatikana na hatia.

Tano, kupangilia vizuri maonesho ya igizo ili kukamilisha dhamira iliyokusudiwa kuwasilishwa. Maonesho hujumuisha vitendo na hoja zinazokamilisha sehemu zinazobeba maudhui ya aina moja. Sehemu kadhaa hujenga tukio au kitendo ambacho hubeba jambo mojawapo muhimu. Mtunzi anatakiwa kutunga kauli au vitendo vinavyoambatana na igizo hilo katika kila onesho.

Sita, kubuni wahusika watakaobeba ujumbe anaouwasilisha. Mtunzi hana budi kutumia wahusika wanaotofautiana kiumri na kiumbo kama vile, watoto,

Fot online use only
do not duplicate

wazee, vijana, wanaume, wanawake, wanene, wembamba, warefu, na wafupi. Wahusika hao huwa na tabia tofauti. Kuna wahusika kama wezi, walevi, wavivu, wachapakazi, wema, wanaofichua maovu katika jamii, au wabaya ambao wanatenda maovu katika jamii kulingana na maudhui yanayokusudiwa kuwasilishwa. Mtunzi atachagua idadi ya wahusika pamoja na maleba kulingana na matukio aliyonayo katika igizo lake.

Saba, kuamua kuhusu urefu wa igizo. Urefu au ufupi wa igizo hutegemea tukio linalokusudiwa kutungiwa igizo. Ikiwa tukio ni fupi, igizo litakalotungwa sharti liwe fupi, na kama tukio ni refu igizo nalo linapaswa kuwa refu.

Nane, kuchagua lugha itakayotumika. Ni sharti atumie lugha ya kisanaa inayovutia na kuleta taharuki. Pia, mtunzi anashauriwa kutumia vihisishi ili kuleta vionjo halisi vitakavyogusa hisia za watazamaji. Aidha, mtunzi anashauriwa kuchunguza lugha aliyoitumia katika igizo ili kuhakikisha kuwa haina makosa na ni mwafaka.

**Zoezi la 5.3**

1. Bainisha mambo yafuatayo katokana na igizo la utumikishwaji wa watoto ulilolisoma:
   (a) Wazo kuu linalopatikana katika igizo;
   (b) Wahusika wote waliojitokeza katika igizo;
   (c) Muktadha wa igizo; na
   (d) Matendo ya wahusika wa igizo.
2. Umejifunza nini kupitia igizo ulilolisoma?

FOR ONLINE USE ONLY

**Kazi ya 5.9**



1. Eleza mambo ya kuzingatia katika utunzi wa maigizo.
2. Tunga igizo fupi kuhusu athari za rushwa katika jamii, kisha igiza na wenzako darasani.
3. Tengeneza maleba na vifaa mbalimbali vinavyotumika katika maigizo na uviwasilishe darasani.



KISWAHILI FINAL.indd 58 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

## Zoezi la marudio la 5

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

(i) Mshororo wa mwisho ambao haubadiliki katika beti zote za utenzi huitwa ........................

(a) mshororo takriri

(b) bahari

(c) kituo bahari

(d) kitulizo

(e) kituo

(ii) Neno lipi kati ya haya yafuatayo halihusiani na ushairi?

(a) Mshororo

(b) Kipande

(c) Bahari

(d) Dayalojia

(e) Muwala

(iii) Utungo wa kishairi unaoeleza kwa urefu kuhusu matukio ya kihistoria huitwaje?

FOR ONLINE USE ONLY

(a) Wimbo

(b) Shairi

(c) Ngonjera

(d) Majigambo

(e) Utenzi

(iv) Ipi kati ya zifuatazo si sifa ya ngonjera?

(a) Huwa na vina, mizani, na urari

(b) Huwa na mhusika mmoja

(c) Huwa na malumbano

(d) Hutambwa mbele ya hadhira

(e) Hupatikana katika maigizo na ushairi

Fot online use only
do not duplicate

(v) Kipi kati ya vifuatavyo si kipengele kinachopaswa kuzingatiwa wakati wa kutunga igizo?

(a) Uteuzi wa lengo

(b) Uteuzi wa muundo

(c) Uteuzi wa mandhari

(d) Uteuzi wa mizani

(e) Uteuzi wa wahusika

2. Oanisha maelezo yaliyopo fungu A na dhana zilizopo fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi ili yaweze kuleta maana.

| Fungu A | | Fungu B | |
|---|---|---|---|
| (i) | Utungo wenye mpangilio maalumu wa maneno wenye lugha ya picha au ishara | A. | shairi |
| (ii) | Sehemu ya mshororo katika shairi | B. | mtindo |
| (iii) | Mshororo wa mwisho katika ubeti wa shairi | C. | kituo |
| (iv) | Mjengo, mpangilio, au sura ya shairi | D. | kipande |
| (v) | Hayazingatii urari wa vina na mizani wala idadi sawa ya mishororo katika ubeti | E. | mashairi ya kisasa |
| | | F. | muundo |
| | | G. | mashairi ya kimapokeo |

FOR ONLINE USE ONLY

3. Kwa ufupi, eleza kanuni za utungaji wa mashairi.

4. Kuna tofauti gani kati ya mashairi na ngonjera?

5. Kwa ufupi, bainisha kanuni za kutunga mashairi, maigizo, tenzi, na ngonjera.

6. Eleza maana za maneno yafuatayo:

| | |
|---|---|
| (a) vina | (h) mtindo |
| (b) mizani | (i) muundo |
| (c) ubeti | (j) mshororo |
| (d) kituo bahari | (k) mgogoro |
| (e) muwala | (l) ujumbe |
| (f) mandhari | (m) falsafa |
| (g) wahusika | (n) dhamira |



KISWAHILI FINAL.indd 60
2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

# Sura ya Sita

## Uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi

### Utangulizi

*Kitu chochote kisipotunzwa, huweza kupotea na kusahaulika. Fasihi simulizi inapaswa kuhifadhiwa ili iweze kutumika kwa vizazi vilivyopo na vijavyo. Katika sura hii, utajifunza njia za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi pamoja na kueleza ubora na udhaifu wa kila njia. Pia, utajifunza umuhimu wa kuhifadhi kazi za fasihi katika jamii zetu. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuhifadhi kazi mbalimbali za fasihi simulizi na kutathmini njia utakazoamua kutumia katika kuhifadhi kazi hizo.*

### Kazi ya 6.1

**Chunguza picha zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.**










Fot online use only
do not duplicate

**Maswali**

1. Bainisha vitu vilivyopo katika picha ulizozichunguza.
2. Eleza matumizi ya kila kitu ulichokibainisha katika swali la kwanza.
3. Watu waliomo katika picha hiyo wanafanya nini?

**Zingatia**

Kuhifadhi kazi za fasihi simulizi ni kitendo cha kuzitunza kazi hizo kwa matumizi ya vizazi vilivyopo na vijavyo. Lengo lake ni kuifanya fasihi simulizi iendelee kuwapo na irithishwe kwa vizazi na vizazi kwa matumizi ya baadaye. Fasihi simulizi huhifadhiwa kwa njia mbalimbali.

Kwanza, fasihi simulizi huweza kuhifadhiwa *kichwani*. Njia hii imekuwa ikitumiwa kuhifadhi kazi za fasihi simulizi tangu kale na inaendelea kutumika hadi leo. Kwa kutumia njia hii, kazi ya fasihi simulizi huhifadhiwa akilini mwa fanani na huweza kuwasilishwa pale fanani anapoamua kufanya hivyo.

Pili, fasihi simulizi huweza kuhifadhiwa kwa *maandishi*. Njia hii ilianza kutumika baada ya binadamu kuvumbua maandishi. Uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi kwa njia hii hupitia hatua kubwa mbili. Hatua ya kwanza ni kubuni kisa au wazo; na hatua ya pili ni kuliweka wazo hilo katika maandishi. Kazi za fasihi simulizi zinazoweza kuhifadhiwa katika maandishi ni kama vile hadithi, nyimbo, mashairi, ngonjera, na majigambo.

Tatu, *vinasasauti* huweza kutumika kuhifadhia fasihi simulizi. Vinasasauti ni vifaa maalumu vinavyotumika kuhifadhi kazi za fasihi simulizi kwa kunakili au kurekodi sauti ya fanani. Njia hii hutunza sauti peke yake bila vitendo vya fanani. Miongoni mwa aina za vinasasauti ni tepurekoda na audiorekoda. Aina hizi hutofautishwa na teknolojia inayotumika kunasa sauti. Tepurekoda hutumia kifaa kinachotumia mkanda au utepe maalumu kunasa sauti, ilihali audiorekoda hufanya kazi hiyohiyo, bali kwa kutumia mfumo wa kidijiti. Njia hii ni ya kisasa zaidi kuliko ile ya maandishi.

Nne, fasihi simulizi huweza kuhifadhiwa katika *kanda* na *diski za video*. Njia hii huhusisha kanda zenye uwezo wa kunakili au kurekodi sauti pamoja na picha za vitendo vya fanani. Hivyo, matendo na sauti ya fanani wa kazi ya fasihi simulizi huonekana kwenye video.

Tano, fasihi simulizi huweza kuhifadhiwa katika *kompyuta*. Sauti zilizorekodiwa kwa tepurekoda au audiorekoda zinaweza kuhamishwa na kuwekwa katika kompyuta. Kadhalika, kompyuta huhifadhi picha jongezi ziambatanazo na matendo ya fanani na hadhira, yaani video. Njia hii imeanza kutumika baada ya watu kuwa wajuzi wa kutumia kompyuta.



KISWAHILI FINAL.indd 62 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Zoezi la 6.1**

1. Bainisha njia tatu zinazotumika katika uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi, kisha eleza namna zinavyotumiwa.
2. Eleza faida za kuhifadhi fasihi simulizi kwa njia ya vinasasauti.

**Kazi ya 6.2**

1. Kusanya nyimbo na mashairi mbalimbali, kisha tumia njia yoyote unayoipenda kuzihifadhi kazi hizo.
2. Eleza kwa nini umeamua kutumia njia hiyo badala ya zingine.

**Zingatia**

Njia zinazotumika katika uhifadhi wa fasihi simulizi zina ubora na udhaifu. Kwa upande wa ubora, fasihi simulizi inapohifadhiwa kichwani, huwa mali ya jamii nzima. Uwasilishaji wake huweza kufanyika wakati wowote bila maandalizi wala gharama yoyote. Pia, fasihi simulizi ikihifadhiwa kichwani, huwa hai kwa kuwa fanani huwasiliana ana kwa ana na hadhira yake; na uwasilishaji wake huhusisha vitendo na mbinu tofauti za kisanaa kama vile kucheza, kubadili sauti, na miondoko. Kwa upande wa udhaifu, kazi ya fasihi simulizi inapohifadhiwa kichwani, ni rahisi kubadilika. Hii hutokea kwa kuwa fanani anaweza kubadilisha maudhui, mpangilio, au mbinu za uwasilishaji. Pia, kuna uwezekano mkubwa wa kazi kupotea iwapo fanani atapoteza kumbukumbu au kufariki kwani kazi anayokuwa ameihifadhi kichwani nayo hupotea.

Fasihi simulizi ikihifadhiwa katika maandishi, haibadiliki; huweza kudumu kwa muda mrefu. Zaidi, huweza kuifikia hadhira hata iliyoko mbali na fanani; na haipotezi fani na maudhui yake kwa urahisi, bali hudumu hadi fanani atakapoamua kuibadilisha. Changamoto za kuhifadhi fasihi simulizi kimaandishi ni pamoja na kuwa mali ya aliyeihifadhi; kuhitaji ujuzi wa kusoma na kuandika; pamoja na kuwa na gharama za uhifadhi, kwani fanani anahitaji vifaa vya kuandikia kama vile kalamu, karatasi, penseli, meza, na kompyuta. Pia, uwasilishaji wake si hai kwa sababu fanani na hadhira hawaonani ana kwa ana, na kazi huweza kuchuja kutokana na fanani na hadhira kutoonana ana kwa ana.

Fasihi simulizi ikihifadhiwa kwa njia ya vinasasauti, huweza kuwafikia watu hata walio mbali na mtunzi kwa haraka na kwa urahisi. Pia, ubora wa kazi hiyo haupotei wala kuharibika endapo vifaa vitatunzwa vizuri; vionjo vya msanii husikika kwa kuwa sauti husikika moja kwa moja kutoka kwenye kifaa husika; na kazi ya msanii haibadiliki, bali hubaki katika uhalisia wake. Changamoto ya



KISWAHILI FINAL.indd 63 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi kwa njia hii ni kwamba, ni ghali kwa sababu huhusisha vinasasauti. Pia, uwasilishaji wake si hai kwa sababu hadhira husikia sauti ya fanani, lakini wahusika na matendo yanayofanyika hayaonekani; na kazi huwa mali ya aliyeihifadhi. Aidha, kazi haibadiliki kulingana na mazingira na wakati.

Uhifadhi wa fasihi simulizi katika kompyuta ni njia ya uhakika kwa vile kazi za fasihi simulizi zinazohusika huhifadhiwa vizuri na hutolewa pale zinapohitajika. Uhifadhi wa kazi kwa kompyuta humwezesha fanani kuwasilisha kazi yake kwa watu wengi kwa kutumia mitandao ya kijamii. Pia, kompyuta huhifadhi kiasi kikubwa cha kazi za fasihi simulizi kwa wakati mmoja. Hata hivyo, uhifadhi kwa njia hii una changamoto zifuatazo: njia hii haiwezi kutumika bila umeme, ni njia ya gharama. Huhitaji ujuzi wa kuitumia kwani watu wasiokuwa na ujuzi wa kompyuta hawawezi kuitumia. Aidha, kompyuta ikishambuliwa na virusi, kazi iliyohifadhiwa huweza kupotea.

Uhifadhi wa fasihi simulizi katika kanda na diski za video husaidia kuonekana kwa fanani na vifaa anavyovitumia. Aidha, sauti na milio ya ala wanazotumia husikika kwa hadhira. Vilevile, njia hii huipa uhai kazi ya fasihi simulizi kwa kuwa hadhira huona matendo yanayofanywa na fanani. Kadhalika, kazi ya fasihi simulizi hudumu kwa muda mrefu endapo kanda na diski za video zilizotumika kuhifadhia kazi hiyo zitatunzwa vizuri. Udhaifu wa njia hii ni gharama, kwani fanani hulazimika kununua kanda na diski za video pamoja na kumlipa mpiga picha. Pia, kazi ikisharekodiwa, huuzwa kwa bei kubwa. Vilevile, uhifadhi wa kazi ya fasihi kwa njia hii hunufaisha watu wachache ambao wana uwezo wa kumiliki video. Aidha, ingawa hadhira inaweza kumwona fanani, haiwezi kuwasiliana ana kwa ana na fanani.

**Zoezi la 6.2**

1. Pendekeza njia nyingine zinazoweza kutumiwa kuhifadhi kazi za fasihi simulizi.
2. Eleza ubora na udhaifu wa njia ulizozipendekeza.
3. Kwa nini ni muhimu kuhifadhi kazi za fasihi simulizi?
4. Ni kwa namna gani kazi za fasihi simulizi zikihifadhiwa kwa njia ya maandishi hupoteza ubora wake?

**Zingatia**

Uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi una umuhimu katika ukuzaji na uendelezaji wa utamaduni katika jamii. Kazi za fasihi simulizi ni vielelezo vya utamaduni



KISWAHILI FINAL.indd 64 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

wetu wa asili. Hivyo, zikihifadhiwa, utamaduni unakuwa umehifadhiwa pia. Vilevile, kazi zilizohifadhiwa zinaweza kuwa vivutio vya utalii wa utamaduni. Fasihi simulizi huelimisha, huburudisha, na hurithisha maarifa na maadili. Hivyo, ni muhimu kuzihifadhi kazi hizi ili zisiharibike au kupotea kwa madhumuni ya kutumika baadaye. Lengo kuu ni kutunza amali za jamii na kuzifanya ziendelee kutumika kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Fasihi simulizi pia hutumika kama sehemu ya ajira. Kwa mfano, shughuli mbalimbali za kisanaa kama vile ngoma na maigizo huwapatia wasanii vipato. Aidha, ni kichocheo cha umoja na maelewano miongoni mwa wanajamii kwa kuwa zinawaleta watu pamoja. Kwa mfano, baadhi ya makabila yenye desturi ya kutaniana huweza kutatua migogoro yao kwa kutumia utani kupitia kazi za fasihi simulizi. Hivyo, kazi za fasihi simulizi ni muhimu zihifadhiwe ili kuendeleza desturi.

## Zoezi la marudio la 6

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

   (i) Upi ni ubora wa njia ya kuhifadhi kazi ya fasihi simulizi kwa kichwa?

   (a) Ni kongwe

   (b) Ina uhai

   (c) Ina gharama

   (d) Hukutana chini ya mti

   (e) Ni rahisi kubadilika

FOR ONLINE USE ONLY

   (ii) Njia za kisasa za uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi zina changamoto gani?

   (a) Zina gharama na hazipatikani

   (b) Hufanya kazi za fasihi simulizi zipotee

   (c) Hupoteza uhalisia wake wa awali kama vile utendekaji wa matukio

   (d) Fanani na hadhira hawakutani ana kwa ana

   (e) Hudumu kwa muda mrefu

   (iii) Maandishi kama njia mojawapo ya uhifadhi wa fasihi simulizi yana faida gani ya msingi?

   (a) Huvutia msomaji

   (b) Hudumu kwa muda mrefu

   (c) Hupunguza uwezo wa hadhira kufikiri

Fot online use only
do not duplicate

(d) Hutumiwa na watu wote

(e) Hubadilika kulingana na wakati

(iv) Njia ipi ya kisasa ya uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi inatumika zaidi?

(a) Maandishi

(b) Kichwa

(c) Redio

(d) Vinasasauti

(e) Video

(v) Ipi ni sentensi sahihi zaidi kuhusu tofauti kati ya tepurekoda na audiorekoda?

(a) Tepurekoda hutumika zaidi vijijini, wakati audiorekoda hutumika zaidi mijini.

(b) Tepurekoda hutumia kanda, wakati audiorekoda hutumia mfumo wa kidijiti.

(c) Tepurekoda hutunza sauti bila vitendo, wakati audiorekoda hutunza sauti na vitendo.

(d) Tepurekoda inaharibika haraka, wakati audiorekoda huchelewa kuharibika.

(e) Tepurekoda haiwezi kubebwa nje ya mahali ilipotumika, wakati audiorekoda inaweza kubebwa popote.

FOR ONLINE USE ONLY

2. Bainisha namna jamii yako inavyokuza na kuendeleza kazi za fasihi simulizi kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

3. Eleza njia zinazotumika katika jamii yako kuhifadhi kazi za fasihi simulizi.

4. Fafanua changamoto zinazoweza kujitokeza katika kuhifadhi kazi za fasihi simulizi kwa njia mbalimbali.

5. Ni kwa namna gani uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi hutegemea mazingira na uwezo wa kiuchumi?



KISWAHILI FINAL.indd 66 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

# Sura ya Saba

## Uandishi

**Utangulizi**

*Mawasiliano hufanyika kwa njia mbalimbali. Miongoni mwazo ni mazungumzo, maandishi, na ishara. Katika sura hii, utajifunza kuwasiliana kimaandishi. Hususani, utajifunza kuandika insha za hoja, barua rasmi, ujumbe wa simu ya mkononi, baruapepe, kadi za mialiko, na dayalojia. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kukuza stadi ya kuandika na kuwasiliana katika miktadha mbalimbali kwa njia ya maandishi.*

### Insha za hoja

**Kazi ya 7.1**

**Soma insha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

FOR ONLINE USE ONLY

Elimu ni maarifa au ujuzi aupatao mtu ili kukabiliana na mazingira yake. Maarifa au ujuzi huweza kupatikana shuleni, nyumbani, na katika jamii inayomzunguka.

Elimu ni muhimu katika jamii yoyote ile kwa sababu humwezesha binadamu kuishi kulingana na mazingira yake. Lengo kuu la elimu ni kuhakikisha binadamu anapata maendeleo endelevu katika maisha yake. Kutokana na elimu, binadamu anaweza kujiajiri au kuajiriwa na kujipatia kipato cha kuendeshea maisha yake. Aidha, elimu husaidia kujenga taifa imara. Taifa linapowekeza katika elimu bora kwa wananchi, huimarisha na kujenga kizazi cha sasa na cha baadaye. Ni muhimu kuwekeza katika elimu itakayowajengea wananchi ujuzi na maarifa ili waweze kujikwamua kutoka katika umaskini na kulijenga taifa lao.

Elimu ni muhimu katika jamii yoyote kwa sababu husaidia kutatua matatizo yaliyopo katika jamii hiyo. Kila mtu huishi maisha ya aina fulani, ambapo ujuzi alionao humsaidia kutatua matatizo yanayomkabili na yanayoikabili jamii yake. Kwa mfano, elimu ya mazingira huwasaidia wanajamii kutunza

Fot online use only
do not duplicate

mazingira. Elimu ya afya husaidia jamii kukabiliana na tatizo la maradhi ili kuzifanya afya zao kuwa imara muda wote na kuwawezesha kufanya kazi kwa ajili ya ujenzi wa taifa.

Vilevile, elimu huipatia jamii maarifa ya kufikiri kitunduizi ambayo huiwezesha kufanya uamuzi sahihi wa kimaisha. Kutokana na ujuzi wa kufikiri kwa kina, jamii inaweza kugundua na kuvumbua vitu mbalimbali. Kwa mfano, maendeleo ya sayansi na teknolojia yatokanayo na maarifa na ujuzi unaopatikana kutokana na elimu yamesaidia kugunduliwa na kuvumbuliwa kwa vifaa vya kisasa. Baadhi ya vifaa hivyo ni zana za kilimo, mashine, ndege, kompyuta, zana za kivita, simu za mikononi, treni za umeme, magari, na vifaatiba.

Zaidi ya hayo, elimu, hususani inayotolewa katika mfumo rasmi kama shuleni na vyuoni, husaidia kutambua thamani ya muda. Muda, kama rasilimali, ni muhimu sana katika maendeleo ya binadamu. Kwa kuwa muda ni mali, watu wenye elimu hutumia muda wao vizuri kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii ili kuongeza uzalishaji mali kwa lengo la kukuza uchumi wao na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Elimu husaidia kujenga tabia njema; hivyo, husaidia kujua mema na mabaya. Elimu huwafanya raia kuwa watu wema na wenye maadili. Watu wenye elimu hukemea matendo maovu katika jamii. Kwa mfano, wasomi wengi hukemea mila potofu kama ukeketaji na vitendo viovu kama wizi.

Hali kadhalika, elimu huchochea haki na usawa katika jamii. Haki ni kitu au huduma ambayo binadamu anastahili kuipata kutoka kwa wengine au mamlaka husika kwa mujibu wa sheria. Jamii ya watu waliopata mwanga wa kielimu hudai haki zao pamoja na usawa. Kwa mfano, wanawake wasomi ndio walio mstari wa mbele katika kudai haki na usawa wa kijinsia kuanzia ngazi ya familia mpaka kwenye vyombo vya kufanya uamuzi.

Elimu ni muhimu kwa sababu ndiyo urithi pekee kwa mwanadamu ambao hauharibiki. Urithi wa mali huisha, lakini urithi wa elimu hudumu. Hivyo, ni vizuri kurithishwa elimu kuliko kurithishwa mali.

Mbali na yote yaliyokwishaelezwa, elimu huwafanya watu wajiamini. Kujiamini ni kitendo cha kuwa na imani ya kuweza kufanya jambo fulani. Watu wenye elimu hujiamini katika kufanya mambo mbalimbali. Kujiamini huko huwawezesha kuhoji masuala mbalimbali ili kupata majibu, ikiwa ni pamoja na kudai haki zao pale zinapokiukwa.

Kwa hiyo, jamii haina budi kuwekeza katika elimu kwa kuwa husaidia



KISWAHILI FINAL.indd 68 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

watu katika nyanja mbalimbali za maisha. Kwa sababu hiyo, elimu inaweza kuchukuliwa kuwa mwanga na ufunguo wa maisha. Kwa kuzingatia hili, elimu inayotolewa lazima iwe ya kujenga fikra za ubunifu na ugunduzi wa kiteknolojia utakaoleta maendeleo endelevu na kuwawezesha vijana na taifa kwa ujumla kushindana katika soko la ajira. Kwa kufanya hivyo, elimu itasaidia kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika maisha ya kila siku.

**Maswali**

1. Pendekeza kichwa cha insha uliyoisoma.
2. Ni mafunzo gani umeyapata kutokana na insha uliyoisoma?
3. Ni hoja gani zimejengwa na mwandishi wa insha hii?
4. Onesha utetezi wa hoja za mwandishi wa insha hii kwa kutoa mifano.

**Zingatia**

Insha za hoja huandikwa ili kutoa mawazo, maoni, au hoja kuhusu jambo au suala fulani. Mathalani, hoja hizo zinaweza kuwa umuhimu wa elimu, umuhimu wa misitu, faida za kuhifadhi mazingira, au uhuru wa biashara. Insha hizi huelezea au hudadisi jambo kwa kutoa hoja kadhaa. Hoja hizo zinaweza kuwa za kukubali au kupinga jambo hilo. Hivyo, insha za hoja hutetea au kupinga mawazo ya aina fulani kwa kutoa uthibitisho ulio dhahiri. Pia, hutumia lugha iliyo fasaha inayoepuka matumizi makubwa ya semi na tamathali za semi.

Unapoandika insha ya hoja, kuna mambo muhimu ya kuzingatia ili insha iwe bora na yenye mtiririko mzuri. Jambo la kwanza ni kichwa cha insha. Hii ni mada ya insha ambayo hueleza kwa muhtasari kuhusu insha. Mada ya insha huandikwa kwa herufi kubwa juu ya insha sehemu ya katikati. Pia, hupigiwa mstari, hasa katika uandishi wa mkono. Aghalabu, huandikwa kwa wino uliokozwa katika uandishi wa kuchapa. Jambo la pili ni mwanzo wa insha. Huu ni utangulizi ambao hufasili au hueleza kwa kifupi jambo litakaloandikwa na huandikwa katika aya moja. Jambo la tatu ni kiini ambacho hubeba mawazo yote ya mwandishi na huandikwa katika mtiririko wa aya.

Jambo la nne ni sehemu ya mwisho. Hii ni sehemu ambayo mwandishi huhitimisha mawazo yake aliyolenga kuyaeleza. Hitimisho hutoa muhtasari wa yale yaliyojadiliwa katika insha. Katika sehemu hii, mwandishi huweza kutoa maoni na mapendekezo yake kuhusu jambo alililoliandikia. Hivyo, mwandishi hana budi kuandika muhtasari wenye mvuto kwa msomaji wake. Aidha,



KISWAHILI FINAL.indd 69 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

mwandishi anatakiwa adokeze msimamo wake katika sehemu hii. Mambo yote haya huwekwa chini ya kipengele kimoja kiitwacho muundo wa insha.

**Kazi ya 7.2**

Andika insha ya hoja yenye maneno 250 kuhusu mada unayoipenda.

## Zingatia

Katika uandishi wa insha za hoja, mbali na mambo yanayohusu muundo wa insha, kuna mambo mengine ya kuzingatia. Kabla ya kuandika insha, mwandishi hana budi kupangilia mawazo yake kimantiki ili kuwa na mtiririko mzuri wa maudhui kuanzia mwanzo hadi mwisho wa insha na kuepuka kumkanganya msomaji wake. Vilevile, mwandishi anatakiwa atoe hoja zenye mashiko, uzito, na ushawishi. Hoja zinazoandikiwa ni vyema ziambatane na mifano mbalimbali ya kuzishadidia zaidi. Pia, mwandishi anapaswa kuzingatia taratibu za uandishi kama vile matumizi ya herufi kubwa na ndogo na uwekaji wa alama za uandishi pale panapostahili ili kurahisisha usomekaji. Anapaswa pia kupanga hoja zake kwa mtiririko mzuri ili kumwezesha msomaji kuelewa kile alichokusudia. Aidha, mwandishi anapaswa aeleze kwa uwazi na kwa kina mambo ya msingi kuhusu suala analolijadili. Maelezo yake yanapaswa yalete mvuto utakaomshawishi msomaji kuendelea kusoma insha. Mambo ya msingi kuhusu suala linalojadiliwa ni pamoja na fasili, sababu, faida, umuhimu, hasara, au mapendekezo kulingana na mada inayohusika.

Hali kadhalika, mwandishi wa insha hana budi kupanga mawazo yake katika aya kwa kuzingatia mtiririko wa maudhui unaojengana kuanzia mwanzo hadi mwisho wa insha yake. Kila aya inatakiwa ibebe wazo kuu moja tu. Vilevile, mwandishi anapaswa kuzingatia uteuzi mzuri wa maneno ambayo yanaeleweka na yanalenga kumshawishi msomaji wake. Maneno hayo lazima yaendane na mada inayozungumziwa. Lugha isiyo fasaha isitumike katika uandishi wa insha za hoja. Aidha, mwandishi anatakiwa kuepuka matumizi ya vifupisho katika uandishi wa insha yake; badala yake, aandike maneno yake kwa kirefu. Kwa mfano, badala ya kutumia *n.k.*, atumie *na kadhalika*; badala ya *k.m.*, atumie *kwa mfano*; na badala ya *k.v.*, atumie *kama vile*. Sababu ya kuepuka vifupisho ni kuepuka uwezekano wa kuwa na tafsiri tofauti miongoni mwa wasomaji. Pamoja na hayo, mwandishi anatakiwa aoneshe msimamo wake dhahiri katika ujenzi wa hoja zake. Kulitekeleza hili, anapaswa atoe hoja madhubuti zinazoshadidiwa kwa mifano dhahiri yenye mashiko kwa kile anachokitetea.



KISWAHILI FINAL.indd 70 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Zoezi la 7.1**

1. Unaelewa nini kuhusu insha za hoja?
2. Ni wakati gani insha za hoja huandikwa?
3. Eleza mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha za hoja.
4. Fafanua kwa kifupi muundo wa insha za hoja.

## Barua rasmi

**Kazi ya 7.3**

**Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**



**Maswali**

1. Wanafunzi hao wanafanya nini?
2. Ainisha vifaa vinavyotumiwa na wanafunzi hao kufanya jambo ulilolibaini katika swali la kwanza.
3. Bainisha matumizi ya kila kifaa ulichokitaja.



KISWAHILI FINAL.indd 71 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

## Zingatia

Katika uandishi wa barua, kuna barua zinazohusu mambo ya kiofisi kama vile kuomba kazi, kuomba nafasi za masomo, mkopo, kumwalika kiongozi, kutoa taarifa ya kushindwa kuhudhuria mikutano, na kuagiza vifaa vya shughuli mbalimbali.

Barua hizo huandikwa kwa ufupi kwa kuzingatia lugha fasaha na sentensi zenye maana kamili ili kuepuka maelezo yasiyo sahihi. Vilevile, huzingatia alama za uandishi na huandikwa waziwazi juu ya jambo lililokusudiwa.

Barua hizo huwa na muundo maalumu ambao huzitofautisha na barua za kirafiki. Barua hizo huundwa na vipengele kumi na kimoja ambavyo ni: anwani ya mwandishi, tarehe, namba ya kumbukumbu, anwani ya mwandikiwa, mwanzo wa barua, kichwa cha barua, kiini cha barua (barua yenyewe), mwisho wa barua, saini, jina la mwandishi, na cheo cha mwandishi.

Anwani ya mwandishi huandikwa juu kwenye pembe ya upande wa kulia wa karatasi. Anwani ya mwandishi hujumuisha jina la eneo analoishi, namba ya sanduku la posta pamoja na jina la mahali posta ilipo. Anwani hii inatakiwa iandikwe kwa ukamilifu na kwa usahihi ili kuonesha barua imetoka kwa nani.

Pia, barua huwa na tarehe. Tarehe huandikwa upande wa kulia wa karatasi chini ya anwani ya mwandishi. Kuna namna nyingi za kuandika tarehe, kwa mfano, 1-2-2020, 1/2/2020, 1.2.2020, na 1 Februari 2020. Tarehe huandikwa ili kuonesha barua hiyo iliandikwa lini. Pia, humsaidia mwandikiwa kujua kama barua imemfikia kwa wakati.

Namba ya kumbukumbu ni kitambulisho cha barua. Namba hii hutumika ikiwa barua husika ni mwendelezo wa barua zilizopita na zitakazoandikwa baadaye kuhusu mada ileile na kwa mwandikiwa yuleyule. Hivyo, ikiwa barua inayoandikwa haina mwendelezo huo, namba ya kumbukumbu siyo ya lazima. Namba ya kumbukumbu huhusisha jina la mwandishi, jina la mwandikiwa, maudhui ya barua, na tarehe. Pia, huonesha ni barua ya ngapi katika mwendelezo. Kwa mfano, TET/ WEST/VSM/10520/006. Namba hiyo inaonesha kwamba, mwandishi ni Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), inaandikwa kwa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (WEST), inahusu Vitabu vya Shule za Msingi (VSM), imeandikwa Tarehe kumi mwezi Mei mwaka 2020 (10520) na ni barua ya sita.(006).

Anwani ya mwandikiwa inahusisha jina, cheo cha mwandikiwa na jina la taasisi au kampuni, sanduku la posta, na mahali (wilaya, mkoa, manispaa, au jiji) posta ilipo. Huandikwa upande wa kushoto chini ya namba ya kumbukumbu. Nafasi ya mstari mmoja huachwa baina ya namba ya kumbukumbu na anwani ya mwandikiwa.

Mwanzo wa barua huandikwa chini ya anwani ya mwandikiwa. Huanza na neno *Ndugu*, ambalo huwa peke yake au huongezewa neno lingine la kutaja wadhifa



KISWAHILI FINAL.indd 72 2021/09/13 12:13

Fot online use only

au heshima ya cheo cha mwandikiwa, kwa mfano, *Mkuu wa Wilaya*. Kichwa cha barua ni mada ya barua. Kichwa cha barua sharti kiwe kifupi na kinachoeleweka. Inafaa kiandikwe kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari katika uandishi wa mkono au kiandikwe kwa wino uliokozwa katika uandishi wa kuchapa.

## Kazi ya 7.4

**Soma kwa makini barua rasmi zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Barua ya kwanza**

Skuli ya Sekondari Mweresi,
S.L.P. 320,
**Zanzibar**.

Kumb. Na. SSM/MM-KK/UJZ/25820/02 25/8/2020.

Meneja Mkuu,
Kampuni ya Kilinge,
S.L.P. 10,
**Zanzibar**.

Ndugu,

**YAH: KUAGIZA VIFAA VYA UJENZI**

FOR ONLINE USE ONLY

Tafadhali rejea kichwa cha barua hapo juu.

Ninaomba kuagiza vifaa kutoka katika kampuni yako kwa ajili ya kukarabati jengo la maabara ya shule. Vifaa vinavyohitajika ni:

Saruji mifuko 10

Misumari ya inchi 3 kilo 20

Mbao za kuezekea 20

Utakapofikisha vifaa hivyo shuleni, mchakato wa malipo utafanyika kwa kuzingatia taratibu za manunuzi ya umma.

Wako katika ujenzi wa taifa,



Ochola Vuai

Mkuu wa Skuli

Fot online use only
do not duplicate

**Barua ya pili**

Shule ya SekondariAzimio,
S.L.P. 41,
**Nansio**.
14/9//2020.

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe,
S.L.P. 29,
**Nansio**.

Ndugu,

**YAH: MAOMBI YA KAZI YA AFISA MTENDAJI WA KIJIJI**

Tafadhali husika na kichwa cha barua hapo juu.


Ninaomba nafasi ya kazi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji katika Halmashauri yako kama ulivyotangaza katika mbao za matangazo za Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya na katika gazeti la *Habari Leo* la tarehe 10/9/2020.

FOR ONLINE USE ONLY

Nimewahi kukaimu nafasi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Buhima kwa muda wa miezi sita. Hivyo, nina uzoefu wa kutosha pamoja na uwezo wa kufanya kazi hiyo.

Pamoja na barua hii, ninaambatisha wasifu wangu na nakala za vyeti vyangu.

Wako katika ujenzi wa taifa,



Amosi Jumapili

Mwombaji

**Maswali**

1. Barua mbili ulizozisoma zinahusu nini?
2. Kichwa cha barua kina umuhimu gani?
3. Neno “Ndugu” katika barua lina umuhimu gani?




KISWAHILI FINAL.indd 74 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

4. Eleza hatua utakazozitumia kuandika barua rasmi.
5. Kwa nini barua rasmi huwa na anwani mbili?
6. Kila barua uliyoisoma ilikuwa na lengo lipi?
7. Eleza umuhimu wa namba ya kumbukumbu katika barua.

**Kazi ya 7.5**

1. Jaza visanduku vifuatavyo kulingana na vipengele vinavyounda barua rasmi.



FOR ONLINE USE ONLY

2. Andika barua rasmi kwa msimamizi wa maktaba ya shule yako ukiomba kuazima vitabu vinavyohusu uandishi wa insha na barua rasmi.



KISWAHILI FINAL.indd 75 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Zoezi la 7.2**

1. Fafanua kwa ufupi maana ya barua rasmi.
2. Eleza mambo ya msingi yanayotakiwa katika barua rasmi.
3. Bainisha dhima mbalimbali za barua rasmi.

## Ujumbe mfupi wa simu ya mkononi

**Kazi ya 7.6**

**Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**




**Maswali**

1. Kifaa kilichoshikwa mikononi kinatumikaje katika mawasiliano?
2. Bainisha mambo yasiyopungua matatu ambayo yanadhihirika katika ujumbe unaoonekana kwenye kifaa kilichoshikwa mikononi.
3. Eleza dhima za ujumbe mfupi wa simu ya mkononi.



KISWAHILI FINAL.indd 76 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Zingatia**

Simu ya mkononi ni kifaa kinachobebeka na, kwa kawaida, hutumiwa kwa mawasiliano pale wanaowasiliana wanapokuwa hawaonani. Licha ya kutumika katika mawasiliano ya kuongea, simu ya mkononi hutumika pia katika mawasiliano ya kutuma na kupokea ujumbe mfupi wa maandishi. Ujumbe wa simu ya mkononi ni maandishi mafupi ambayo huonesha taarifa anayotakiwa kuipata mpokeaji. Lengo la kuandika ujumbe wa simu ya mkononi ni kuwasiliana kati ya mtumaji na mpokeaji wa ujumbe. Ili mtu aandike ujumbe wa simu, ni lazima awe na simu ya mkononi.

**Kazi ya 7.7**

1. Soma ujumbe unaoonekana kwenye picha ya kazi ya 7.6, kisha eleza ujumbe huo unahusu nini.
2. Jibu ujumbe huo. Jina lako liwe Mama Anita.

**Zingatia**

Ujumbe mfupi wa simu ya mkononi huandikwa kwa kuzingatia mambo kadhaa. Kwanza, lazima pawe na lengo la kuandika ujumbe. Kabla ya kuanza kuandika ujumbe, ni lazima pawe na jambo ambalo mwandishi anakusudia kumweleza mpokeaji wa ujumbe. Jambo hilo ndilo huchochea kuandikwa kwa ujumbe.

Pili, namba ya simu ya mpokeaji inapaswa iandikwe kwa usahihi. Kuandika namba ya simu kwa usahihi husaidia ujumbe kufika kwa mlengwa. Namba ya simu ikikosewa kuandikwa ujumbe huweza kwenda kwa mtu asiyehusika.

Tatu, ujumbe wa simu ya mkononi unatakiwa uandikwe kwa ufupi na kwa kuzingatia sheria zinazodhibiti mawasiliano nchini. Mathalani, hivi sasa, kuna Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015 inayomkataza mtumiaji wa simu kuandika au kusambaza taarifa ya uongo, uchochezi, au mambo yanayokiuka maadili ya Kitanzania.

Nne, mwandishi wa ujumbe anapaswa kuandika ujumbe kwa namna inayojitosheleza. Ujumbe unaojitosheleza humwezesha mpokeaji kuuelewa vizuri.

Tano, mwandishi wa ujumbe anatakiwa kumwelewa mpokeaji wa ujumbe huo ili aandike ujumbe mwafaka. Iwapo ujumbe unaoandikwa ni wa kiofisi, mwandishi anapaswa kufuata kanuni zote za uandishi. Kwa mfano, anapaswa kuepuka matumizi ya vifupisho visivyojulikana, matumizi holela ya herufi kubwa, na kuhakikisha kwamba anatumia viakifishi kwa usahihi. Ikiwa ujumbe unaoandikwa



KISWAHILI FINAL.indd 77 2021/09/13 12:13

Fot online use only

si wa kiofisi, mwandishi hafungwi na taratibu hizi, ilimradi ahakikishe kwamba ujumbe anaouandika utaeleweka vyema kwa mpokeaji.

Sita, mwandishi anapaswa kuhakiki usahihi wa maandishi yake kabla ya kutuma ujumbe. Hii itasaidia kuepuka kutuma ujumbe ulio na makosa. Ujumbe wenye makosa unaweza usieleweke vizuri kwa mpokeaji na, hivyo, kukwamisha mawasiliano. Saba, ujumbe wa simu ya mkononi unatakiwa uwe sahihi. Mwandishi anapaswa kuandika jambo kwa usahihi ili kuepuka upotoshaji.

**Kazi ya 7.8**

Jifanye wewe ni mwanafunzi wa bweni. Unataka kumpa taarifa mzazi wako kuwa unahitaji kununua kitabu cha Kiswahili cha Kidato cha Pili. Kwa kutumia simu ya mwalimu mlezi, andika ujumbe mfupi wa kuomba fedha kwa mzazi wako kwa ajili ya kununua kitabu.

**Zingatia**

Ujumbe mfupi wa simu ya mkononi hauna muundo maalumu. Kwa kiasi kikubwa, hutegemea mazingira na uhusiano wa wanaowasiliana. Ujumbe wa simu ya mkononi unaweza kujumuisha; salamu, taarifa iliyokusudiwa, na lengo la kuandika. Jambo lingine ni cheo cha mwandishi, ikiwa ujumbe ni wa kiofisi, au utambulisho wowote wa mwandishi. Tazama mifano ya ujumbe wa simu hapa chini.

FOR ONLINE USE ONLY

**Mfano wa 1**

Habari za mchana? Kesho nitasafiri kikazi kuelekea Mwanza. Ninaomba ufike ofisini leo ili nikukabidhi ofisi.

J. Kamalamo

**Mfano wa 2**

Shikamoo mama. Tutafunga shule tarehe 26.3.2020. Ninaomba unitumie nauli. Mwanao Furaha. Asante.

**Kazi ya 7.9**

**Chunguza ujumbe wa simu ufuatao, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Habari! uc4c 2fa8. Kila m2 ana maixha yake.

1. Umebaini nini katika ujumbe huo?
2. Andika ujumbe huo kwa kutumia lugha fasaha ya Kiswahili.



KISWAHILI FINAL.indd 78 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Zoezi la 7.3**

1. Onesha tofauti tano kati ya ujumbe wa simu ya mkononi na barua.
2. Andika ujumbe wa simu ya mkononi, kisha eleza muundo wake.

## Baruapepe

**Kazi ya 7.10**

**Soma baruapepe ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Wanafunzi waliosajiliwa Kidato cha Kwanza**

kode.kazoka@tie.go.tz

Wanafunzi waliosajiliwa Kidato cha Kwanza

Habari za kazi?
Ninaomba upokee orodha ya wanafunzi waliosajiliwa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Ruaha, Januari 2020 kama ulivyoagiza.

Kuona orodha ya majina ya wanafunzi naomba ufungue kiambatisho.

Ninaomba kuwasilisha.

Kole Kaminyoge
Mkuu wa shule

ORODHA YA WANAFUNZI WALIOSAJILIWA KIDA... ( 13 K)

Tuma

FOR ONLINE USE ONLY

Fot online use only
do not duplicate

**Maswali**

1. Bainisha kichwa cha baruapepe uliyoisoma.
2. Aliyeandika baruapepe uliyoisoma ana wadhifa gani?
3. Kwa nini orodha ya majina ya wanafunzi haijaonekana bayana kwenye baruapepe?

**Zingatia**

Baruapepe ni ujumbe unaotumwa kwa intaneti kupitia kompyuta, simu ya mkononi, au kifaa chohote kilichounganishwa kwenye mtandao wa intaneti. Uandishi wa baruapepe huzingatia lengo la kuandika baruapepe pamoja na usahihi wa anwani ya baruapepe ya mpokeaji ili kuepusha baruapepe kwenda kwa mtu asiyehusika; hivyo, kushindwa kufika kwa mlengwa. Kumwelewa mpokeaji wa ujumbe husaidia kuamua aina ya lugha utakayoitumia. Kuzingatia sheria za nchi, kwa mfano, Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015 inayomkataza mtumiaji wa mitandao kuandika au kusambaza taarifa za uongo na uchochezi, ni jambo jingine la kuzingatia wakati wa kuandika baruapepe. Mambo mengine ya kuzingatia ni matumizi ya lugha fasaha na ya heshima inayoendana na ujumbe wa baruapepe, usomekaji wa maandishi, na usahihi wa ujumbe unaoandikwa ili kuepuka uwezekano wa kupotosha ujumbe.

Vipengele muhimu katika uandishi wa baruapepe ni anwani ya baruapepe ya mwandishi na mwandikiwa na kichwa au mada ya baruapepe. Mada inapaswa kuwa mahususi na inayoelezea kwa usahihi kusudi litakalompa mpokeaji wa baruapepe sababu halisi ya kuifungua. Vipengele vingine ni salamu, kiini cha baruapepe, ambacho huhusu lengo la kuandika baruapepe, ujumbe wa kufunga ili kuhitimisha hoja, na utambulisho wa mwandishi. Kipengele cha utambulisho wa mwandishi huhusu jina au jina na cheo, cheo, na anwani.

Baruapepe hutumika kutoa taarifa juu ya jambo au tukio fulani. Jambo hilo linaweza kuwa malalamiko, kifo, ugonjwa, kufaulu mitihani, kupata kazi, kujiunga na shule, kusafiri, kuomba mahitaji fulani kutoka kwa watu wengine au kujuliana hali baina ya watu.

**Kazi ya 7.11**

Chunguza mfano wa baruapepe uliyopewa katika kazi ya 7.10, kisha bainisha mambo muhimu utakayoyazingatia katika kuandika baruapepe kwa mkuu wako wa shule kumtaarifu kuwa hutaweza kufika shuleni siku ya kufungua shule kwa kuwa hukufanikiwa kupata usafiri.



KISWAHILI FINAL.indd 80 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Zoezi la 7.4**

1. Fafanua mambo ya kuzingatia wakati wa kuandika baruapepe.
2. Eleza muundo wa baruapepe.
3. Baruapepe zina dhima gani katika mawasiliano?

## Kadi za mialiko

**Kazi ya 7.12**

**Chunguza kadi ya mwaliko ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**



MWALIKO WA SHEREHE YA KUMBUKUMBU YA KUZALIWA MTOTO

Familia ya Bw. na Bi. Lameck Mangala wa Namtumbo inapenda kuwaalika Ndg./Mch./Mwl./Dkt./Prof........................ kwenye sherehe ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwa mtoto wao mpendwa, Paulo Mangala, itakayofanyika katika Ukumbi wa Sabasaba, siku ya Jumamosi tarehe 25/05/2019 kuanzia saa 10:30 jioni mpaka saa 2:00 usiku.

Majibu kwa wasiofika:
Mangala Makemba,
S.L.P. 126,
Namtumbo.
Simu 075000000

FOR ONLINE USE ONLY

**Maswali**

1. Mwandishi wa kadi hiyo ni nani?
2. Kwa mujibu wa kadi hiyo, ni tukio gani linakusudiwa kutokea?
3. Namba za mawasiliano katika kadi ya mwaliko zina umuhimu gani?
4. Eleza faida ya kutaja muda na mahali tukio litakapofanyika katika kadi ya mwaliko.

Fot online use only
do not duplicate

**Zingatia**

Kadi za mialiko huandikwa kwa ajili ya kuwakaribisha watu kuhudhuria tukio fulani kama vile harusi, akika, ubatizo, mahafali, au harambee. Kadi husaidia kumkaribisha mwalikwa na kumwelekeza mahali tukio litakapofanyika. Vilevile, humsaidia mwalikwa kujua tarehe na siku ya tukio husika.

**Kazi ya 7.13**

1. Kusanya kadi mbalimbali za mialiko.
2. Chunguza muundo na taratibu za uandishi wa kadi ulizozikusanya.
3. Andaa kadi ya mwaliko ukimwalika mwalimu wako wa darasa kuhudhuria sherehe ya mahafali ya kaka yako anayehitimu kidato cha nne.

**Zoezi la 7.5**

1. Eleza kwa ufupi maana ya kadi za mialiko.
2. Fafanua vipengele vya kuzingatia katika kuandika kadi za mialiko.
3. Kadi za mialiko zina umuhimu gani katika jamii?

FOR ONLINE USE ONLY

## Dayalojia

**Kazi ya 7.14**

**Soma dayalojia ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Mwanafunzi:** Shikamoo mwalimu.

**Mwalimu:** Marahaba, hujambo? (*Anaitikia salamu kwa ukali.*)

**Mwanafunzi:** Sijambo mwalimu.

**Mwalimu:** Mbona umechelewa kufika shuleni leo? (*Anaongea kwa ukali huku ameshika kiboko mkononi.*)

**Mwanafunzi:** Samahani mwalimu, nina … (*Anashindwa kuongea vizuri.*)

**Mwalimu:** Una nini? (*Anamnyooshea kiboko.*)

**Mwanafunzi:** (Kwa huzuni) Nina tatizo mwalimu. Mdogo wangu … (*anatokwa na machozi.*) Amepata ajali asubuhi ya leo. Amegongwa na pikipiki na amevunjika mguu. Hivi sasa,



KISWAHILI FINAL.indd 82 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

| | |
|---|---|
| | yuko hospitalini. |
| **Mwalimu:** | Du! Pole sana! Anaendeleaje? (*Anauliza kwa huzuni.*) |
| **Mwanafunzi:** | Anaendelea vizuri kiasi mwalimu. (*Anamjibu kwa huzuni.*) |
| **Mwalimu:** | Lo! Pole sana! Mungu atamponya. (*Anamshika bega na kumbembeleza.*) |
| **Mwanafunzi:** | Asante mwalimu! (*Anamgeukia mwalimu*). Nimekuja kuomba ruhusa ili niende kumsaidia mdogo wangu na kumpelekea chakula. |
| **Mwalimu:** | Ngoja nimwite kiranja wa zamu ili alete daftari la ruhusa. (*Anaita, Masanja*! ...) |
| **Masanja:** | Naam, mwalimu! (*Anakuja kwa haraka.*) |
| **Mwalimu:** | Ninaomba uniletee daftari la ruhusa. (*Daftari linaletwa na mwalimu anaandika ruhusa, kisha anamruhusu mwanafunzi.*) |
| **Mwanafunzi:** | Asante mwalimu. (*Anaanza kuondoka.*) |
| **Mwalimu:** | Pole sana! Mwenyezi Mungu amponye. (*Anaondoka kuelekea darasani kufundisha.*) |
| **Mwanafunzi:** | Asante, mwalimu! (*Anaitikia kwa mbali huku akiondoka.*) |

FOR ONLINE USE ONLY

**Maswali**

1. Ni wahusika wangapi wameshiriki katika dayalojia hiyo?
2. Dayalojia hiyo inahusu nini?
3. Kwa nini mwalimu alimruhusu mwanafunzi kurudi nyumbani?
4. Eleza mbinu zilizotumika kuandika dayalojia hiyo.

**Zingatia**

Dayalojia ni mazungumzo ya kupokezana kati ya watu wawili au zaidi. Mazungumzo hayo yanaweza kuwa ya ana kwa ana au kwa njia ya simu. Pia, huweza kuandikwa au kuzungumzwa. Dayalojia zinazoandikwa ni pamoja na michezo ya redio, tamthilia, na maigizo. Dayalojia huandikwa kwa kuzingatia jambo linalomsukuma mwandishi kuandika dayalojia kulingana na mahitaji ya jamii anayoiandikia. Mwandishi anapaswa kutoa maelekezo ya ufafanuzi katika mabano ili kumfahamisha msomaji matendo yanayofanywa na wahusika.



KISWAHILI FINAL.indd 83 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

Kadhalika, mazungumzo yanapaswa yawe ya mkato na yasiyozidiana sana kati ya wahusika, yaani mhusika mmoja asitawale mazungumzo kuliko wengine ili kila mhusika aweze kushiriki kikamilifu. Pia, ni muhimu kuzingatia matumizi ya vihisishi ili kufanya dayalojia iwe na vionjo vyenye kusisimua. Mwandishi anapaswa kuhakikisha kunakuwa na mwingiliano na udakizi wa mazungumzo ya wahusika ili dayalojia iwe na uhalisi. Aidha, ni muhimu kuzingatia upangaji wa mawazo kimantiki kwa kufuata mtiririko wa matukio au visa na kugawa majukumu ya wahusika kulingana na mandhari waliyomo pamoja na matendo yao. Kwa mfano, kama mhusika ni mvuvi, vifaa anavyopewa kutumia, lugha anayopewa kuzungumza, na matendo yake lazima viendane na mandhari ya uvuvi.

**Zoezi la 7.6**

1. Unaelewa nini kuhusu dayalojia?
2. Fafanua mambo ya kuzingatia katika uandishi wa dayalojia.

**Kazi ya 7.15**

**Soma dayalojia ifuatayo, kisha igiza dayalojia hiyo na wenzako darasani.**

FOR ONLINE USE ONLY

**Kalinge:** Bwana Luhende, habari ya leo? (*Anamsabahi kwa uchangamfu.*)

**Luhende:** Nzuri! (*Anaitikia salamu kwa unyonge.*)

**Kalinge:** Rafiki yangu, unaumwa? Unaonekana mnyonge na mwenye mawazo sana. Kulikoni?

**Luhende:** Siumwi, ila nina mgonjwa hapa hospitalini. Amelazwa tangu juzi.

**Kalinge:** Mgonjwa ni nani wako?

**Luhende:** Mdogo wangu.

**Kalinge:** Du! Pole sana! Anaumwa nini? (*Anauliza kwa sauti ya mshangao na huzuni.*)

**Luhende:** Anaumwa malaria. Amepimwa na kugundulika kuwa ana malaria kali sana. Hivyo, amelazwa.

**Kalinge:** Anaendeleaje?



KISWAHILI FINAL.indd 84 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Luhende:** Madaktari wameniambia kuwa ana nafuu kidogo. Sijapata kumwona kwa kuwa madaktari wanawatembelea wagonjwa.

**Kalinge:** Alikuwa na dalili zipi?

**Luhende:** Alikuwa anapoteza fahamu. Pia, alikuwa kama mtu aliyechanganyikiwa. Si hivyo tu, tulipofika hapa hospitalini, madaktari walituambia ana upungufu wa damu. (*Anapiga chafya.*)

**Kalinge:** *(Anamuuliza kwa mshangao.)* Hali hii inasababishwa na nini?

**Luhende:** Kuchelewa kupata matibabu! (*Anainamisha kichwa chini.*)

**Kalinge:** Mh! Ugonjwa huu ni hatari sana. (*Anaguna kidogo.*)

**Luhende:** Madaktari wanasema kuwa wadudu wa malaria wajulikanao kama plasimodiamu wakiingia mwilini wanavunjavunja seli hai nyekundu, hali inayosababisha mtu kuishiwa damu.

**Kalinge:** Loo! Hii ni hatari. Tutakwisha! Tunatakiwa kuchukua tahadhari kubwa.

**Luhende:** Kweli kabisa! Hata wahenga walisema kuwa kinga ni bora kuliko tiba. (*Anasema kwa msisitizo.*)

**Kalinge:** Ndiyo maana serikali yetu imeamua kuelimisha watu kuhusu kuchukua tahadhari ili kujikinga na ugonjwa huu.

FOR ONLINE USE ONLY

**Luhende:** Hiyo ni tahadhari nzuri.

**Kalinge:** Hata sisi tunatakiwa kuchukua tahadhari.

**Luhende:** Kweli kabisa! Tunapaswa kusafisha mazingira ili kusiwe na mazalia ya mbu, kulala kwenye vyandarua, na kupulizia dawa ya mbu. *(Anaongea kwa kusisitiza.*)

**Kalinge:** Ninakushukuru rafiki yangu kwa elimu hii ya ugonjwa wa malaria. Ninamwombea mgonjwa wako apone haraka.

**Luhende:** Asante, kwa heri! (*Wanaagana kwa kupungiana mikono, kisha wanaondoka.*)



KISWAHILI FINAL.indd 85 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

## Zoezi la marudio la 7

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

(i) Chunguza taarifa ifuatayo, kisha jibu swali linalofuata.

Skuli ya Sekondari Bandarini,
S.L.P. 197,
**Zanzibar**.
17/3/2021.

Taarifa hii ina vipengele vingapi?

(a) Kimoja: anwani ya mwandishi

(b) Viwili: anwani ya mwandishi na tarehe

(c) Viwili: anwani ya mwandishi na alama za uandishi

(d) Vitatu: anwani ya mwandishi, mji aliopo mwandishi, na tarehe

(e) Vinne: sehemu mahsusi aliyopo mwandishi, sanduku la posta, mji aliopo mwandishi, na tarehe

(ii) Vifuatavyo ni vipengele muhimu vinavyopaswa kuwamo katika kadi za mwaliko, isipokuwa ………………..

FOR ONLINE USE ONLY

(a) cheo cha mwalikwa

(b) mahali pa kufanyikia tukio

(c) maudhui ya tukio

(d) vihisishi vya kusisitiza jambo

(e) muhusika wa tukio

(iii) Chunguza aina zifuatazo za uandishi wa tarehe, kisha bainisha aina iliyoandikwa kimakosa ………………..

(a) 9/12/1961

(b) 9-12-1961

(c) 9.12.1961

(d) 9 Desemba, 1961

(e) Desemba 9, 1961



KISWAHILI FINAL.indd 86 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

(iv) Ipi kati ya seti zifuatazo ni sahihi zaidi katika kanuni za uandishi wa dayalojia?

(a) Ubanaji wa maneno, maelekezo ya vitendo, na anwani za watendaji

(b) Maelekezo ya vitendo, matumizi ya vihisishi, na anwani za wahusika

(c) Matumizi ya vihisishi, maelekezo ya vitendo, na uzingatiaji wa muwala

(d) Uzingatiaji wa mantiki, ujenzi mzuri wa uhusika, na saini za wahusika

(e) Uzingatiaji wa muwala, anwani za wahusika, na ubanaji wa maneno

(v) Vipengele vifuatavyo hutumiwa katika uandishi wa barua rasmi na baruapepe, isipokuwa ............. .

(a) anwani ya mwandishi na mwandikiwa

(b) lengo

(c) mada/kichwa

(d) saini

(e) jina la mwandishi

FOR ONLINE USE ONLY

2. Oanisha maelezo yaliyopo fungu A na dhana zilizopo fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi ili kukamilisha maana.

| **Fungu A** | **Fungu B** |
|---|---|
| (i) Huandikwa juu kwenye pembe ya upande wa kulia wa karatasi. | A. barua rasmi |
| (ii) Wako katika ujenzi wa taifa | B. ndugu |
| (iii) Hutumia maneno maalumu yenye kuzingatia maadili. | C. insha |
| (iv) Hurahisisha kujua barua iliandikwa lini. | D. tarehe |
| (v) Neno linalosimama badala ya salamu katika barua rasmi. | E. kimalizio cha barua rasmi |
| | F. barua za kirafiki |
| | G. anwani ya mwandishi |

Fot online use only
do not duplicate

3. Eleza mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha za hoja.
4. Mwandikie baruapepe rafiki yako ukimweleza namna unavyoendelea na masomo yako.
5. Eleza njia zinazotumika katika kuwasilisha dayalojia.
6. Kwa kutumia mifano, tofautisha baruapepe na ujumbe mfupi wa simu ya mkononi.
7. Andika dayalojia kuhusu elimu ya mazingira.

FOR ONLINE USE ONLY

Fot online use only
do not duplicate

# Sura ya Nane

## Usimuliaji

**Utangulizi**

*Watu huweza kupashana habari kwa njia mbalimbali. Usimuliaji ni njia mojawapo inayotumika katika kupeana habari. Katika sura hii, utajifunza namna ya kusimulia matukio mbalimbali kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kukuza stadi za kuzungumza, kusikiliza, na kufikiri kitunduizi.*

### Kusimulia matukio mbalimbali kwa ufasaha

**Kazi ya 8.1**

**Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**



**Maswali**

1. Mtu aliyekaa kwenye kiti anafanya nini?
2. Watoto waliokaa kwenye mkeka wanafanya nini?



KISWAHILI FINAL.indd 89 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

**Zingatia**

Masimulizi ni maelezo yanayotolewa kuhusu namna tukio fulani lilivyotokea katika kipindi fulani cha maisha. Tukio hilo linaweza kuwa la furaha kama vile kufaulu mitihani, kuzaliwa kwa mtoto, kutembelea mbuga za wanyama, au la huzuni kama vile kuvamiwa kwa kijiji, kupata ajali, kuzama kwa meli, kupinduka kwa gari, kutokea kwa ukame, kutokea kwa kundi la nzige, kutokea kwa mafuriko, na kutokea kwa njaa au vita. Utoaji wa maelezo kuhusu tukio fulani ndio huitwa usimuliaji. Msimuliaji huelezea nini kilitokea, jinsi kilivyotokea, mahali kilipotokea, sababu za kutokea kwake, na athari zilizojitokeza. Hivyo, msimuliaji anatakiwa kutoa maelezo muhimu ambayo yataiwezesha hadhira kulielewa ipasavyo tukio linalosimuliwa.

Msimuliaji anapaswa kuifahamu hadhira yake. Pia, anatakiwa kuwa na uelewa mpana wa lugha na utamaduni unaohusika kwani utamwezesha kuwasilisha vyema masimulizi yake bila makosa. Aidha, anapaswa kuwa na mbinu za kifaraguzi zifaazo katika usimuliaji. Mbinu hizo ni pamoja na uwezo wa kuunda, kugeuza, na kuwasilisha kazi yake papo kwa papo kulingana na hadhira yake. Kwa mfano, msimuliaji huweza kutunga wimbo na kuiimbisha hadhira yake anapoona imechoka au inataka kusinzia.

Vilevile, msimuliaji anapaswa kuzifahamu tabia za binadamu, ikiwa ni pamoja na mambo ya kumkera, kumfurahisha, kumhuzunisha, kumchangamsha, au kumvutia. Jambo hili litamwezesha kubaini matakwa ya hadhira yake wakati wa usimuliaji. Hivyo, anaweza kubadili usimuliaji wake ili kukidhi matakwa hayo. Hali kadhalika, anatakiwa kuwa na uwezo wa kuonesha hisia kulingana na kile anachokiwasilisha. Kwa mfano, ikiwa ni masimulizi ya huzuni, aoneshe hisia za huzuni, ikiwa ni masimulizi ya furaha basi naye aoneshe hisia za furaha.

**Kazi ya 8.2**

**Soma masimulizi ya "Ulemavu si Ugonjwa", kisha msimulie mwanafunzi mwenzako darasani.**

**Ulemavu si Ugonjwa**

Ilikuwa siku ya Jumatatu tarehe 20 Februari 2016, majira ya saa 12 alfajiri, siku ambayo nilipata ajali ya gari nilipokuwa navuka barabara kuelekea shuleni. Ajali hiyo ilitokana na kugongana kwa basi la Muungano lililokuwa linafanya safari zake Iringa na Dodoma na daladala iliyokuwa inatoka Dodoma kwenda Mtera. Basi hilo lilikuwa katika mwendo wa kasi sana. Lilipojaribu kuikwepa

Fot online use only
do not duplicate

daladala iliyokuwa inakuja mbele yake ndipo magari hayo yaligongana uso kwa uso. Kwa kuwa mimi nilikuwa ninavuka barabara, nilisukumwa na daladala hiyo na kuangukia jiwe lililokuwa pembeni mwa barabara. Jiwe hilo liliniumiza sehemu ya mgongo, hali iliyonisababishia kupooza miguu. Pia, nilivunjika mkono wa kushoto na kupata majeraha sehemu mbalimbali za mwili.

Chanzo cha ajali hiyo kilikuwa uzembe wa dereva wa basi la abiria aliyekuwa anaendesha basi kwa mwendo wa kasi bila tahadhari. Kwa hakika, ajali hiyo ilikuwa na madhara makubwa, kwani abiria kumi wa daladala na saba wa basi walipoteza maisha papo hapo. Aidha, abiria ishirini wa basi na kumi wa daladala walijeruhiwa vibaya.

Polisi walipigiwa simu na mashuhuda wa ajali hiyo. Walifika kwa haraka katika eneo la tukio. Waliwakamata madereva wote wawili na kuwapeleka katika Kituo cha Polisi cha Mtera. Punde si punde, gari la kubeba wagonjwa lilifika eneo la ajali, likatubeba majeruhi hadi Hospitali ya Wilaya ya Mpwapwa kwa ajili ya kupatiwa huduma za matibabu.

Tukiwa njiani kuelekea hospitalini, nilipoteza fahamu kutokana na kuvuja damu nyingi. Nilizinduka siku ya pili majira ya saa 11:00 jioni. Nilishangaa kuona nimezungukwa na madaktari, manesi, pamoja na wanafunzi wenzangu huku nikiwa nimefungwa bandeji miguuni na mkononi. Nilitaka kusimama, lakini nilishindwa. Niliendelea kulala kitandani. Wazazi wangu nao walikuwapo pale hospitalini kwa sababu tayari walikuwa wamepata taarifa za ajali ile.

Niliruhusiwa baada ya matibabu ya mwezi mmoja pale hospitalini, lakini tayari nilikuwa na ulemavu wa kudumu. Nilipofika nyumbani, wanafunzi wenzangu ambao hawakupata nafasi ya kuniona nilipokuwa hospitalini, walikuja nyumbani kunijulia hali na kunipa pole. Nilifarijika sana, lakini nilikuwa nimekata tamaa ya kuendelea na masomo. Nilikuwa ninajawa na mawazo nikijiuliza maswali mbalimbali, ikiwa ni pamoja na namna ya kurudi shuleni.

Niliamua kuwaambia wazazi wangu juu ya wazo langu la kuacha shule. Wazazi wangu walikataa wazo hilo. Walinishauri na kunisihi nisiache shule. Waliniambia kuwa kilema si ugonjwa. Waliniahidi kunipangia nyumba eneo la jirani na shule. Baada ya ushauri wa wazazi wangu, nilikubali kuendelea na shule.

Shule ilipofunguliwa, mama yangu aliambatana nami kuelekea shuleni. Nilipangiwa nyumba karibu na shule ambamo niliishi pamoja na wanafunzi wenzangu. Pia, nilinunuliwa kiti cha kutembelea pamoja na mahitaji yote ya shule. Nilipofika shuleni, nilipokelewa na walimu na wanafunzi wenzangu.



KISWAHILI FINAL.indd 91 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

Walinipa pole kutokana na ajali ile iliyonisababishia ulemavu wa kudumu.

Kama kawaida yangu, nilianza kusoma kwa bidii. Nilikuwa mwanafunzi wa kidato cha nne; hivyo, nilikaza buti kuhakikisha kuwa ninaambulia chochote katika matokeo. Muda wa kujisajili kwa ajili ya mtihani ulipofika, tulisajiliwa wanafunzi 50 kufanya mtihani wa kidato cha nne. Niliendelea kusoma kwa bidii zaidi. Muda wa kufanya mtihani ulipofika, tulifanya mtihani vizuri. Nilimaliza mitihani yangu na kurudi nyumbani kwetu, huku nikisubiri matokeo kwa hamu kubwa.

Baada ya miezi mitatu, Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani alitangaza matokeo. Shule yangu ilikuwa imefanya vizuri. Ilikuwa imeshika nafasi ya ishirini kitaifa na ya kwanza kimkoa. Nilipata ufaulu wa daraja la kwanza na nilifanya vizuri zaidi katika masomo ya sayansi. Walimu wangu walinipigia simu na kunipongeza kwa ufaulu huo.

Nilichaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika Shule ya Sekondari Jangwani iliyoko jijini Dar es Salaam. Wazazi wangu walifurahi sana. Muda wa kwenda shuleni ulipokaribia, walininunulia mahitaji yote ya shule. Shule ilipofunguliwa, baba alinipeleka shuleni kuripoti. Tulipofika shuleni, tulipokelewa na walimu na wanafunzi wenzangu ambao walikuwa wametangulia kufika. Nilipewa ushirikiano wa kutosha kutokana na ulemavu wangu. Nilisoma kwa bidii. Nilikuwa nikiongoza katika majaribio na mitihani ya mihula. Walimu wangu walinipenda sana.

FOR ONLINE USE ONLY

Baada ya miaka miwili, tulifanya mitihani ya kumaliza kidato cha sita. Tulipomaliza mitihani, nilirejea nyumbani kwetu kusubiri matokeo. Baada ya miezi miwili hivi, matokeo yalitangazwa. Nilikuwa nimefaulu kwa kiwango cha daraja la kwanza tena. Wazazi wangu walifurahi na kunipongeza.

Niliomba kujiunga na mafunzo ya shahada ya awali ya udaktari wa binadamu katika fani ya mifupa katika Chuo Kikuu cha Muhimbili. Nilichaguliwa kujiunga na mafunzo hayo. Niliomba mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Nilipata mkopo kwa asilimia mia moja. Nilisoma kwa bidii. Baada ya miaka mitano, nilihitimu mafunzo yangu ya udaktari na kuajiriwa katika Hospitali ya Bugando iliyoko jijini Mwanza kama daktari wa mifupa. Kwa hakika, ulemavu si ugonjwa.

Fot online use only
do not duplicate

**Maswali**

1. Msimuliaji alipatwa na kitu gani?
2. Tukio hilo lilitokea wapi?
3. Eleza chanzo cha tukio hilo.
4. Bainisha wahusika wa tukio hilo.
5. Fafanua madhara ya tukio hilo.

**Zingatia**

Wakati wa kusimulia tukio, msimuliaji anatakiwa kubainisha mambo kadhaa. Kwanza, anatakiwa kubainisha aina ya tukio analolisimulia katika maelezo yake. Kwa mfano, anatakiwa kubainisha kama ni tukio la harusi, siku ya kuanza kidato cha kwanza, ajali ya barabarani, au uchaguzi wa viongozi. Pia, msimuliaji anatakiwa kueleza mahali tukio lilipotokea ili msikilizaji wake aweze kumwelewa. Hali kadhalika, msimuliaji anatakiwa kumweleza msikilizaji wake wakati ambapo tukio limetendeka. Kwa mfano, anatakiwa kueleza kama lilitokea asubuhi, mchana, jioni au hata usiku. Zaidi, anatakiwa kueleza kuhusu siku, mwezi, mwaka bila kusahau muda halisi, yaani ilikuwa saa ngapi.

Aidha, msimuliaji wa tukio hana budi kutaja wahusika wa tukio. Kwa mfano, tukio limehusisha wahusika gani, jinsi zao na umri wao au limehusisha vitu gani. Aghalabu, msimuliaji anatakiwa kueleza chanzo cha tukio au sababu za tukio. Aidha, msimuliaji wa tukio lazima abainishe mwisho wa tukio kilitokea nini au hatima yake ilikuwaje. Kwa mfano, kama ni ajali, hatima inaweza kuwa dereva anayehusika kuadhibiwa na majeruhi kupelekwa hospitalini.

Pia, msimuliaji anatakiwa kuzingatia lafudhi na matamshi sahihi ya maneno ili kumwezesha msikilizaji kuelewa kile kinachosimuliwa. Msimuliaji hana budi kuweka msisitizo panapostahili na kupambanua kauli, kama ni kauli halisi, aiseme na kama ni kauli taarifa, aiseme. Vilevile, anapaswa kuzingatia mpangilio mzuri wa mawazo ili kuleta mantiki. Mpangilio mzuri wa mawazo humwezesha msikilizaji kuelewa kwa urahisi kile kinachosimuliwa. Msimuliaji hana budi kuzingatia urefu wa masimulizi. Masimulizi yake yasiwe marefu sana kiasi cha kupoteza muda na kumchosha msikilizaji au hadhira yake.



KISWAHILI FINAL.indd 93 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

## Zoezi la 8.1

1. Unaelewa nini kuhusu usimuliaji?
2. Eleza sifa tano za msimuliaji.
3. Bainisha njia za usimuliaji wa matukio.
4. Fafanua mambo ya kuzingatia katika usimuliaji wa matukio.
5. Eleza vipengele vya usimuliaji wa matukio.
6. Kwa kawaida, masimulizi huwa na muundo gani?

## Zingatia

Masimulizi yanaweza kuambatana na matumizi ya viungo vya mwili ili kufanya usimuliaji uwe hai. Kwa minajili hiyohiyo, masimulizi yanaweza kuishirikisha hadhira katika kutenda matendo mbalimbali kama vile kuimba, kuitikia, kupiga makofi, kushangilia, na kucheka. Matendo hayo huifanya hadhira isichoke wala kusinzia.

Vilevile, masimulizi yanapaswa kutumia lugha inayoeleweka na yenye kuvutia itakayoifanya hadhira ivutiwe na masimulizi na iendelee kusikiliza. Pia, masimulizi hufanywa kwa hisia kulingana na tukio linalosimuliwa. Kwa mfano, kama tukio ni la furaha inafaa lisimuliwe kwa furaha; na kama ni la huzuni, lisimuliwe kwa huzuni. Mwisho, msimuliaji anaweza kusimulia kwa njia ya ufaraguzi, ambapo atatumia ufundi wa papo kwa papo ili kuibua hisia na kuburudisha hadhira yake.

## Kazi ya 8.3



Kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, simulia tukio lolote lililowahi kutokea katika mazingira unayoishi.



KISWAHILI FINAL.indd 94 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

## Zoezi la marudio la 8

1. Oanisha maelezo yaliyopo fungu A na dhana zilizopo fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi ili kukamilisha maana.

| Fungu A | Fungu B |
|---|---|
| (i) Eleza kwa mdomo tukio la kubuni au la kweli. | A. kiini cha masimulizi |
| (ii) Watendaji wa matukio yanayoelezwa katika kisa ili kutoa ujumbe. | B. wahusika |
| (iii) Matamshi sahihi yanayosaidia kueleweka kwa masimulizi. | C. simulia |
| (iv) Huelezea tukio halisi kwa undani kwa kuzingatia chanzo, wahusika, na wakati. | D. uhai wa masimulizi |
| (v) Matumizi ya viungo vya mwili, kwa mfano, kupiga makofi katika masimulizi. | E. fafanua |
| | F. lafudhi |
| | G. hadithia |

FOR ONLINE USE ONLY

2. Eleza mbinu tatu za kifaraguzi ambazo msimuliaji anaweza kuzitumia katika kusimulia matukio.
3. Linganisha na tofautisha usimuliaji wa matukio ya kale na ya sasa.
4. Usimuliaji wa matukio una umuhimu gani katika maisha ya kila siku?
5. Fafanua faida za kuishirikisha hadhira katika masimulizi.

Fot online use only
do not duplicate

# Sura ya Tisa

## Ufahamu

**Utangulizi**

*Ufahamu ni hali ya kuelewa jambo na kuweza kulifafanua kwa kutoa taarifa zinazohusiana nalo. Katika sura hii, utajifunza ufahamu wa kusikiliza, ufahamu wa kuona, ufahamu wa kusoma, kusoma kwa burudani, na matumizi ya kamusi. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kusoma maandishi, kusikiliza sauti, na kutoa taarifa kuhusiana na habari utakayoisoma au kuisikiliza.*

### Ufahamu wa kusikiliza

**Kazi ya 9.1**



**Sikiliza mwenzako akisoma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Nchi ya Rahatele**

Katika nchi ya Rahatele, waliishi wananchi wachapakazi na wasikivu. Wananchi hawa walisikiliza kila jambo waliloambiwa na mtu yeyote, awe wa ndani au nje ya nchi yao. Walifanya kazi kwa maslahi mapana ya nchi yao. Kila agizo lililotolewa na Mfalme au Malkia lilisikilizwa na kutekelezwa ipasavyo. Mfalme aliyeitwa Bwana Misifa, na Malkia aliyeitwa Chaurembo walifurahishwa sana na tabia hii.

Siku zilikwenda na kupita. Polepole, wananchi wa Rahatele walijisahau na kuanza kukengeuka. Waliacha tabia ya kufanya kazi wakaendekeza uvivu na ulevi wa kupindukia. Wananchi kutoka nchi za jirani waliwashauri, lakini hawakuwasikiliza hata kidogo.

Uchumi wa nchi ya Rahatele ulianza kuyumba na, hatimaye, kuporomoka kabisa. Mfalme alitoa agizo kwa kila mwananchi kufanya kazi kwa bidii na kuacha ulevi, lakini wapi. Wananchi wake hawakumsikiliza hata kidogo. Agizo lake lilipuuzwa. Mfalme alikasirika sana. Akaamuru askari wake kumkamata mtu yeyote ambaye hakutii agizo lake. Watu walikamatwa na kufungwa jela, lakini wapi. Waliobaki waliendelea na tabia ya kutofanya kazi na kuendekeza



KISWAHILI FINAL.indd 96 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

ulevi.

Hali hiyo iliendelea kwa muda mrefu kidogo. Hatimaye, akiba ya chakula waliyokuwa nayo iliisha. Ikatokea njaa kali kutokana na uhaba wa chakula ulioikabili nchi ya Rahatele. Watu walianza kumlilia Mfalme wao ili awasaidie chakula kwani wangekufa kwa njaa. Pia, walimwomba msamaha kwa kutosikiliza maagizo yake.

Mfalme aliwaonea huruma wananchi wake. Akaamua kuwasamehe. Aliwaambia kuwa atawasaidia, lakini wanapaswa kujifunza. Aliwanunulia chakula kutoka nchi za jirani, akawagawia, na kuwataka wafanye kazi kwa bidii na kuacha uvivu.

Baada ya baa la njaa kupita, wananchi wa Rahatele walianza kubadilika. Walianza kufanya kazi za shambani kwa bidii. Walipata mavuno mengi ya mazao mbalimbali. Uchumi wa mwananchi mmojammoja na wa nchi kwa ujumla ulifufuka na kuimarika. Walianza kuishi tena maisha ya raha. Hawakutaka kuisikia tena harufu ya pombe. Waliendelea na tabia ya kufanya kazi na kuwa wasikivu kama ilivyokuwa hapo awali.

**Maswali**

1. Fafanua sababu mbili za kushuka kwa uchumi wa nchi ya Rahatele.
2. Bainisha vitendo viwili vinavyoonesha kuwa mfalme aliwapenda wananchi wake.
3. Fafanua mambo matatu muhimu yaliyowasaidia wananchi wa Rahatele kupata mavuno mengi.
4. Bainisha tabia mbili ambazo wananchi wa Rahatele walikuwa nazo kabla ya kuzuka kwa baa la njaa.

FOR ONLINE USE ONLY

**Zingatia**

Ufahamu wa kusikiliza ni uelewa ambao mtu huupata kutokana na kusikiliza jambo analosomewa au kusimuliwa. Msikilizaji anatakiwa kuwa makini na kuelekeza akili yote kwa mzungumzaji au msimulizi ili kuweza kusikia kile kinachozungumzwa, kinachosomwa, au kinachosimuliwa. Pia, msikilizaji anatakiwa kuzingatia hoja kuu. Anaweza kuandika hoja hizo ili azikumbuke hapo baadaye. Aidha, msikilizaji anapaswa kuwa makini, hasa pale mzungumzaji, msimuliaji, au msomaji anapotumia ishara mbalimbali kama vile kurusha mikono, kutingisha kichwa, kutingisha mabega, au kupepesa macho. Kwa kiasi kikubwa, ishara hizi huchangia kupata maana katika mazungumzo.



KISWAHILI FINAL.indd 97 2021/09/13 12:13

Fot online use only
do not duplicate

Msikilizaji wa habari inayozungumzwa au kusomwa anatakiwa kusikiliza kwa makini ili aweze kuelewa na kubaini mawazo makuu. Aidha, anapaswa kubaini iwapo mambo muhimu yaliyomo katika habari hiyo yanaendana nayo. Ili afanikiwe kuyatekeleza haya, msikilizaji anapaswa kuyaelewa matamshi ya mzungumzaji.

Msikilizaji anapaswa kubaini mawazo makuu yaliyojitokeza katika habari aliyoisikiliza. Kulifanikisha hili, anatakiwa kuzingatia mada ili aweze kujipima kama ameelewa aliyoyasikia. Mzungumzaji anapaswa kupanga maelezo kwa usahihi na kusema kwa kifupi na kwa lugha sahihi.

**Kazi ya 9.2**

Fupisha habari uliyoisikiliza kuhusu nchi ya Rahatele kwa maneno 150.

**Zoezi la 9.1**

1. Fafanua mambo ya kuzingatia wakati wa ufahamu wa kusikiliza.
2. Bainisha milango miwili ya fahamu inayohusika katika ufahamu wa kusikiliza.

FOR ONLINE USE ONLY

## Ufahamu wa kuona

**Kazi ya 9.3**

**Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**






KISWAHILI FINAL.indd 98 2021/09/13 12:14

Fot online use only
do not duplicate

**Maswali**

1. Picha hiyo inahusu nini?
2. Mtu aliyesimama anafanya nini?
3. Kitendo hicho kimetokea mahali gani?
4. Bainisha makundi mawili ya watu wanaoonekana kwenye picha.

### Zingatia

Ufahamu wa kuona huhusisha kutazama tukio, picha, grafu, au vitu vingine vya kuonekana. Vitu huonwa mubashara kwa njia ya ana kwa ana au kupitia televisheni, filamu, na video. Katika ufahamu wa kuona, watu hutumia maarifa waliyonayo kuchanganua kitu au jambo walililoliona na kulieleza kwa njia ya masimulizi au maandishi. Mtazamaji wa tukio fulani anapaswa kubaini tukio linahusu nini, wahusika wa tukio ni kina nani, tukio limetokea mahali gani, tukio limetokea muda gani, na limesababisha athari gani.

### Kazi ya 9.4

Andika aya moja kuhusu picha uliyopewa katika kazi ya 9.3.

FOR ONLINE USE ONLY

## Ufahamu wa kusoma

### Kazi ya 9.5

**Soma habari ifuatayo, kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Ili kuondoa utata wa matumizi ya maneno **sanaa** na **fasihi**, inafaa kuyaeleza maneno hayo kwa uwazi zaidi. Sanaa imeelezwa kuwa ni uzuri ulio katika umbo lililosanifiwa. Fasihi ni sehemu ya uzuri huo. Katika fasihi, kuna uzuri wa kifasihi na wa jambo linalosemwa. Uzuri wa kifasihi huitwa fani na jambo lisemwalo huitwa maudhui. Kwa maneno mengine, sanaa ya fasihi inaundwa na fani na maudhui. Fasihi lazima iwe na sehemu hizi mbili. Ikikosekana mojawapo, kazi haiwi ya kifasihi.

Mtunzi wa kazi ya fasihi huwa na jambo la kusema na huwa na namna ya kulisema. Kwa hiyo, ana dhamira na anatumia ufundi wa maneno mbalimbali kufikisha dhamira yake.

Kazi ya fasihi inaweza kuwa na upungufu kutokana na upotofu wa fani au wa maudhui. Maudhui yanajengwa na dhamira, ujumbe, maadili, falsafa, na mara

Fot online use only
do not duplicate

nyingine, suluhisho. Dhamira ya mtunzi ikiwa potofu au ikiwa haikubaliki katika jamii, inapunguza uzuri wa kazi yake.

**Chanzo:** Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Tanzania (1992:160).

**Maswali**

1. Kwa mujibu wa habari hii, nini maana ya fasihi?
2. Eleza tofauti iliyopo kati ya sanaa na fasihi.
3. Mtunzi anaposema kazi ya fasihi inaweza kuwa na upungufu kutokana na upotofu wa fani au maudhui, ana maana gani?
4. Eleza umuhimu wa sanaa katika fasihi.
5. Fafanua umuhimu wa fani na maudhui katika fasihi.

**Zingatia**

Ufahamu wa kusoma ni uelewa wa jambo fulani anaoupata mtu kutokana na kusoma kifungu cha habari, makala, matini, kitabu, au gazeti. Ili aweze kuelewa, msomaji anahitaji kubainisha mawazo makuu yanayotokana na habari aliyoisoma. Msomaji anaweza kuelewa jambo kupitia kusoma kwa sauti au kusoma kimya. Anaposoma kwa sauti, msomaji huzingatia matamshi sahihi ya maneno na nguvu ya utamkaji wa silabi zenye mkazo katika maneno ili kupata maana sahihi ya maneno. Anaposoma kimyakimya, huzingatia alama za uandishi na mtiririko wa aya.

FOR ONLINE USE ONLY

**Kazi ya 9.6**

**Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Kijiji cha Kivumbi kilikuwa na watu wengi walioishi kwa kushirikiana. Watu wa kijiji hicho walifanya kazi kwa umoja na ushirikiano. Ardhi ya Kivumbi ilikuwa kubwa na yenye rutuba, lakini chakula kilikuwa haba kutokana na ukame. Ukosefu wa mvua kwa muda mrefu ulisababisha vijito na visima vidogovidogo vilivyokuwapo kukauka. Watu wa Kijiji cha Kivumbi waliishi kwa taabu na mifugo yao ilidhoofu.

Kijijini humo mlikuwa na mzee mmoja aliyejulikana kwa jina la Ndumbwi. Mzee Ndumbwi alikuwa na hekima na busara nyingi, na hakupendezwa na hali ya Kijiji cha Kivumbi. Siku moja, aliwaita watu wote kijijini humo. Alitaka



KISWAHILI FINAL.indd 100 2021/09/13 12:14

Fot online use only
do not duplicate

awaambie mawazo yake.

Watu walipokusanyika, Mzee Ndumbwi alisimama akawaambia, "Ndugu zangu, nina neno la kuwaambia." Watu wote wakanyamaza ili wamsikilize. Akamwita mtoto mmoja apite mbele yao. Akampa kijiti kimoja. Akamwambia, "Vunja." Mtoto akakivunja kijiti kile kwa urahisi. Mzee Ndumbwi akampa vijiti kumi vilivyofungwa pamoja ili avivunje. Mtoto akashindwa kuvivunja. Akamwita Mzee Kole avivunje. Naye akashindwa. Vijana kadhaa waliojidai kuwa na nguvu sana wakajaribu mmojammoja kuvunja vile vijiti kumi kwa pamoja. Nao wakashindwa pia.

Mzee Ndumbwi akasimama tena akawaambia, "Mfano huu wa vijiti unatuhusu sisi. Mtoto ameweza kuvunja kijiti kimoja kwa urahisi, lakini ameshindwa kuvunja vijiti kumi. Vijana hawa pamoja na Mzee Kole ni mfano wa ukame. Ni rahisi kwa ukame kumshinda mtu mmojammoja kama ilivyokuwa rahisi kwa mtoto mmoja kuvunja kile kijiti kimoja, lakini ukame hauwezi kuwashinda watu wengi wanaoshirikiana kwa pamoja."

Baada ya mfano huo, Mzee Ndumbwi aliwasisitiza watu wa Kivumbi kushirikiana kama siafu kwa kuwa siafu ni viumbe wadogo, lakini wanaweza kumshambulia, hata kumuua, adui yao. Maelezo yake yaliwapendeza sana wanakijiji.

Siku ileile, watu wa Kivumbi walianza kuweka mikakati ya kukabiliana na tatizo la ukame kijijini humo. Walipatana kuchimba kisima cha kijiji. Kila mtu alitoa kitu alichoweza ili kufanikisha zoezi hilo. Watu wa Kijiji cha Kivumbi walifanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha malengo yao. Baada ya muda, kisima kilikamilika. Maji ya kutosha yakapatikana. Watu wa Kivumbi walifurahi sana kupata maji kwa ajili ya mahitaji yao na ya mifugo yao.

**Maswali**

1. Kijiji cha Kivumbi kilikumbwa na tatizo gani?
2. Nani aliwakusanya watu wa Kijiji cha Kivumbi?
3. Wananchi wa Kivumbi walifanya nini ili kuondokana na tatizo la ukame?
4. Eleza maana ya methali isemayo **umoja ni nguvu**, **utengano ni udhaifu**.
5. Ni nani katika Kijiji cha Kivumbi alikuwa na busara na hekima?
6. Umepata mafunzo gani kutokana na kisa hiki?



KISWAHILI FINAL.indd 101 2021/09/13 12:14

Fot online use only
do not duplicate

**Zingatia**

Ili msomaji aelewe ujumbe uliomo katika maandishi anayosoma, anatakiwa kumakinika kwa lengo la kubaini mawazo makuu. Haya ni yale mambo muhimu yanayoelezwa katika habari. Vilevile, msomaji anapaswa kuzingatia alama za uakifishaji kama vile mkato, nukta, alama ya kuuliza, alama ya mshangao, alama za fungua na funga semi, nuktapacha, mabano, mkwaju, na ritifaa ili asipate tafsiri potofu ya ujumbe wa habari hiyo. Endapo msomaji hatazingatia alama za uakifishaji, anaweza kupotosha maana ya mwandishi. Mathalani, anaweza kuichukulia kauli taarifa kuwa ni swali au mshangao. Aidha, anapaswa kubaini maana ya maneno na misemo mbalimbali. Habari nyingine huwa na maneno ya kisanaa; hivyo, msomaji hana budi kubaini maana za maneno hayo katika muktadha wa habari hiyo ili imsaidie kuelewa vyema maana ya mwandishi.

Kwa kuzingatia hayo yote, msomaji atakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya habari anayoisoma na anaweza kuifupisha.

**Kazi ya 9.7**

**Soma kwa makini habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Kisiwa cha Kobe kipo katika nchi ya Kusadikika. Siku moja, katika kisiwa hicho, ilitokea ajali mbaya sana ya kupinduka na kuzama kwa kivuko cha MV Maendeleo. Kivuko hicho kilikuwa kinafanya kazi ya kusafirisha abiria na mizigo. Kivuko hicho kilipinduka na kuzama mita kadhaa kabla ya kutia nanga. Kilikuwa kikitokea Kisiwa cha Kerebe.

FOR ONLINE USE ONLY

Ajali hiyo ilisababisha vifo vya watu zaidi ya 250 pamoja na upotevu wa mali na mizigo. Watu 100 tu ndio walionusurika katika ajali hiyo. Manusura wa ajali hiyo walisimulia chanzo chake, kila mmoja akisema yake.

Vilio kutokana na ajali hiyo vilitawala nchi nzima. Mkuu wa nchi alitangaza maombolezo ya siku tatu nchi nzima kama sehemu ya kuwakumbuka watu waliopoteza maisha katika ajali ile. Bendera ya nchi hiyo ilipeperushwa nusu mlingoti kama sehemu ya maombolezo.

Wananchi na serikali ya nchi hiyo waliwafariji manusura wa ajali na familia zilizopoteza wapendwa wao. Wananchi na makampuni mbalimbali yalichanga fedha na vitu mbalimbali kama rambirambi kwa wafiwa. Serikali nayo ilitoa kiasi cha fedha kipatacho milioni moja kwa kila familia iliyokumbwa na mkasa huo wa kuwapoteza wapendwa wao.

Miili iliyoopolewa katika ajali ile ilizikwa katika eneo moja. Katika eneo



KISWAHILI FINAL.indd 102 2021/09/13 12:14

Fot online use only
do not duplicate

hilo, serikali ilijenga mnara wa kumbukumbu na kuandika majina ya watu wote waliopoteza maisha katika ajali ile kama sehemu ya kuwakumbuka na kuwaenzi.

Pia, serikali ilichukua hatua ya kuwasimamisha kazi watumishi wa kivuko waliosababisha ajali ile kutokana na uzembe. Baadaye, serikali iliunda tume kuchunguza chanzo cha ajali ile. Mwenyekiti wa Tume alipewa hadidu za rejea. Tume ilianza uchunguzi wake. Tume ilibaini kuwa chanzo cha ajali kilikuwa uzembe wa wafanyakazi wa kivuko kupakia abiria wengi na mizigo kupita uwezo wa kivuko. Kivuko kilikuwa na uwezo wa kubeba abiria 300 na tani 10 za mizigo, lakini siku ya tukio lile kivuko kilibeba abiria 400 na zaidi ya tani 20 za mizigo. Tume ilikabidhi ripoti kwa Mkuu wa nchi.

Baada ya kuipitia ripoti hiyo, mkuu wa nchi aliagiza mamlaka husika kuwachukulia hatua za kisheria wahusika wote. Mamlaka ya Bandari na Usafirishaji iliwachukulia hatua wahusika wote kwa kutoa onyo kwa baadhi ya wafanyakazi na wengine walisimamishwa kazi.

**Maswali**

1. Kisiwa cha Kobe kipo katika nchi gani?
2. Kivuko kilichopinduka na kuzama kiliitwaje?
3. Uzembe uliosababisha kuzama kwa kivuko ulitokana na nini?
4. Serikali ilifanya nini kama ishara ya kuwakumbuka na kuwaenzi watu waliopoteza maisha katika ajali ya kivuko?
5. Unaelewa nini kuhusiana na dhana zifuatazo?
    (a) Kuopoa
    (b) Hadidu za rejea
    (c) Rambirambi
    (d) Manusura
6. Serikali ilichukua hatua zipi mara baada ya ajali ya kivuko?
7. Eleza mafunzo uliyoyapata kutokana na habari hiyo.
8. Fupisha habari uliyoisoma kwa maneno 100.

FOR ONLINE USE ONLY

Fot online use only
do not duplicate

**Zingatia**

Msomaji anapaswa kuelekeza mawazo katika jambo lililoandikwa ili kujibu maswali kutokana na habari aliyoisoma. Ili kujibu vizuri maswali kutokana na habari aliyoisoma, msomaji anatakiwa kusoma kwa makini kila kipengele. Pia, anapaswa kubaini mawazo makuu katika habari na kubaini maana katika maneno, misemo, na sentensi. Vilevile, anapaswa kujibu maswali kama alivyoulizwa kwa kuzingatia alama za uakifishaji na kutilia maanani vidokezo vya maana kulingana na mawazo ya mwandishi. Msomaji anapaswa kueleza mawazo kuhusiana na jambo linalosemwa na mwandishi kwa kujiuliza maswali kadiri anavyosoma pamoja na kuandika ufupisho.

Kufupisha habari iliyosomwa ni kitendo cha kueleza habari hiyo kwa kutumia maneno machache bila kupoteza kiini au lengo la habari hiyo. Aghalabu, habari iliyofupishwa huwa theluthi moja ya habari ya awali. Lengo la ufupisho ni kuwapa wasomaji uwezo wa kupambanua walichokisoma na kukielewa. Hivyo, kufupisha ni kueleza mawazo makuu yaliyomo katika habari kwa maneno mengine bila kuipotosha habari hiyo. Ufupisho ni muhimu kwa sababu husaidia kupima uelewa wa msomaji katika kuchambua mawazo makuu na kuyaandika kwa maneno machache bila kupotosha maana.

Ili kuandika ufupisho mzuri, mwandishi anatakiwa kuisoma habari aliyopewa zaidi ya mara moja ili kupata uelewa wa kutosha na kubainisha mawazo makuu. Vilevile, mwandishi anapaswa kutumia lugha fasaha na yenye mtiririko mzuri wa hoja. Aidha, anapaswa kuzingatia mambo muhimu tu yanayohitajika, huku akitumia maneno yake mwenyewe. Anapofanya hivyo, anapaswa aepuke kupotosha maana ya awali. Aidha, mwandishi anapaswa kuandika sentensi zilizo kamili na kutumia alama za uakifishaji kwa usahihi.

Maandiko yanayoweza kufupishwa ni kama vile ripoti na kumbukumbu za mikutano, madondoo ya hoja katika hotuba au kumbukumbu za kila siku, na habari za matukio mbalimbali.

**Kazi ya 9.8**



**Sikiliza mwanafunzi mwenzako akisoma kwa sauti habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Siku moja, Mtendawema ambaye ni dereva teksi, alipokuwa barabarani, alimwona mtu akiwa anatokwa na damu nyingi. Alikuwa amelala barabarani. Alimsogelea na kumuuliza kuwa ilikuwaje. Alimwambia kuwa alipata ajali. Alikuwa amegongwa na gari alipokuwa anakatiza barabara.



KISWAHILI FINAL.indd 104 2021/09/13 12:14

Fot online use only
do not duplicate

Alimwomba Mtendawema amsaidie kumfunga kitambaa ili kuzuia damu isiendelee kutoka. Mtendawema alimsaidia. Damu haikuendelea kutoka tena. Mtu yule alimshukuru Mtendawema kwa msaada aliompatia.

Mtu yule alimwomba tena Mtendawema amnyanyue ili aende hospitalini kupata matibabu. Mtendawema alimnyanyua na kumweka kwenye gari lake na kumpeleka hospitalini. Walipofika hospitalini, walipokelewa na madaktari na manesi. Walichukua vipimo na kubaini kuwa hakuumia sana. Walimlaza wodini na kumpa matibabu kwa muda. Baadaye, walimruhusu aende nyumbani. Mtendawema alimchukua mtu yule kwa kutumia gari lake hadi nyumbani kwake.

Walipofika nyumbani, Mtendawema alimuaga ili kurejea kwenye shughuli zake. Mtu yule alimshukuru sana kwa msaada mkubwa aliompatia kwa kuwa aliokoa maisha yake. Walipeana namba za simu kwa ajili ya mawasiliano, kisha waliagana, na Mtendawema akaondoka.

Ilipofika saa mbili usiku, mtu yule alimpigia simu Mtendawema akitaka wawe marafiki. Alimwambia kwa kutumia methali isemayo, "Akufaaye kwa dhiki, ndiye rafiki wa kweli." Mtendawema alimkubalia ombi lake. Tangu siku hiyo, mtu huyo na Mtendawema ni marafiki wakubwa. Mpaka sasa, wanashirikiana katika shida na raha.

FOR ONLINE USE ONLY

**Maswali**

1. Bainisha makosa yaliyojitokeza wakati wa usomaji.
2. Fupisha habari hiyo kwa maneno yasiyozidi 80.

**Zoezi la 9.2**

1. Matini zipi zinaweza kufupishwa?
2. Eleza faida za ufupisho.
3. Bainisha hatua za kufuata katika kufupisha habari.
4. Kwa ufupi, fafanua mambo ya kuzingatia wakati wa kufupisha habari iliyosomwa.



KISWAHILI FINAL.indd 105 2021/09/13 12:14

Fot online use only
do not duplicate

## Kusoma kwa burudani

### Kazi ya 9.9

**Soma matini yoyote kwa muda usiozidi dakika ishirini, kisha andika kwa kifupi mambo yafuatayo kutokana na matini hiyo:**

(a) Tarehe uliyosoma matini
(b) Kichwa cha matini
(c) Jina la mwandishi wa matini
(d) Ufupisho usiozidi maneno 100
(e) Fundisho au ujumbe uliopata kutokana na matini uliyoisoma
(f) Jambo lililokuvutia
(g) Maoni yako kuhusiana na matini

### Zingatia

Kusoma kwa burudani ni aina ya usomaji ufanywao kwa lengo la kujifurahisha. Usomaji wa burudani unaweza kuhusisha maandiko kama magazeti, majarida, au vitabu. Ingawa lengo la msomaji ni kujiburudisha, pia hujiongezea maarifa kwa sababu majarida, magazeti, na vitabu huelezea mambo mbalimbali yanayoihusu jamii. Maandiko hayo humwezesha msomaji kujiongezea kiwango cha uelewa wa lugha, ikiwa ni pamoja na kujifunza maneno mapya.

Kuna umuhimu mkubwa kwa msomaji kujijengea tabia ya kujisomea kwa sababu tabia hiyo humwezesha kupima kiwango cha uelewa wa maarifa aliyoyapata. Msomaji anaweza kujipima kwa kujiwekea utaratibu wa kutunza kumbukumbu ya maandiko aliyoyasoma. Kumbukumbu hizo hujumuisha ufupisho wa kila andiko, tarehe aliyosoma, jina la andiko, na jina la mwandishi. Vipengele vingine ni fundisho au ujumbe mkuu, jambo linalomvutia, na mtazamo au maoni yake kwa ujumla. Kama andiko limechapishwa, msomaji aweke kumbukumbu ya jina la mchapishaji na mwaka wa uchapishaji.

### Zoezi la 9.3

1. Kusoma kwa burudani kunaweza kufasiliwa kwa namna gani?
2. Fafanua mambo ya kuzingatia katika kusoma kwa burudani.
3. Usomaji wa burudani una umuhimu gani?
4. Mtu mwenye utamaduni wa kujisomea magazeti, majarida, vipeperushi, na vitabu mbalimbali anapata faida gani?



KISWAHILI FINAL.indd 106 2021/09/13 12:14

Fot online use only
do not duplicate

## Matumizi ya kamusi

### Kazi ya 9.10

**Chunguza ukurasa ufuatao wa kamusi, kisha jibu maswali yanayofuata.**

asubuhi 21 auk.a[4] a

**asubuhi** /asubuhi/ *nm (-) [i-/zi-]* mwanzo wa siku; jua lichomozapo; che; (nh) *~ na mapema.* (>Kar)

**asumini** /asumini/ pia **asmini** /asmini/ *nm (-) [i-/zi-]* ua la mwasumini lichanualo jioni, lenye harufu nzuri ambalo hutumika kutengenezea manukato na kwenye shada la kufunga nywele za wanawake, n.k.; *~ mwitu* afu. (>Kar)

**asusa** /asusa/ *nm (-) [i-/zi-]* kitu chochote k.v. karanga, korosho, nyama iliyochomwa, n.k. kinacholiwa wakati k.v. wa burudani.

**atami.a** /atamija/ *kt [ele]* kalia au lalia mayai kama afanyavyo kuku au ndege ili kuyapa joto mpaka yatotoe. ***~ana, ~ka, ~lia, ~sha, ~wa.***

**ateri** /atɛri/ *nm (-) [i-/zi-]* mshipa unaosambaza damu inayotoka moyoni, mwilini. (>Kng)

**athari** /aθari/ *nm (-) [i-/zi-]* **1** matokeo au alama inayobakia kwa muda baada ya mtu au kitu kufikwa na jambo fulani. **2** hali inayomwambukiza mtu tabia au mazoea yake. **3** jeraha. (>Kar)

**athir.i** /aðiri/ *kt [ele]* **1** tia doa au dosari; jeruhi. **2** shawishi mtu kufanya jambo. ***~ia, ~iana, ~ika, ~isha, ~iwa.*** (>Kar)

**ati!**[1] /ati/ pia **eti!**[1] /ɛti/ *ki* neno la kumfanya mtu asikilize: *~ Juma!*

**ati**[2] /ati/ pia **eti!**[2] /ɛti/ *ki* **1** neno la kuonesha shaka juu ya jambo fulani: *~ kesho sikukuu?* **2** neno la kuonesha dharau: *~ naye anajifanya ni askari.*

**atia**[1] /atija/ *nm (-) [i-/zi-]* kitu apewacho mtu; zawadi. (>Kar)

**atia**[2] /atija/ *nm (-) [i-/zi-]* neema anayojaaliwa mtu kuwa nayo; kipawa. (>Kar)

**atib.u** /atibu/ *kt [ele]* toa makosa; laumu, kengemeka, shutumu, aili. ***~ia, ~iana, ~ika, ~isha, ~iwa.*** (>Kar)

**atifali** /atifali/ *nm (-) [wa-]* (ksh) watoto wadogo. (>Kar)

**atik.a** /atika/ *kt [ele]* ng'oa mmea k.v. mche wa mnazi au mchungwa, na kuupanda mahali pengine; pandikiza, kitia. ***~ia, ~iana, ~ika, ~isha, ~wa.***

**atil.i** /atili/ *kt [ele]* poteza, haribu: *Wakati ni mali, si vizuri kuu~.* ***~ia, ~iana, ~ika, ~isha, ~iwa.*** (>Kar)

**atilik.a** /atilika/ *kt [sie]* **1** pata jeraha au kilema kutokana na ajali au ugonjwa. **2** fujika kwa kitu kutokana na kutotumika. ***~ia, ~ika, ~isha.*** (>Kar)

**Atlantiki** /atlantiki/ *nm (-) [i-]* bahari kubwa ya pili duniani iliyopo baina ya pwani za Ulaya na Afrika upande wa mashariki na Amerika Kaskazini na Amerika Kusini upande wa magharibi. (>Kng)

**atlasi**[1] /atlasi/ *nm (-) [i-/zi-]* namna ya nguo laini inayong'aa. (>Kar)

**atlasi**[2] /atlasi/ *nm (-) [i-/zi-]* kitabu cha ramani. (>Kng)

**atomiki** /atɔmiki/ *kv* -enye atomu: *Bomu la ~.* (>Kng)

**atomu**[1] /atɔmu/ *nm (-) [i-/zi-]* chembe ndogo kabisa ya kitu chochote. (>Kng)

**atomu**[2] /atɔmu/ *nm (-) [i-/zi-]* (fiz) sehemu ndogo ya elementi yenye chaji hasi na inayozunguka kiini katika mzunguko maalumu. (>Kng)

**atu.a** /atuwa/ *kt [ele]* shtua, agh. kwa taarifa ya kutisha k.v. kifo: *Habari ya kifo chake imeni~ moyo.* ***~ana, ~lia, ~lika, ~lisha, ~liwa.***

**au** /awu/ *ku* neno la kuonesha jambo mojawapo kati ya mawili yaliyohusika; ama: *Chukua hiki ~ kile.* (>Kar)

**au.a**[1] /awuwa/ *kt [ele]* **1** chunguza kwa makini; kagua. **2** fuata kwa makini: *~ nyayo.* ***~lia, ~liana, ~lika, ~lisha, ~liwa.***

**au.a**[2] /awuwa/ *kt [ele]* weka mipaka; pima shamba: *~ shamba.* ***~lia, ~liana, ~lika, ~lisha, ~liwa.***

**au.a**[3] /awuwa/ *kt [ele]* toa matunda; zaa. ***~lia, ~lika, ~lisha, ~liwa.***

**auk.a**[1] /awuka/ *kt [sie]* shika moto kwa kuni au makaa: *Makaa yame~.* ***~ia, ~ika, ~isha.***

**auk.a**[2] /awuka/ *kt [sie]* fika muda maalumu uliowekwa: *Asha amesha~ arubaini* ameshafikisha siku arubaini tangu ajifungue. ***~ia, ~ika, ~isha.***

**auk.a**[3] /awuka/ *kt [ele, sie]* endeleza, stawisha. ***~ia, ~iana, ~ika, ~isha, ~iwa.***

**auk.a**[4] /awuka/ *kt [ele, sie]* (kwa mimea) fika kiwango cha kutoa matunda. ***~ia, ~iana, ~ika, ~isha, ~iwa.***

FOR ONLINE USE ONLY

**Kielelezo Namba 9.1:** *Ukurasa wa kamusi*

**Chanzo:** TUKI (2013:21).

Fot online use only
do not duplicate

**Maswali**

1. Bainisha maneno 10 yaliyopo katika ukurasa wa kamusi yaliyoandikwa kwa wino mkozo na rangi maalumu.
2. Kwa kutumia kielelezo ulichopewa, eleza maana za maneno uliyoyataja.
3. Kwa kila neno ulilolitaja katika swali la kwanza, andika ni aina gani ya neno.

**Zingatia**

Kamusi ni kitabu cha rejea chenye orodha ya maneno kutoka lugha moja yaliyoandikwa kwa mpangilio wa kialfabeti (**A** - **Z**) na kila moja kutolewa ufafanuzi wa maana zake kwa lugha hiyohiyo au kwa lugha nyingine. Katika kamusi, huingizwa **vidahizo** na **vitomeo**.

Vidahizo ni maneno yaliyoorodheshwa kialfabeti (**A** - **Z**) na kuandikwa kwa wino uliokozwa. Wakati mwingine, huandikwa kwa rangi maalumu. Vidahizo huingizwa katika kamusi ili vitolewe ufafanuzi ambao hujumuisha maana (fasili), kategoria za maneno, matamshi, ngeli za nomino, tahajia, etimolojia, mtindo, na mifano ya matumizi. Neno la kwanza na la mwisho katika ukurasa huchapwa katika sehemu ya juu ya ukurasa ili kumwongoza msomaji atambue lilipo neno analolitafuta, iwapo lipo katika ukurasa anaousoma, wa mbele, au wa nyuma yake. Kwa mfano, katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, *Toleo la 3* (TUKI, 2013), kidahizo cha kwanza ni **aa!** Kidahizo cha mwisho ni **zuzuwa.a**.

Vitomeo ni vidahizo pamoja na taarifa zake zote anazohitaji mtumiaji wa kamusi. Kwa mfano, katika Kielelezo Namba 9.1, neno **athari** pamoja na taarifa zake zote ni kitomeo.

Kamusi huwa na dhima mbalimbali. Dhima mojawapo ni kudokeza taarifa mbalimbali za kisarufi kama vile aina za maneno (nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi, viwakilishi, viunganishi, vihisishi, na vihusishi) na ngeli za nomino ambazo hujipambanua katika umbo la umoja na wingi. Aghalabu, vidahizo huandikwa katika umoja. Wingi huoneshwa katika mabano duara. Tazama mfano ufuatao:

**kigoda** /kigɔda/ nm (vi-) [ki- /vi-] kiti kidogo agh. cha miguu mitatu, kisichokuwa na kiegemeo.

Umbo (vi-) katika mfano huo linaonesha wingi wa neno **kigoda** ambao ni **vigoda**.

Hali kadhalika, kamusi huonesha mifano ya matumizi ya neno husika kama vile kutumiwa katika methali, misemo, na nahau. Kwa mfano, **Akufaaye kwa ~ ndiye rafiki wa kweli** (*methali*). Methali hii hutumiwa kuonesha matumizi ya neno dhiki ambalo nafasi yake huoneshwa kwa alama ya wimbi (~). Mbali na matumizi ya kimethali na kimisemo, kamusi huonesha jinsi neno linavyotumika



KISWAHILI FINAL.indd 108 2021/09/13 12:14

Fot online use only
do not duplicate

katika muktadha halisi. Katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, mifano ya matumizi ya namna hii imeingizwa baada ya maelezo ya maana. Maelezo hayo yamefuatiwa na nukta mbili (:) na kuandikwa kwa hatimlazo (italiki). Tazama mfano ufuatao:

**pangan.a** /pangana/ kt kaa mahali kwa utaratibu fulani: *Watu wame~ getini wakisubiri kuingia uwanjani.*

Vilevile, kamusi hutumika kuonesha mnyambuliko wa vitenzi. Baada ya maelezo ya maana, mnyumbuliko wa kitenzi hubainishwa kwa kutumia alama ya wimbi ikifuatiwa na viambishi nyambulishi. Tazama mfano ufuatao:

**chez.a** /tʃɛza/kt fanya mambo kujiburudisha: *ana~*, *~ea*, *~eana*, *~eka*, *~esha*, *~ewa*, *~wa*.

Pia, kamusi hutumika kuonesha maana za maneno ya lugha ambayo ndiyo msamiati wa lugha inayohusika. Ili kuweza kubaini maana za maneno ya lugha, mtumia kamusi anapaswa kuangalia vitomeo. Aidha, anatakiwa azingatie mpangilio wa alfabeti kwa kuanza na herufi inayotangulia na inayofuatia ili kubaini kwa urahisi mahali kilipo kidahizo kinachotafutwa.

Zaidi ya hayo, kamusi huonesha matamshi ya maneno (vidahizo). Matamshi haya huoneshwa kwa kutumia alama za kifonolojia ambazo ni alama za mikwaju (/ /). Tazama mifano ya matamshi ya maneno yafuatayo:

**kebo** /kɛbɔ/

**chakula** /tʃakula/

**shule** /ʃulɛ/

**gavana** /gavana/

**geugeu** /gɛwugɛwu/

FOR ONLINE USE ONLY

Kwa kuonesha matamshi, kamusi humsaidia mtumiaji kujua namna ya kutamka maneno anayotafuta katika kamusi. Matamshi hayo humsaidia mjifunzaji wa lugha kuwa na umilisi katika sarufi ya lugha, hususani katika uwanja wa fonolojia.

**Zoezi la 9.4**

1. Fasili dhana ya kamusi.
2. Kwa nini maneno katika kamusi hupangwa kialfabeti?
3. Eleza matumizi ya kamusi.
4. Kwa kutumia kamusi, eleza maana za maneno yafuatayo:

   (a) pongoo
   (b) utandawazi
   (c) utengemano
   (d) maadili
   (e) vurumai
   (f) maadhura

Fot online use only
do not duplicate

(g) wakaa

(h) karantini

(i) mrakibu

**Kazi ya 9.11**

1. Panga maneno yafuatayo kialfabeti kama yanavyopangwa katika kamusi.

mwanafasihi, mwanaharamu, mwanagenzi, mwanahewa, mwanajeshi, mwanajamii, mwanajopo, mwanaanga, mwananchi

shadda, shaha, shaka, shahada, shahidi, shadidi, shairi, shahibu, shajara

kubuhu, kubwa, kucha, kudu, kuku, kuli, kudu, kumbakumba, kumbuka

chaguo, chai, chaji, chuki, chakacha, chaka, choo, chakula, chambo, chaki, chale

## Zoezi la marudio la 9

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

FOR ONLINE USE ONLY

(i) Jambo gani la msingi hupimwa katika ufahamu wa kusoma kwa sauti?

(a) Uulizaji wa maswali

(b) Kutamka maneno inavyotakiwa

(c) Matini

(d) Maswali ya kweli au si kweli

(e) Majarida

(ii) Fasili ya kiimbo ni ………….

(a) hali ya kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti ya lugha katika utamkaji wa maneno

(b) utamkaji wa nguvu zaidi katika sehemu fulani ya neno

(c) jinsi ya kuandika silabi

(d) hali ya kuelewa na kutambua maana ya jambo

(e) kusoma maandishi na kusikiliza sauti za wazungumzaji

Fot online use only
do not duplicate

(iii) Fasili ya matamshi katika kusoma kwa sauti ni …………..

(a) utenganishaji wa silabi

(b) namna ya kutamka silabi au maneno ya lugha

(c) taratibu na kanuni mbalimbali za uandishi katika lugha

(d) utamkaji wa nguvu zaidi katika sehemu fulani ya neno

(e) usomaji mzuri unaofuata mtiririko wa aya

(iv) Miongoni mwa mambo ya kuzingatia katika kufupisha habari kwa mdomo ni ………….

(a) mtiririko wa mazungumzo

(b) alama za uandishi

(c) wazo kuu

(d) kuzungumza kwa sauti

(e) kuwa makini na kinachosemwa

(v) Lipi si jibu sahihi kati ya yafuatayo kuhusu ufahamu wa kusoma kwa sauti?

(a) Kutamka maneno inavyotakiwa

(b) Kuzingatia alama za uandishi

(c) Kusoma kwa kufuata mtiririko

(d) Kusoma bila kutoa sauti

(e) Kuzingatia nguvu ya utamkaji wa neno.

FOR ONLINE USE ONLY

Fot online use only
do not duplicate

2. Oanisha maelezo yaliyopo fungu A na dhana zilizoko fungu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi ili kukamilisha maana.

| Fungu A | Fungu B |
|---|---|
| (i) Uelewa unaopatikana kwa njia ya kusoma. | A. usomaji wa kina |
| (ii) Aina ya usomaji ambao humwezesha msomaji kupata ujumbe na kutamka kwa lafudhi ya Kiswahili sanifu. | B. kusoma kwa sauti |
| (iii) Kusoma habari pasipo kutamka maneno kwa sauti. | C. kusoma kimya |
| (iv) Humwezesha msomaji kusoma maandishi mengi kwa muda mfupi na kupata anachokihitaji. | D. ufahamu wa kuona |
| (v) Msomaji huzingatia maana za maneno, sentensi, na aya ambazo hubeba mawazo makuu ya mwandishi. | E. usomaji wa juujuu |
| | E. usomaji wa burudani |
| | G. ufahamu wa kusoma |

FOR ONLINE USE ONLY

3. Fafanua mambo ya kuzingatia katika kujibu maswali ya ufahamu wa kusoma.
4. Eleza tofauti kati ya kusoma kimya na kusoma kwa sauti.
5. Kusanya maneno kumi kutoka kwenye mazingira yanayokuzunguka, kisha tumia kamusi kuonesha matamshi, kueleza maana zake, na kutoa mifano ya matumizi yake.
6. Tunga sentensi moja kwa kila neno ulilolikusanya katika swali namba 5.
7. Bainisha mambo ya kuzingatia wakati wa kutafuta maana za maneno kwenye kamusi.



KISWAHILI FINAL.indd 112 2021/09/13 12:14

For online use only
do not duplicate

## Faharasa

| | |
|---|---|
| **Aghalabu** | mara kwa mara, kwa kawaida, mara nyingi |
| **Audiorekoda** | kifaa cha kurekodia sauti kwa njia ya kieletroniki |
| **Baruapepe** | ujumbe unaotumwa kwa njia ya kidijiti kupitia kompyuta au simu inayounganishwa kwenye mfumo wa mtandao wa intaneti |
| **Dayalojia** | mazungumzo ya kupokezana kati ya pande mbili au zaidi |
| **Dhamira** | kipengele cha kimaudhui katika kazi ya fasihi ambacho hueleza lengo la kazi hiyo |
| **Falsafa** | imani ya mtunzi kuhusu ukweli wa maisha |
| **Fanani** | msanii katika fasihi simulizi; mtu anayesimulia hadithi |
| **Fasili** | maelezo ya maana ya neno |
| **Fonolojia** | ni taaluma ambayo hushughulikia sauti za lugha mahususi |
| **Irabu** | aina ya sauti ya lugha inayotamkwa bila kuwapo kikwazo chochote kwenye mkondo wa hewa kutoka mapafuni kupitia kinywani |
| **Kidahizo** | neno kuu katika kamusi ambalo huingizwa kwa rangi iliyokoza na kutolewa fasili na taarifa mbalimbali |
| **Kiimbo** | namna ya usemaji ambapo sauti hupanda na kushuka wakati wa kuzungumza |
| **Kikokotozi** | kifaa kinachotumika kupigia hesabu |
| **Kipashio** | sehemu ya tungo inayounda au kuundwa na tungo nyingine ikiwa na kazi bainifu ya kisarufi |
| **Kitomeo** | kidahizo kinachoingizwa kwenye kamusi kikiwa na maelezo yake |
| **Konsonanti** | sauti ambayo hutamkwa kwa kubana au kuzuia mkondohewa kutoka mapafuni kwenda nje kupitia ama chemba ya kinywa au chemba ya pua |
| **Lafudhi** | namna mtu au jamii ya watu inavyotamka maneno ya lugha wanayoitumia |
| **Lahaja** | tofauti za matamshi, maumbo, na matumizi ya maneno baina ya jamii za wazungumzaji wa lugha yenye asili moja |
| **Majigambo** | sanaa ya kutoa maneno ya kujisifia au kujikweza |
| **Makinika** | kuwa makini |

FOR ONLINE USE ONLY



KISWAHILI FINAL.indd 113 2021/09/13 12:14

Fot online use only
do not duplicate

| | |
|---|---|
| **Maleba** | mavazi maalumu yanayovaliwa na wasanii wanapofanya maonyesho mbalimbali |
| **Mandhari** | mahali ambapo matukio ya kifasihi hutendeka |
| **Manusura** | aliyesaidika au aliyepona kwa bahati |
| **Mathalani** | kiunganishi ambacho hutumika katika utoaji wa mifano |
| **Misimu** | maneno yanayozuka na kutumiwa na watu kwa muda fulani na baadaye kupotea au kusanifishwa |
| **Mizani** | idadi ya silabi katika mshororo wa kazi ya ushairi |
| **Mkazo** | utamkaji wa nguvu zaidi wa silabi mojawapo ya neno |
| **Mnyambuliko** | uzalishaji wa neno kutokana na kuweka viambishi kwenye kiini cha neno |
| **Mofimu** | kipashio kidogo dhahania cha kisarufi kinachowakilisha maana katika neno, kihifadhiwacho ndani ya mofu |
| **Mofu** | umbo linalowakilisha mofimu |
| **Mshororo** | mstari mmojawapo kwenye kila ubeti wa kazi ya ushairi |
| **Muktadha** | mazingira yanayobainisha mahali jambo lilipofanyika |
| **Muwala** | mtiririko mzuri wa mawazo kimantiki katika kazi ya fasihi |
| **Mzizi** | umbo la msingi la neno ambalo ndilo kiini cha neno kisichobadilika na kisichogawanyika zaidi |
| **Ombwe** | uwazi unaokuwapo mahali fulani |
| **Opoa** | toa kitu kilicho ndani ya kitu cha majimaji |
| **Rejesta** | mtindo wa lugha unaotumika mahali penye shughuli fulani |
| **Shadidia** | sisitiza jambo fulani |
| **Silabi** | kipashio kidogo kabisa cha kimatamshi kinachoundwa na konsonanti na irabu au irabu peke yake ambacho hutamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti |
| **Sitiari** | tamathali ya usemi yenye kuhusisha vitu viwili vyenye sifa zinazofanana |
| **Sitiri** | hifadhi jambo au kitu ili kisionekane |
| **Takhmisa** | shairi lenye mishororo mitano kwa kila ubeti |
| **Takriri** | hali ya kurudiwarudiwa kwa umbo la neno, silabi, au fungu la maneno |



KISWAHILI FINAL.indd 114 2021/09/13 12:14

Fot online use only
do not duplicate

| | |
|---|---|
| **Tanbihi** | maelezo yanayotolewa sehemu ya mwisho au chini ya ukurasa au sura kwa ajili ya kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu hoja fulani iliyozungumziwa awali ndani ya ukurasa au sura hiyo |
| **Tarbia** | shairi la mishororo minne kila ubeti |
| **Tashihisi** | usemi wenye kukipa sifa ya uhai kitu kisichokuwa na uhai |
| **Taswira** | picha inayomjia au anayoiwaza mtu akilini mwake |
| **Tathinia** | shairi lenye mishororo miwili kila ubeti |
| **Tathlitha** | shairi lenye mishororo mitatu kila ubeti |
| **Tathmina** | shairi lenye mshororo mmoja kila ubeti |
| **Tepurekoda** | kifaa cha kurekodi mawimbi ya sauti kwenye tepu au kanda |
| **Uakifishaji** | uwekaji wa alama za uandishi kama vile nukta na mkato katika maandishi |
| **Ubeti** | kifungu cha mishororo katika kazi ya ushairi |
| **Umahiri** | uhodari au ustadi wa kufanya jambo fulani |
| **Umilisi** | maarifa na ujuzi anaokuwa nao mtu kwenye taaluma au fani fulani |
| **Urari** | ulinganifu au usawa |
| **Wimbi** | alama ya uandishi yenye mstari wa matao inayotumiwa kuepusha marudio ya kidahizo katika kamusi (~) |

FOR ONLINE USE ONLY

# Bibliografia


Abedi, A.K. (1954). *Sheria ya Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Akilimali, K.H.A. (1974). *Diwani ya Akilimali.* Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Baraza la Kiswahili la Taifa (2017). *Mwongozo kwa Waandishi wa Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: TUKI na BAKITA.

Giuseppe, N. Wimbo wa Mazingira. ulinakiliwa tarehe 19.2.2021 katika https://www.youtube.com/watch?v=Uo-jJ2Wf4uM(19.2.2021)

Kihore,Y.M., Massamba, D.P.B. & Msanjila, Y.P. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (*SAMAKISA*): *Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (1983). Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili, katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*: *Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M. & Msanjila, Y.P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA): Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TUKI.

Mbijima, R.J. (2020). *Uduni Wangu*: *Ngonjera za Watoto*. Dar es Salaam: Seromercy Publishing Company Limited

Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mlyauki, J., Mulashan, E. & Ndilime, D. (2009). *Kiswahili Kitukuzwe 4*: *Kidato cha Nne Kitabu cha Mwanafunzi*. Malaysia: Pearson Education Ltd.

Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha.* Dar es Salaam: EPD.

Mulokozi, M.M. & Kahigi, K.K. (1982). *Kunga za Ushari na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: TPH.

Njege, S. (2013). *Jiandae Ufaulu Kiswahili Kidato cha 3 & 4*. Dar es Salaam: Oxford University Press.




KISWAHILI FINAL.indd 116 2021/09/13 12:14

Fot online use only
do not duplicate

Njogu, K. & Nganje, D.K. (2006). *Kiswahili kwa Vyuo vya Ualimu*. Nairobi: The Jomo Kenyata Foundation.

Njogu, K. & Chimerah, R. (2008). *Nadharia na Mbinu*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Nkwera, F.M.V. (1978). *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TPH.

Nuru, S.M. (1975). *Johari za Kiswahili - 15 Mtango wa Kiswahili.* Dar es Salaam: General Printers Limited.

Taasisi ya Elimu Tanzania (1996). *Kiswahili Kidato cha Pili: Kitabu cha Mwanafunzi.* Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2019). *Kiswahili Shule za Sekondari: Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita*: *Lugha na Sarufi.* Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2019). *Kiswahili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita*: *Fasihi.* Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu,* Toleo la 3. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Tanzania (1986). *Kiswahili Sekondari.* Dar es Salaam: KIUTA.

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Tanzania (1992). *Kiswahili Vyuoni.* Dar es Salaam: KIUTA.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2005). *Muhtasari wa Kiswahili wa Shule za Sekondari Kidato cha I - IV*. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Wizara ya Elimu na Utamaduni (1974). *Tujifunze Lugha Yetu: Kitabu cha Sita.* Dar es Salaam: Tanzania Litho.

FOR ONLINE USE ONLY

ISBN 978-9987-09-268-0
9 789987 092680